# KANUNI ZA KIKRISTO

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki © 2023 Shepherds Global Classroom
Imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kutoka katika Toleo la Tatu la Kiingereza.
Inapatikana kwa upakuaji bila malipo kwenye https://www.shepherdsglobal.org/downloads

Kozi hii inapatikana chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 (CC BY-NC-ND 4.0) isipokuwa pale ambapo imebainishwa vinginevyo.
https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/

Kozi hii inaweza kunakiliwa na kusambazwa bila malipo katika muundo wa kuchapishwa na wa kidijitali lakini haipaswi kubadilishwa kwa njia yoyote na haiwezi kuuzwa kwa faida (ingawa gharama za uchapishaji zinaweza kutozwa). Taasisi za elimu ziko huru kutumia/kunakili kozi hii hata kama zinatoza ada ya masomo. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea www.shepherdsglobal.org/copyright

Nyenzo za wahusika wengine ni hakimiliki ya wamiliki husika na zinashirikiwa chini ya leseni mbalimbali.

Isipokuwa iwe imetajwa vinginevyo, maandiko yote yametoka katika Biblia ya SUV (Swahili Union Version), ya Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania. Imetumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

Baadhi ya nyenzo za kozi hii zimetolewa kutoka katika kitabu kinachoitwa I Believe, kilichoandikwa na wahadhiri wa God’s Bible School and College, huko Cincinnati, Ohio.

Mwandishi mkuu: Dkt. Stephen K. Gibson

# YALIYOMO

MUHTASARI WA KOZI 5
1. KITABU CHA MUNGU 9
2. SIFA ZA MUNGU 23
3. UTATU WA MUNGU 33
4. UBINADAMU 43
5. DHAMBI 53
6. ROHO 63
7. KRISTO 73
8. WOKOVU 87
9. MASUALA YA WOKOVU 99
10. ROHO MTAKATIFU 113
11. UTAKATIFU WA KIKRISTO 125
12. KANISA 139
13. HATIMA YA MILELE 149
14. MATUKIO YA MWISHO 157
15. KANUNI ZA IMANI ZA KALE 167
NYENZO ZINAZOPENDEKEZWA 177
REKODI YA MAZOEZI 180
MAREJEO YA MAANDIKO 181
FARAHASA 184

# MUHTASARI WA KOZI

## MAELEZO YA KOZI

Kozi hii inatoa ufahamu wa kanuni za msingi katika kila kimoja cha vitengo vikuu vya theolojia ya Kikristo, kama vile Mungu, Kristo, dhambi, wokovu, na kanuni zingine kuu. Mwanafunzi atajifunza jinsi ya kuepuka makosa katika kanuni. Mwanafunzi ataandaliwa kuwafundisha wengine kanuni za Kikristo.

## MALENGO YA KOZI

1. Kujifunza kanuni za msingi za imani ya Kikristo.
2. Kutumia Biblia ipasavyo kama chanzo na mamlaka ya kanuni.
3. Kutambua makosa makuu katika kanuni.
4. Kupata ufahamu unaosaidia kuimarisha uhusiano wetu na Mungu.
5. Kupokea maudhui na muundo wa kufundisha wengine.

## MAELEKEZO KWA AJILI YA VIONGOZI WA DARASA

Maelekezo haya yanaeleza jinsi darasa linavyoweza kufundishwa kwa kiwango cha juu zaidi cha ubora. Kiongozi wa darasa lazima azingatie kiwango hiki kwa ajili ya wanafunzi wanaopokea cheti kutoka kwa Shepherds Global Classroom au washirika wake. Kwa aina zingine za vikundi ambavyo haviwezi kutimiza viwango hivi, mwalimu anaweza kurekebisha viwango kulingana na uwezo wa kikundi husika na kutoa cheti tofauti.

Tunakadiria kuwa somo moja litachukua dakika 90 au zaidi. Inaweza kuwa bora kwa kikundi kukutana mara mbili kwa kila somo. Ikiwa kikundi kitakutana mara mbili, baadhi ya maelekezo lazima yarekebishwe. Kwa mfano, hakutakuwa na mtihani katika mikutano yote miwili.

Kila mwanafunzi anahitaji nakala ya kitabu hiki.

Vidokezo kwa ajili ya viongozi wa darasa vimejumuishwa katika kozi yote pamoja na maelekezo ya sehemu mahususi za masomo. *Vimeandikwa kwa mwandiko wa mlazo*.

Mwanzoni mwa kipindi cha darasa, peana **mtihani** wa somo la awali. Kila mwanafunzi lazima ayaandike majibu kutoka kwenye kumbukumbu yake bila msaada wowote. Ikiwa mwanafunzi hataweza kupita mtihani, unaweza kumruhusu ajaribu tena wakati mwingine (muda uliokadiriwa: dakika 10). Majibu ya mtihani yanaweza kupakuliwa kutoka kwenye ShepherdsGlobal.org.

Baada ya mtihani, tumia orodha ya malengo ya somo la awali kama maswali ya mapitio. Uliza swali kwa kila lengo na uwaruhusu wanafunzi waeleze (muda uliokadiriwa: dakika 15).

Anza somo jipya kwa kumwomba mwanafunzi asome kifungu kilichotolewa. Wape wanafunzi nafasi wajadili kwa ufupi kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo (muda uliokadiriwa: dakika 10).

Pitia maudhui ya somo kwa kusoma na kufafanua kila sehemu. Washiriki wa darasa wanaweza kufundisha baadhi ya sehemu (muda uliokadiriwa: dakika 45).

**Maandiko** mengi yametumiwa katika kozi hii. Marejeo ya Maandiko yaliyotolewa kwenye mabano yenye neno *soma* yanapaswa kusomwa kwa sauti darasani. Marejeo mengine ya maandiko yanatumika tu kuunga mkono kauli zilizo katika maudhui. Si lazima kila mara kuangalia au kusoma vifungu hivyo darasani.

**Maswali ya majadiliano** na **mazoezi ya darasani** yanaonyeshwa kwa vishale. Wakati mwingine maswali ya majadiliano hutanguliza sehemu; wakati mwingine yanapitia sehemu iliyoangaziwa awali. Kiongozi wa darasa anapaswa kuuliza swali na kuwapa wanafunzi muda wa kujadili jibu. Si lazima kueleza kikamilifu jibu wakati huo, hasa ikiwa swali linatanguliza sehemu.

Darasa linapaswa kusoma **"Kauli ya Imani"** pamoja mara mbili mwishoni mwa kila somo.

Mwishoni mwa kila somo, kila mwanafunzi anapaswa kupewa kifungu cha maandiko kutoka kwenye orodha iliyotolewa. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, wanapaswa kusoma kifungu hicho na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada husika. Wanapaswa kumwonyesha kiongozi wa darasa aya hiyo katika kipindi kitakachofuata.

Angalau mara tatu wakati wa kozi hii, mwanafunzi anapaswa kuwafundisha watu wasioshiriki katika darasa lake somo moja nzima au sehemu ya somo. Hili linaweza kufanywa katika darasa kanisani, kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani, au katika mazingira mengine. Mwishoni mwa kila kipindi cha darasa, wakumbushe wanafunzi kuhusu zoezi hili, na uwape nafasi ya kutoa ripoti ikiwa wamefundisha chochote tangu kipindi cha mwisho cha darasa.

Mwishoni mwa darasa, wakumbushe wanafunzi kusoma maudhui ya somo linalofuata kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa (muda uliokadiriwa wa matangazo na mazoezi: dakika 10).

Ikiwa mwanafunzi anataka **kupata cheti kutoka kwa Shepherds Global Classroom au mmoja wa washirika wake**, anapaswa kuhudhuria vipindi vya darasa na kukamilisha mazoezi. Mwanafunzi akikosa darasa, anapaswa kusoma somo alilokosa, afanye mtihani na afanye zoezi la kuandika. Fomu itatolewa mwishoni mwa kozi kwa ajili ya kurekodi mazoezi yaliyokamilishwa.

## MAELEKEZO KWA WANAFUNZI

Unapaswa kusoma maudhui ya kila somo kabla ya darasa kukutana, ili uweze kushiriki katika majadiliano ukiwa na uelewa bora zaidi.

Mwanzoni mwa kila kipindi cha darasa, jitayarishe kufanya mtihani wa somo la awali. Chunguza maswali ya mtihani yaliyotolewa.

Njoo siku zote na Biblia, nakala iliyochapishwa ya somo husika, na kalamu ya wino kwa ajili ya kuongeza vidokezo vyako mwenyewe kwenye maudhui.

Kuwa tayari kutafuta marejeo ya maandiko, kujibu maswali ya majadiliano, na kushiriki jinsi kiongozi wa darasa anavyoelekeza.

Mwishoni mwa kila somo, utapewa kifungu cha maandiko. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, soma kifungu na uandike aya kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo. Mwonyeshe kiongozi wa darasa aya hiyo.

Angalau mara tatu wakati wa kozi hii unapaswa kuwafundisha watu wasioshiriki katika darasa lako somo moja nzima au sehemu ya somo. Mafundisho haya yanaweza kutekelezwa katika darasa kanisani, kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani, au katika mazingira mengine. Toa ripoti kwa kiongozi wa darasa kila wakati unapomfundisha mtu.

## SOMO LA 1

# KITABU CHA MUNGU

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Dhana ya Ufunuo wa Jumla na Ufunuo Maalum.
    - Ushahidi kwamba Biblia ni Neno la Mungu.
    - Uhamasisho wa maandiko.
    - Kwa nini uhamasisho wa maandiko unamaanisha kuwa maandiko hayana makosa.
    - Maneno *iliyohamasishwa*, *isiyoweza kuwa na makosa*, na *isiyokuwa na makosa*.
    - Kwa nini Biblia imekamilika na haiwezi kuongezewa habari za ziada.
    - Jinsi Biblia ilivyo chanzo kikuu na mamlaka ya mwisho ya kanuni.
    - Jinsi Biblia ilivyo muhimu katika maisha ya kila siku ya Mkristo.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu Biblia.

2. Mwanafunzi ataepuka kusikiliza mamlaka yasiyofaa au kujifunza Biblia akiwa na kusudi finyu.

## UTANGULIZI

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Kwa kawaida kipindi kitaanza na mtihani juu ya somo la awali na mapitio ya malengo ya somo la awali. Kwa kuwa hili ni somo la kwanza, nenda kwenye maandiko yaliyo hapa chini.*

» Someni Zaburi 119:1-16 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu Biblia?

Mungu, Muumba wa ulimwengu, amenena. Amejifunua mwenyewe na kusudi la uumbaji wake. Ukweli ambao Mungu ametufunulia unaitwa ufunuo. Kuna kitabu katika Biblia kinachoitwa “Ufunuo,” lakini neno *ufunuo* linaweza pia kutumika kwa ajili ya ukweli wote ambao Mungu amefunua.

» Je, baadhi ya njia ambazo Mungu ametumia kutufunulia ukweli ni zipi?

## AINA MBALIMBALI ZA UFUNUO

Kwa sababu Mungu amefunua ukweli kwa njia tofauti, tunazungumza kuhusu aina mbili: Ufunuo wa Jumla na Ufunuo Maalum.

### Ufunuo wa Jumla

**Ufunuo wa Jumla ni kile ambacho Mungu ametuonyesha kuhusu yeye mwenyewe kupitia uumbaji wake**. Tunaona akili na uwezo wa ajabu wa Mungu katika muundo wa ulimwengu.

Uumbaji wa juu zaidi wa Mungu ni mwanadamu. Tunajifunza mambo fulani kumhusu Mungu tunapotazama jinsi watu wameumbwa. Ukweli kwamba tunaweza kufikiri, kuvutiwa na umaridadi, na kutofautisha mema na mabaya (ingawa si kwa njia kamili) unatuonyesha kwamba ni lazima Muumba wetu ana uwezo huo kwa kiwango cha juu zaidi. Tunajua kwamba Mungu lazima awe mtu anayeweza kufikiri na kuwasiliana kwa sababu sisi tuna uwezo huo.

Kwa sababu Ufunuo wa Jumla unatuonyesha kwamba Mungu anaweza kunena, tunatambua kwamba Ufunuo Maalum unaweza kutokea. Kwa sababu Mungu anaweza kunena, inawezekana kwamba kuna jumbe kutoka kwa Mungu na hata kitabu kutoka kwa Mungu.

Kupitia Ufunuo wa Jumla, watu wanajua kwamba kuna Mungu, kwamba wanapaswa kumtii, na kwamba tayari wamemwasi. (Soma Warumi 1:20-21.) Lakini Ufunuo wa Jumla hautuelezi jinsi ya kuingia katika uhusiano sahihi na Mungu. Ufunuo wa Jumla unatuonyesha umuhimu wa Ufunuo Maalum kwa sababu unaonyesha kwamba watu ni wenye dhambi na hawana kisingizio mbele za Muumba wao, lakini hautuambii suluhu.

### Ufunuo Maalum

**Mungu alitupa Ufunuo Maalum kupitia maandiko yaliyohamasishwa na kupitia Yesu, Mwana wake**. Ufunuo Maalum unaeleza hali ambayo Ufunuo wa Jumla unaonyesha kuwa ndio hali yetu: tumeanguka na tuna hatia. Ufunuo Maalum unaeleza Mungu, unaeleza Anguko na dhambi, na unaonyesha njia ya kupatanishwa na Mungu.

Fikiria kama hungejua kwamba kuna Biblia. Unatambua kwamba kuna Mungu. Unajua

> “Siamini kwamba mtu yeyote anaweza kuhubiri Injili bila kuhubiri Sheria. Ukishusha Sheria utakuwa unafifisha nuru ambayo kwayo mwanadamu anaona hatia yake.”
>
> Charles Spurgeon

kwamba kuna tatizo kati yako na Mungu. Hujui ni nini kitatokea baada ya kifo. Hujui kusudi la maisha. Hujui jinsi ya kumkaribia Mungu.

Kisha fikiria kwamba mtu fulani anakuonyesha kitabu na anakuambia kwamba kimetoka kwa Mungu ili kujibu maswali hayo. Je, unaweza kufikiria jinsi kitabu hicho kingekuwa cha thamani?

## DAI LA BIBLIA

» Biblia inadai nini kujihusu? Toa mifano kadhaa ya kauli za Biblia zinazoonyesha kwamba inadai kuwa imetoka kwa Mungu.

Hebu tuzungumze kuhusu dai ambalo Biblia inatoa kujihusu. Kisha, tutaangazia ushahidi kwamba Biblia ni kweli. Biblia inadai kuwa Neno la Mungu. Katika Agano la Kale, kuna kauli zaidi ya 3,000 kwamba jumbe zilitoka kwa Mungu, ambazo mara nyingi husema tu, “Bwana alisema….”[1] Yesu alichukulia kuwa Agano la Kale lilihamasishwa na Mungu. (Soma Mathayo 5:17-18; Yohana 10:35; Marko 12:36.) Waandishi wa Agano Jipya walichukulia kuwa Agano la Kale limetoka kwa Mungu. (Soma Matendo 3:18; 2 Timotheo 3:16; 2 Petro 1:20-21.) Waandishi wa Agano Jipya walichukulia kwamba maandishi ya Agano Jipya yalihamasishwa na Mungu. (Soma 1 Wakorintho 14:37; 2 Petro 3:16.)

Ikiwa mtu hakubali dai la Biblia kujihusu, anapaswa kuangalia ushahidi. Hebu fikiria tena kwamba hujui kuhusu Biblia. Unajua kwamba Mungu ni mtu na anaweza kunena akitaka. Kwa hivyo, unajua kwamba  kitabu kinaweza kutoka kwa Mungu. Kisha mtu anakuonyesha kitabu na anakuambia kwamba ni kitabu kutoka kwa Mungu.

» Unawezaje kujua kwamba Biblia kwa kweli ni Neno la Mungu? Ungetarajia iweje?

Mahali ambapo injili inahubiriwa, popote duniani, watu huhisi usadikisho wa ndani wa ukweli wake. Wanapoamini injili na kutubu, wanapata msamaha wa Mungu na maisha yaliyobadilika. Kwa watu wengi, hiyo ndio sababu yao ya kwanza ya kuamini Biblia (Soma 1 Wathesalonike 1:5.)

Kisha kwa wale walio na uhusiano na Mungu, Roho wa Mungu hunena kupitia maandiko, akiwapa ufahamu na usadikisho. Jinsi Roho Mtakatifu anavyoitumia Biblia inathibitisha kwamba ni Neno la Mungu. (Soma Waefeso 6:17.)

> **“Sheria inagundua ugonjwa; injili inatoa tiba.”**
>
> **Martin Luther**

Tunapotembea katika uhusiano na Mungu, tunapata kwamba Biblia hufunua kwa usahihi asili yake na jinsi anavyofanya kazi nasi. Biblia inatuonyesha njia ya

1 Ili kuona mifano, tazama Hesabu 34:1; Hesabu 35:1, 9.

kuanza uhusiano na Mungu na njia ya kuendelea kutembea pamoja naye. Huu ni ushahidi kwamba Biblia ni Neno la Mungu. (Soma Zaburi 119:1-2.)

Lakini je, ukitaka ushahidi usiyotegemea matukio ya kiroho uliopitia wewe mwenyewe? Watu katika dini nyingine pia hupitia matukio ya kiroho, lakini matukio hayo hayatokani na ukweli. Je, tunawezaje kujua kwamba matukio ya kiroho tunayopitia yanatokana na ukweli?

» Je, kuna ushahidi kwamba Biblia ni sahihi katika mambo inayosema?

Biblia iliandikwa na waandishi zaidi ya 40 katika kipindi cha miaka 1,500. Wengi wa waandishi hao hawakufahamiana. Kwa kawaida tungetarajia nini kutoka kwa kitabu kama hicho? Tungedhani kwamba itakuwa na kila aina ya makosa na makinzano. Lakini fikiria mambo yafuatayo kuhusu Biblia. Maelfu ya maeneo ya kijiografia yaliyotajwa katika Biblia yamepatikana; maelfu ya matukio ya kihistoria yamethibitishwa kuwa yalitokea na watu binafsi wanaotajwa katika Biblia wamethibitishwa kuwa walikuwepo katika historia; hakuna kitu chochote kilichogunduliwa kimekanusha taarifa ya Biblia; na Biblia haijikanushi yenyewe kamwe. Kauli kama hizi si kweli kuhusu kitabu chochote kingine kilichowahi kuandikwa. Ushahidi unaunga mkono dai la Biblia kwamba ilihamasishwa na Mungu.

Tukitumia vipengele sita, tunaweza kueleza kwa ufupi ushahidi unaounga mkono dai la Biblia kuwa ni Neno la Mungu. Tunajua Biblia kweli ni Neno la Mungu kwa sababu:

- Maelfu ya taarifa za Biblia zimethibitishwa.
- Hakuna kauli yoyote ya Biblia ambayo imekanushwa.
- Biblia haijikanushi yenyewe.
- Injili inathibitishwa na matokeo yake.
- Roho wa Mungu ananena kupitia Biblia.
- Biblia inaongoza uhusiano wetu na Mungu.

## KUFAFANUA UHAMASISHO

» Je, tunamaanisha nini kwamba Biblia imehamasishwa?

Uhamasisho ni kazi isiyo ya kawaida ambayo kupitia kwayo Mungu alijifunua na kuleta ufunuo huo kwa njia ya maandishi. Biblia ndio matokeo ya mwisho ya uhamasisho huo. Biblia imehamasishwa tofauti na vitabu vingine vyote. **Uhamasisho wa Biblia unamaanisha kwamba ni Neno la Mungu kikamilifu, hata maneno yenyewe yaliyotumiwa**.

Wakati mwingine watu huhisi kana kwamba wamehamasishwa wanapokuwa na mawazo makuu, lakini Biblia inamaanisha zaidi ya hilo inapodai kuwa imehamasishwa na Mungu.

> Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki (2 Timotheo 3:16).

Ingawa maandiko yalitiririka kutoka kwenye kalamu zilizokuwa mikononi mwa wanadamu, msisitizo wa kifungu hiki ni kwamba Biblia ilitoka kwa Mungu. Kwa sababu Biblia imetoka kwa Mungu, inaweza kutegemewa kwa ajili ya kufundisha kanuni. Ni bora kuliko kile kilicho bora zaidi ambacho watu wanaweza kufanya.

> Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:20-21).

Vifungu hivi katika 2 Petro vinasema kwamba waandishi waliongozwa na Roho Mtakatifu. Usahihi wa waandishi wa Biblia haukutegemea ufahamu wao wenyewe. Ukweli kwamba walihamasishwa au kuongozwa na Roho Mtakatifu katika uandishi wao unaonyesha kwamba kutegemeka kwa maandishi yao hatimaye kulitegemea Mungu. Biblia inategemeka kama vile Mungu.

## UHAMASISHO ULIKUWAJE?

» Je, baadhi ya njia ambazo waandishi wa Biblia walipokea ukweli wa Mungu kabla ya kuandika zilikuwa zipi?

Wakati mwingine watu hujiuliza jinsi uhamasisho ulifanya kazi. Mungu aliwasilishaje ukweli wake na kuhakikisha kwamba umeandikwa kwa usahihi? Ukweli wa kwanza tunaopaswa kutambua kuhusu mtindo wa Mungu wa ufunuo ni kwamba ni wa aina mbalimbali. Hatumii njia moja tu. (Soma Waebrania 1:1.)

Wakati mwingine Mungu alizungumza kwa sauti ya kusikika, kama vile alipozungumza na Musa (Kutoka 33:11). Wakati mwingine alitoa ndoto au maono, na mwandishi akayaeleza.[2] Labda sehemu ya maandiko iliyokuja moja kwa moja zaidi kutoka kwa Mungu na kuandikwa ilikuwa agano kati ya Mungu na Israeli ambalo liliandikwa kwa kidole cha Mungu (Kumbukumbu la Torati 9:10). Sehemu nyingine za maandiko zinaonekana kuwa zilisemwa na zikaandikwa, kwa sababu vifungu vikuu katika Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu vinakuja baada ya kauli inayosema, "Bwana akanena na Musa, akisema…"

Uhamasisho haumaanishi kwamba Mungu alimnenea mwandishi maneno kwa sauti ya kusikika. Tunaona tofauti za haiba na mitindo ya uandishi kati ya waandishi mbalimbali. Kwa mfano, mtindo wa Paulo ni tofauti sana na wa Petro. Mtazamo wetu wa uhamasisho unatambua jinsi Mungu alivyotumia haiba, misamiati, mitindo ya uandishi, elimu na utafiti wa kihistoria wa wanadamu.

---

2 Kwa mifano ya ufunuo kupitia maono, tazama Danieli 7 na 8, na sehemu kubwa ya kitabu cha Ufunuo.

Mtazamo sahihi wa uhamasisho ni kwamba Mungu alimhamasisha mtu mzima, akitumia fikira na haiba ya mwandishi mwanadamu kueleza ukweli wa kiungu, si tu kufunua ukweli bali pia alisimamia mchakato wa kuandika ili maandiko yawe na usahihi kamili.

Watu wengine hufikiri kwamba Mungu alitoa tu mawazo ambayo alitaka kuwasilisha na mwandishi mwanadamu aliyaeleza vizuri kadiri anavyoweza, na kufanya makosa yasioepukika na ya kibinadamu katika maelezo yake. Mtazamo huo hauambatani na maelezo ya Biblia kuhusu uhamasisho. Biblia inaeleza kwamba waandishi waliongozwa na Roho Mtakatifu katika uandishi wao, kwa hivyo tunajua kwamba hawakuachwa waandike peke yao, wakifanya makosa.

Kwa sababu Biblia ni Neno la Mungu, haisemi jambo lolote lisilo sahihi kwa sababu Mungu hakosei (Soma Mithali 30:5.) Kwa kuwa Mungu alijifunua katika historia iliyorekodiwa katika Biblia, ni lazima maelezo yote yawe sahihi ili tuwe na ufunuo wa Mungu unaotegemeka. Kwa hivyo, kwa sababu ya maelezo ya Biblia kuhusu uhamasisho, tunajua kwamba Mungu aliongoza uandishi ili maandiko yawe sahihi kikamilifu.

## MANENO YANAYOTUMIWA KUTETEA USAHIHI KAMILI WA BIBLIA

### Iliyohamasishwa

Biblia ilihamasishwa, kumaanisha kwamba ni Neno la Mungu kikamilifu, hata maneno yenyewe yaliyotumiwa. Neno hili awali lilitosha kuthibitisha kutegemeka na usahihi kamili wa Biblia, lakini sasa baadhi ya watu wanaosema wanaamini kwamba Biblia ilihamasishwa wanakataa kwamba ni sahihi kikamilifu. Maneno yafuatayo yameanza kutumika kutetea vipengele muhimu vya uhamasisho.

### Isiyoweza kuwa na makosa

Neno hili linamaanisha “haiwezi kushindwa.” Tunaposema kwamba Biblia haiwezi kuwa na makosa, tunamaanisha kwamba inaweza kuaminiwa na kamwe haiwezi kutupotosha. Biblia haiwezi kuwa na makosa si tu katika maelezo yake ya kikanuni, bali pia katika kila kauli inayotoa.

### Isiyokuwa na makosa

Neno hili linamaanisha “bila makosa.” Biblia ni sahihi katika kila kauli inayotoa. Kwa kuwa Mungu hawezi kamwe kusema uongo au kufanya kosa (soma Tito 1:2) na Biblia ni Neno la Mungu, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Biblia haina makosa. Mtu akisema kwamba Biblia inaweza kuwa na makosa kwa sababu wanadamu walihusika katika uandishi wake, anasahau maelezo kuhusu uhamasisho katika 2 Petro 1:21: waandishi waliongozwa na Roho Mtakatifu. Mtazamo wa kibiblia na wa kihistoria kuhusu uhamasisho ni kwamba

Biblia nzima imehamasishwa, hata maneno yake yenyewe, na kwa hivyo haina makosa. (Soma Mathayo 5:18.)

## Je kuhusu Makosa katika Kunakili?

Kabla ya uchapishaji wa mashine kuwepo, hati zote pamoja na maandiko zilinakiliwa kwa mkono. Hatuna hati za asili zilizoandikwa na Paulo, Isaya au Musa. Miongoni mwa maelfu ya nakala za kale zilizoandikwa kwa mkono tulizo nazo katika lugha ya Kigiriki na Kiebrania, kuna tofauti ndogo ndogo, na hatuwezi kujua katika hali zote ni maneno gani hasa yalitumiwa katika maandishi ya asili. Hata hivyo, tofauti hizo ni ndogo sana kiasi kwamba hakuna kanuni inayoweza kutiliwa shaka kwa sababu ya maneno hayo. Kwa sababu tunajua kwamba nakala za asili hazikuwa na makosa, na kwa sababu tofauti katika nakala hizo ni ndogo sana, tunajua kwamba tunaweza kuamini kila kauli inayotolewa na Biblia.

» Tunajuaje kwamba Biblia ni sahihi ingawa ilinakiliwa kwa mkono mara nyingi?

» Ni sababu gani mbalimbali zinazofanya watu wengine wafikiri kwamba Biblia ina makosa?

## KWA NINI WATU WENGINE WANAFIKIRI BIBLIA INA MAKOSA?

Wakati mwingine watu wengine hudai kwamba Biblia ina makosa. Hiyo ni kwa sababu hawaelewi asili ya Biblia.

Biblia ilitumia mawasiliano ya kawaida ya wanadamu. Kwa mfano, kuna kifungu kinachosema jua linasonga angani. Wanasayansi wengi wanaamini kwamba dunia inazunguka, badala ya jua kusonga, lakini pia wanasema jua huchomoza na kutua. Waandishi wa Biblia walieleza tu kama walivyoona.

Pia kuna kauli za kishairi, kama “Milima iliruka kama kondoo waume” (Zaburi 114:4), au “miti yote ya kondeni itapiga makofi” (Isaya 55:12). Huo ni mtindo wa fasihi ambao ni dhahiri haumaanishi moja kwa moja kile kinachosemwa.

Wakati mwingine waandishi walinukuu watu wengine, wakiwemo watu ambao hawakuongozwa na Roho. (Kwa mfano, hotuba za marafiki wa Ayubu zimeandikwa, ingawa Mungu alisema yale waliyosema hayakuwa sahihi (Ayubu 42:7).)

Hakuna lolote kati ya hayo ambalo ni tatizo kwa kanuni ya uhamasisho. Mungu aliongoza mchakato wa kuandika ili kuhakikisha kwamba hatimaye kile kitakachoandikwa kitakuwa Neno lake.

Wakati mwingine watu hufikiri wanaona mkinzano katika Biblia, lakini wanahitaji kuiangalia kwa makini zaidi. Kwa mfano, Marko 5:1-2 na Luka 8:26-27 inatuambia kuhusu mtu

aliyekuwa amepagawa na pepo ambaye aliwekwa huru na Yesu. Mathayo 8:28 inatuambia kwamba kulikuwa na watu wawili waliokuwa wamepagawa na pepo waliowekwa huru. Huo si mkinzano. Luka na Marko hawakusema kulikuwa na mtu mmoja tu. Walichagua kumwangazia mtu mmoja ambaye alikuwa na historia katika eneo hilo. Mtu akiona kauli za Biblia ambazo zinaonekana kukinzana, hapaswi kuwa na haraka ya kufikia hitimisho fulani, bali achukue muda wa kuelewa muktadha.

## BIBLIA KWA AJILI YA MKRISTO

» Je, baadhi ya njia ambazo Mkristo anapaswa kutumia Biblia ni zipi?

Biblia inatoa sheria ya Mungu. Kufuata sheria hakutuokoi, lakini sheria inatuonyesha jinsi Mungu anavyotaka tuishi. Sheria ya Mungu inaonyesha asili ya Mungu. Tunapaswa kuifuata kwa sababu tunataka kuwa kama Mungu. Kwa sababu tunampenda Mungu, tunapaswa kuipenda sheria yake. Zaburi 119 inaeleza jinsi mtu anayemwabudu Mungu anavyopaswa kufurahia sheria ya Mungu. Mtu anayempenda Mungu atamwomba Mungu aubadili moyo wake ili ufanane na mapenzi ya Mungu. Haiwezekani mtu anayempenda Mungu kutojali kuhusu kumpendeza Mungu.

Neno la Mungu ni nuru. Mtume Petro anatuambia kwamba ulimwengu uko katika giza la kiroho, na Neno la Mungu ni nuru ya kutuongoza katika njia tunayopaswa kufuata. (Soma 2 Petro 1:19-21; tazama pia Zaburi 119:105.) Mtu hapaswi kamwe kufuata mawazo au hisia zinazokinzana na Neno la Mungu. Roho Mtakatifu hawezi kamwe kumwongoza mtu kufanya jambo ambalo Biblia inasema si sahihi.

Neno la Mungu ni chakula chetu cha kiroho. Hamu ya kula ni ishara ya afya bora, na Mkristo atatamani Neno la Mungu kama mtoto mchanga anavyotamani maziwa (1 Petro 2:2). Kadiri Mkristo anavyokomaa, ataweza kuelewa kwa kina zaidi ukweli wa Mungu, kama vile mtoto anavyojifunza kula chakula kigumu (1 Wakorintho 3:2). Ni lazima Mkristo ajilishe kiroho kila siku kwa kula Neno la Mungu.

> **"Uongo mkubwa zaidi ambao utamaduni wetu unaamini leo ni kwamba sisi ni watu wazuri na kwamba, kwa sababu Mungu ni mwenye upendo, hataadhibu dhambi."**
>
> **Francis Chan**

Biblia ni ngao yetu dhidi ya Shetani. Tumeagizwa kujivika silaha za kiroho. Upanga ambao Roho Mtakatifu anatupatia ni Neno la Mungu (Waefeso 6:17). Yesu alijibu majaribu ya ibilisi kwa kutumia maandiko (Mathayo 4:3-4).

Neno la Mungu ni ukweli unaohitaji mwitikio wetu. Yesu alilinganisha neno na mbegu zilizopandwa (Luka 8:11-15). Baadhi ya mbegu hazikufanya vizuri kwa sababu ardhi haikuwa imetayarishwa. Tunaposoma Biblia, ni lazima tuitikie ukweli wake na kusali ili Mungu alete matunda katika maisha yetu kupitia Neno lake.

## KWA SABABU BIBLIA NI NENO LA MUNGU…

Kwa sababu Biblia ni Neno la Mungu…

- Kamwe haitapitwa na wakati au ikose kuwa na umuhimu. Ni muhimu kwa watu wote, mahali popote na wakati wote.
- Ni mwongozo wa kupambanua mapenzi ya Mungu, kwa kuwa Mungu hawezi kamwe kujipinga au kubadili mawazo yake.
- Ni mwongozo wetu wa kupata yaliyo bora zaidi maishani, kwa kuwa Mungu, Muumba wetu, aliitoa kama maagizo kwa ajili yetu.
- Ina kila kitu tunachohitaji kujua ili kuokolewa na kutembea katika uhusiano na Mungu.

Ingawa tunajifunza kutoka kwa wachungaji na kutoka kwa desturi za kanisa, hakuna wazo linaloweza kukubalika ambalo linakinzana na maandiko kwa sababu maandiko ndio mamlaka ya mwisho.

Roho Mtakatifu hutufunulia Neno la Mungu ili tulielewe na hutuelekeza kulitii.

» Mungu bado ananena, lakini je, tunapaswa kutarajia kwamba kuna kitu kinachoweza kuongezwa kwenye Biblia?

## JE, BIBLIA IMEKAMILIKA?

Tangu mtume wa mwisho afe, kanisa limechukulia Biblia kuwa kitabu kilichokamilika. Kanisa halikuchagua tu maandishi fulani ili kuyaita maandiko; badala yake, lilitambua kwamba maandishi fulani yalihamasishwa na Mungu na yalikuwa na mamlaka ya kimaandiko. Maandishi ambayo yalitambuliwa kuwa maandiko yalitimiza sifa ambazo hakuna maandishi mengine ya baadaye yangeweza kutimiza.

Kwa vitabu vya Agano la Kale, kanisa lilihifadhi maandishi ambayo Israeli ilikuwa imehifadhi kama maandiko. Hatimaye, vitabu vya Agano Jipya vilitambuliwa kama maandiko kwa msingi wa sifa zifuatazo:

- Uhusiano wa kihistoria na mitume
- Uwezo wa kujithibitisha vyenyewe
- Kukubalika na kanisa lote

- Matumizi ya heshima ya Agano la Kale
- Manufaa katika kupinga mafundisho potovu

Mungu bado ananena, lakini je, kuna kitu kinachoweza kuongezwa kwenye Biblia sasa? Haiwezekani kwamba maandishi yoyote mapya yanaweza kutimiza sifa husika ili kujumuishwa katika maandiko ya asili. Kwa mfano, hakuna maandishi mapya yanayoweza kuhusishwa na mitume, kwa kuwa hawako tena pamoja nasi. Pia, hakuna maandishi yoyote mapya yanayoweza kukubaliwa na kanisa zima kote ulimwenguni.

Maandiko ni kamili na yanatosha kwa ajili ya wokovu na kuishi maisha ya Kikristo (2 Timotheo 3:14-17). Hakuna kitu chochote muhimu kinachoweza kuongezwa katika maandiko kwa sababu tayari yana kila kitu tunachohitaji. Watu wanaodai kuwa wanapokea ufunuo mpya badala yake wanapaswa kutumia muda wao kusoma ufunuo ambao Mungu ametoa tayari. Watapata hapo kila kitu wanachohitaji na watalindwa kutokana na kufanya makosa.

## MAKOSA YA KUEPUKA

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Washiriki wawili wa darasa wanaweza kueleza sehemu hii na sehemu inayofuata.*

### Kudhoofisha Mamlaka ya Biblia

Mamlaka yako ya mwisho ni yapi? Wakristo wengi wangesema kwamba Biblia ndio mamlaka yao, lakini kwa kweli wanaamini zaidi hisia zao wenyewe. Mtu atasema kitendo fulani ni sawa kwa sababu hahisi ana hatia anapokifanya. Mtu huyo anafanya hisia zake kuwa mamlaka ya mwisho badala ya Biblia.

Kuna sababu nyingi kwa nini watu wanaweza kutoichukulia Biblia kwa uzito. Labda mtu fulani wanayemheshimu anapuuza fundisho lililo wazi la Biblia, na hilo linawatia moyo kufanya vivyo hivyo. Labda wana hatia ya kufanya jambo ambalo Biblia inakataza, na wanajaribu kutafuta njia ya kutetea matendo yao wenyewe. Labda hawajui yale ambayo Biblia inafundisha. Ni lazima tufanye kila juhudi kuielewa Biblia na kutii mamlaka yake.

### Kujifunza Biblia Ukiwa na Kusudi Finyu

Biblia ndio chanzo kikuu cha kanuni za Kikristo. Ni mamlaka ya mwisho kwa swali lolote la kikanuni. Hata hivyo, ni tatizo watu wanapojifunza Biblia ili tu kupata uthibitisho wa kanuni zao. Hawatumii Biblia kama chakula cha kiroho. Wanafikiria tu jinsi ya kuonyesha kwamba mtu mwingine amepotoka. Ni sawa kwetu kuendeleza na kutetea kanuni zetu tukitumia maandiko. Hata hivyo, ikiwa hiyo ndio njia yetu ya pekee ya kutumia Biblia, tutapoteza furaha inayotokana na kuitumia katika uhusiano wetu wa kibinafsi na Mungu.

Watu wengine husoma Biblia kwa kusudi la kuhisi kutiwa moyo tu. Tunapaswa kukumbuka kwamba makusudi ya Biblia yanajumuisha kufundisha, kusadikisha watu juu ya makosa yao na kuwarekebisha (2 Timotheo 3:16). Hatupaswi kuruka amri za Biblia, tukitafuta ahadi zinazotufanya tujihisi vizuri zaidi. Labda Mungu anataka kusadikisha juu ya makosa yetu au kuturekebisha leo au kutufundisha jambo fulani.

## MAKOSA YA MADHEHEBU POTOVU

Makundi fulani ya kidini yanadai kuamini Biblia, lakini yanafanya kitu kingine kiwe mamlaka yao ya mwisho. Wanadai kwamba ni wao tu ndio wanaoweza kueleza Biblia, wakitumia ufunuo au mfumo fulani maalum ambao ni wao tu ndio walio nao. Kanuni zao muhimu zaidi haziwezi kuthibitishwa kupitia Biblia.

Huenda wakawa na kitabu kingine wanachotumia kama maandiko pamoja na Biblia. Huenda wakasema kwamba Biblia haitegemeki kwa sababu ina makosa ya utafsiri na unakili.

Mawazo hayo yanadokeza kwamba Biblia si kamili kama Neno la Mungu. Kwa watu hao, kitu kingine kinakuwa mamlaka ya mwisho.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Biblia ni Neno la Mungu. Mungu aliwahamasisha waandishi ili waandike bila kufanya makosa. Biblia inajumuisha kila kitu tunachohitaji kujua ili kuokolewa kutokana na dhambi na kutembea katika uhusiano na Mungu. Biblia ndio chanzo kikuu cha kanuni zetu na ndio mamlaka ya mwisho. Mkristo anapaswa kujifunza Biblia kila siku ili kumjua Mungu vizuri zaidi, kuongozwa na Mungu, kulishwa kiroho na kuishi maisha yenye maana na yenye furaha.

## MAZOEZI YA SOMO LA 1

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

   - Zaburi 119:33-40
   - Zaburi 119:129-136
   - Mithali 30:5-6
   - Mathayo 5:17-19
   - 2 Timotheo 3:15-17
   - 2 Petro 3:15-16
   - Ufunuo 22:18-19

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 1. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Angalau mara tatu wakati wa kozi hii, utawafundisha watu wasioshiriki katika darasa lako somo moja au sehemu ya somo. Mafundisho haya yanaweza kufanywa katika darasa kanisani, kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani, mkusanyiko wa familia au mazingira mengine. Unawajibika katika kuunda fursa hizi na kutoa ripoti kwa kiongozi wa darasa lako.

4. Kumbuka siku zote kusoma somo linalofuata ili ujiandae kwa darasa linalofuata.

## MTIHANI WA SOMO LA 1

**1.** Ufunuo wa Jumla Ni Nini?

**2.** Je, Mungu ametoa Ufunuo Maalum kwa njia gani mbili?

**3.** Je, Ufunuo Maalum hufanya mambo gani matatu yasiyofanywa na Ufunuo wa Jumla?

**4.** Je, Biblia inatoa dai gani kujihusu?

**5.** Orodhesha sababu sita zinazotufanya tujue kwamba Biblia ni Neno la Mungu.

**6.** Je, kwa nini Biblia ni yenye faida kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki? (2 Timotheo 3:16).

**7.** Je, Bibilia inatoa maelezo gani juu ya uhamasisho yanayotuhakikishia kwamba waandishi walizuiwa ili wasifanye makosa?

**8.** Orodhesha njia nne za uhamasisho ambazo Mungu alitumia.

**9.** Je, inamaanisha nini kwamba Biblia ilihamasishwa?

**10.** Je, inamaanisha nini kwamba Biblia haiwezi kuwa na makosa?

**11.** Je, inamaanisha nini kwamba Biblia haina makosa?

## SOMO LA 2

# SIFA ZA MUNGU

### MALENGO YA SOMO

**1.** Mwanafunzi ataweza kueleza:

- Kwa nini dhana ya mtu kuhusu Mungu ni muhimu sana.
- Jinsi ukweli kwamba Mungu ni Muumba unamfanya awe tofauti na vitu vingine vyote.
- Sifa za Mungu: maana ya yeye kuwa mwenye nafsi, roho, wa milele, mwenye Utatu, mweza yote, yuko kila mahali, asiyebadilika, ajuaye yote, mtakatifu, mwenye haki, na mwenye upendo.
- Jinsi kila sifa ya Mungu ilivyo muhimu katika uhusiano wetu naye.
- Mtazamo wa kibiblia wa ukuu wa Mungu.
- Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu Mungu.

**2.** Mwanafunzi ataepuka kosa la kutoelewa umuhimu wa aina za ibada.

## UTANGULIZI

» Someni Isaya 40 pamoja. Jadilini kile kifungu hiki kinatuambia kuhusu Mungu.

» Je, kwa nini suala la ikiwa mtu ana dhana sahihi ya Mungu au la ni muhimu?

Mungu ni nani? A. W. Tozer alionyesha umuhimu wa swali hili aliposema, "Ninaamini kwamba hakuna makosa katika kanuni au kushindwa katika kutumia maadili ya Kikristo ambayo hayawezi kufuatiliwa na hatimaye kubainika kuwa yanatokana na mawazo duni kuhusu Mungu".[3] Yesu alimwambia mwanamke Msamaria pale kisimani kwamba tatizo la ibada ya Wasamaria ni kwamba hawakumjua ni nani waliyemwabudu. Sifa muhimu zaidi ya mtu yeyote ni dhana yake kuhusu Mungu. Dhana ya mtu kuhusu Mungu ndio msingi wa dini yake. Hakuwezi kuwa na kosa kubwa zaidi kuliko kupotoka kuhusu jinsi Mungu alivyo.

---

3 A. W. Tozer, *The Knowledge of the Holy* (New York: Harper and Row, 1961), 10.

Ulinganisho hautoshi kueleza kikamilifu jinsi Mungu alivyo, kwa kuwa ni dhahiri kuwa yuko juu sana kuliko sisi. Hata Biblia haitupi ufafanuzi rasmi wa Mungu ni nani, lakini kila mahali inaeleza uwepo wake na nguvu zake. Kitabu cha Mwanzo kinatuambia jinsi Mungu alivyoziumba mbingu na nchi; mimea; jua, mwezi, na nyota; na wanyama; na hatimaye wanadamu. Fundisho la kwanza la maandiko liko wazi kabisa: Mungu ndiye Muumba wa vyote vilivyopo. Hivyo, yeye ni tofauti na vitu vingine vyote vilivyopo, kwa kuwa yeye si sehemu ya uumbaji wake.

Katika Biblia yote kuna kauli zingine nyingi kuhusu Mungu. Wanatheolojia wamefupisha kwa uangalifu taarifa za Biblia katika orodha za sifa za Mungu. Hatuwezi kamwe kuelewa sifa zake kikamilifu kwa kutumia ufahamu wetu usio mkamilifu. Hata hivyo, kuchunguza sifa za Mungu kwa heshima kuu ni zoezi la kiroho lenye thamani. Hivyo, tunazingatia kauli zifuatazo kuhusu Mungu. Zinatokana na kujifunua kwake katika Biblia, na kwa sababu hiyo tunajua kwamba ni za kweli.

## SIFA ZA MUNGU

Tutakachoangazia si orodha kamili ya sifa za Mungu, bali ni zile sifa ambazo ni muhimu zaidi kwetu kujua.

» Je, ni sifa gani za Mungu ambazo unaweza kuziorodhesha?

### Mungu ni Mwenye Nafsi

Hii ina maana kwamba yeye ni mtu halisi, aliye hai na mwenye akili, hisia, na nia.[4] Yeye si jumla ya sheria za asili au nguvu zisizo na utu kama vile umeme au uvutano. Anaumba, anatenda, anajua, ana nia, anapanga na ananena.

» Je, ingeleta tofauti gani kwetu kama Mungu asingekuwa na nafsi?

Ukweli kwamba ana nafsi unatuwezesha kuwa na uhusiano naye. Kama asingekuwa na nafsi, tusingeweza kumwomba. Kama asingekuwa na nafsi isingewezekana yeye kufurahishwa au kuchukizwa.

### Mungu ni Roho

"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" (Yohana 4:24).

Ukweli kwamba yeye ni roho unatoa msingi wa ushirika wetu wa kiroho naye na ibada yetu kwake. Sala na ibada hazitegemei vitu vinavyoweza kuonekana, mikao mahususi ya

4 Mwanzo 6:6, Isaya 42:21, Isaya 46:10-11, Nahumu 1:2, Sefania 3:17, Yakobo 5:11, 1 Petro 5:7

mwili, ratiba mahususi au jengo. Mambo hayo yanaweza kutusaidia kuelekeza akili zetu katika ibada, lakini ibada haitegemei mambo hayo.

Ukweli kwamba Mungu ni roho ni sababu moja iliyomfanya atukataze tusitengeneze sanamu yake. (Soma Kutoka 20:4-6.) Akiwa roho, hatuwezi kumwona Mungu (1 Timotheo 1:17) isipokuwa anapochagua kuchukua umbo linaloonekana. (Soma Mwanzo 18:1; Isaya 6:1.) Kwa sababu uwezo wetu wa kumwona Mungu una mipaka, hata wakati anapoonekana katika umbo linaloonekana, ni kweli kusema kwamba hakuna mtu ambaye amemwona Mungu kikamilifu (Kutoka 33:20; Yohana 1:18; Yohana 6:46).

## Mungu ni wa Milele

Hakujawahi kuwa na wakati ambapo Mungu hakuwepo, na hakutawahi kuwa na wakati ambapo hatakuwepo; Mungu hana mwanzo wala mwisho. Mungu alijidhihirisha kwa jina, MIMI NIKO AMBAYE NIKO (Kutoka 3:14). Anaelezwa na Yohana kama yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi (Ufunuo 1:8). Tangu milele hata milele yeye ni Mungu (Zaburi 90:2). Baadhi ya dini zina hekaya kuhusu wakati miungu yao ilizaliwa, lakini Mungu wa kweli ni wa milele.

## Mungu ni Mwenye Utatu

Biblia inasema kuna Mungu mmoja lakini inataja nafsi tatu tofauti kuwa Mungu. Kuna Mungu mmoja tu, lakini katika asili yake kuna nafsi tatu. Ingawa hatuwezi kuelewa kikamilifu Utatu wa Mungu, hilo si jambo lisilo la kimantiki, kwa kuwa hatusemi kwamba kuna vitu vitatu na kitu kimoja ambavyo ni kitu kile kile. Kuna Mungu mmoja, aliye na nafsi tatu. Kwa sababu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ambao wote wana sifa zote za uungu, kila mmoja wao anaweza kustahili kuitwa Mungu na kuabudiwa kama Mungu. (Mengi zaidi yatasemwa kuhusu Utatu wa Mungu katika somo linalofuata.)

## Mungu ni Mweza Yote

Anaweza kufanya chochote anachotaka. “Lakini Mungu wetu yuko mbinguni, alitakalo lote amelitenda” (Zaburi 115:3). Hana mipaka isipokuwa kamwe hatendi kinyume na asili yake takatifu na siku zote anatekeleza yale aliyoahidi kutekeleza. Hakuna jambo gumu au ambalo ni changamoto kwa Mungu. “Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki” (Ufunuo 19:6).

» Je, kujua kwamba Mungu ni mweza yote kunaleta tofauti gani kwetu?

Hili ni jambo la kutia moyo, kwa kuwa tunajua kwamba katikati ya mapambano yetu anaweza “kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu” (Wefeso 3:20). Hata kama mambo yanaonekana yameenda marama kabisa, tunajua kwamba mpango mkuu wa Mungu utatimizwa. Tunaweza kuomba tukiwa na uhakika kwamba Mungu anaweza kuingilia kati katika hali yoyote.

## Mungu Yuko Kila Mahali

Hakuna mahali ambapo hayuko, na hakuna kinachotokea ambacho hakioni. “BWANA asema hivi, Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu” (Isaya 66:1). Yeye ni Mungu wa ulimwengu wote, na nguvu zake hazikomi katika eneo lolote. “Je, mtu ye yote aweza kujificha mahali pa siri, nisimwone? Asema BWANA. Je! Mbingu na nchi hazikujawa nami?” (Yeremia 23:24). Hilo linatuhakikishia kwamba Mungu anajua hali zetu na matatizo yetu. Pia linatuambia kwamba hakuna mtu anayeweza kujificha kutoka kwa Mungu, au kutenda dhambi mahali ambapo Mungu hawezi kuona. Vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake. (Soma Waebrania 4:13.)

## Mungu Habadiliki

Hakujawahi kuwa na wakati ambapo Mungu alifanyika kuwa Mungu, na hataacha kuwa Mungu. (Soma Yakobo 1:17.) Kuna dini zinazoamini kwamba Mungu yuko katika mchakato wa kuendelea kufanyika Mungu, lakini Biblia inatuambia kwamba katika nafsi yake na asili yake, na katika sifa na makusudi yake, Mungu habadiliki kamwe. (Soma Malaki 3:6.) Siku zote anapenda kile kilicho sahihi, na siku zote anachukia kile kilicho kibaya. Mungu wa Milele aliyejidhihirisha kwa Musa kama MIMI NIKO AMBAYE NIKO ndiye MIMI NIKO AMBAYE NIKO wa leo. Hana kikomo, ni wa milele na hawezi kubadilika katika nafsi, hekima, nguvu, utakatifu, haki, wema na ukweli wake. Yeye ni yule yule siku zote na miaka yake haitakuwa na mwisho (Zaburi 102:27).

> **“Hatuhitaji kamwe kupiga kelele kila mahali kwa Mungu ambaye hayuko. Yuko karibu zaidi kuliko nafsi zetu, karibu zaidi kuliko mawazo yetu ya siri.”**
>
> **A.W. Tozer**

## Mungu ni Mjua Yote

“Akili zake hazina mpaka” (Zaburi 147:5). Mungu hahitaji mchakato wa kujifunza, kwa kuwa anajua kila kitu. Mungu hajawahi kujifunza kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote na hakuna mtu anayeweza kumshauri. (Soma Isaya 40:13-14.) Mungu anajua mambo ya siku zijazo na kwa hivyo hashangazwi au hawezi kukosa kuwa tayari kwa lolote litakalotokea (Zaburi 139:4).

» Je, kujua kwamba Mungu ndiye anayejua yote kunaleta tofauti gani kwetu?

Hekima ya Mungu inahusiana na maarifa ya Mungu, yanayodhihirishwa katika uumbaji na hasa katika mpango wa wokovu. (Soma Zaburi 104:24; Warumi 11:33.) Kwa kuwa anajua na anaelewa yote, siku zote anajua kile kilicho sahihi kufanya. Mapenzi ya Mungu siku zote ni bora kwetu kwa sababu Mungu anaelewa kila hali kikamilifu na anajua matokeo ya kila tendo yatakuwaje.

## Mungu ni Mtakatifu

Mungu amejieleza mwenyewe kuwa mtakatifu kimsingi. Nabii Isaya alimrejelea Mungu tena na tena kama "Mtakatifu wa Israeli." Malaika wanasema "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu" mbele zake daima (Ufunuo 4:8, Isaya 6:3). Utakatifu wa Mungu ulikuwa mada ya ibada: "Na walishukuru jina lake kuu la kuhofiwa; Ndiye mtakatifu" (Zaburi 99:3). Yeye ndiye kiwango kamili cha ukamilifu wote wa kimaadili. Matendo yake yanadhihirisha uwepo wa wema wote na kutokuwepo kwa uovu wowote na haiwezi kuwa vinginevyo. Utakatifu wa Mungu unaonyesha kwamba mwanadamu hastahili kutumikia na kuabudu bila kwanza kubadilishwa kwa neema. (Soma Isaya 6:5.) Mungu anataka tuwe watakatifu kama yeye. "Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, 'Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu'" (1 Petro 1:15-16).

## Mungu ni Mwenye Haki

Matendo ya Mungu ni sahihi siku zote. Matendo yake yanatokana na asili yake takatifu. (Soma Kumbukumbu la Torati 32:4.) Asili yake mwenyewe ndio kiwango cha kile kilicho sahihi. Yeye siku zote hutimiza ahadi zake na kamwe hasemi uwongo (Hesabu 23:19; 2 Samweli 7:28).

» Je, kwa nini ni jambo muhimu kwetu kwamba Mungu ni mwenye haki?

Haki yake ndio msingi wa sheria yake, ambayo ndio kiwango kamili cha wajibu wetu kwake na kwa wengine. Anatekeleza sheria yake kwa haki, akiwapa thawabu wale wanaoitii na kuwaadhibu wale wanaoivunja. Hilo linawafariji wale wanaoteseka na kukandamizwa, lakini pia linatuonya kwamba hakuna mtu atakayeepuka adhabu iwapo atatenda mabaya. "Hukumu za BWANA ni kweli, zina haki kabisa" (Zaburi 19:9). Atamlipa kila mtu kulingana na matendo yake (Warumi 2:6). "Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu" (Warumi 14:10).

## Mungu ni Upendo

Sifa hii ni muhimu sana. Hebu fikiria jinsi lingekuwa jambo la kuogofya sana ikiwa Mungu mwenye uwezo wote na maarifa yote asingetupenda! Ingekuwaje kama angekuwa mtakatifu na mwenye haki, lakini hatupendi? Pamoja na uwezo wake na utakatifu wake kamili, Mungu

anatupenda. (Soma Warumi 5:8.) Mungu hubariki uumbaji wake kwa jumla (Soma Mwanzo 1:22, 28). Yeye hasa hubariki wanadamu kwa kuwapa vitu vizuri vya maisha, na aliumba ulimwengu kuwa mahali ambapo watu wanaweza kuishi kwa furaha.[5] Kwa wale wanaompenda na kumtumikia, yeye hugeuza kila jambo la maisha kuwa baraka (Warumi 8:28). Neema, rehema, subira, na amani yake hutubariki kwa sababu ya upendo wake. (Soma Kutoka 34:6; Waefeso 1:7, Waefeso 2:4-5.)

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16). Licha ya dhambi na uasi wetu, yeye hutuonyesha rehema, akitualika tuje kwake kwa njia ya Yesu, ambaye amemtoa kama dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu (1 Yohana 2:2). Msalabani Mungu anatuonyesha moyo wake, ambao umejaa upendo na huruma kwa ajili yetu. "Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu" (1 Yohana 4:10). Mungu anawapenda watu wote, bila kushawishiwa na makabila yao, uwezo wao wa asili au hadhi yao ya kidunia, na anatoa msamaha kwa wote. (Soma Warumi 2:11; Yakobo 2:1-5.) Kwa hivyo, Mungu anataka tuwapende watu wote na tuwe tayari kusamehe mtu yeyote anayetukosea. Upendo na msamaha ni alama za watoto wa Mungu. (Soma Mathayo 5:43-45.)

**"Kuna afueni kubwa katika kujua kwamba upendo wake kwangu ni halisi kabisa licha ya ufahamu wake wa awali wa mambo mabaya zaidi kunihusu, hivyo hakuna chochote anachoweza kugundua kunihusu kinachoweza kumtamausha, jinsi ninavyotamauka sana mara kwa mara juu yangu mwenyewe, na kuzima azma yake ya kunibariki."**

**J.I. Packer**
*Kumjua Mungu*

**"Umetuumba kwa ajili yako, ee Bwana, na mioyo yetu haijatulia mpaka ipate utulivu ndani yako."**

**Agostino wa Hippo**

Mungu alituumba kwa mfano wake. Ingawa sisi tuna kikomo na yeye hana kikomo, tunafanana naye zaidi kuliko kitu chochote kingine katika uumbaji wake. Alituumba ili tuweze kumjua, kumwabudu na kumpenda. Ametuumba kwa ajili yake mwenyewe, na kama Agostino anavyotukumbusha, hatutapata utulivu kamwe hadi tupate utulivu ndani

5 Zaburi 8:4-6; Zaburi 23; Zaburi 36:5-10; Zaburi 103

yake. Tofauti na Mungu, vitu vyote vya kidunia si vya maana, na ni kwake tu ndio tunastahili kujitoa kikamilifu. Haiwezekani kupata uradhi wa kudumu popote pengine isipokuwa katika Mungu. Kwa neema yake tunaweza kukombolewa na kufanywa kuwa na uwezo wa kumwabudu yeye kando na vitu vyote vingine, kumwamini kama Baba yetu wa Mbinguni na kutekeleza mapenzi yake katika kila nyanja ya maisha yetu.

## MUNGU NI MKUU

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshiriki wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Mungu ana uwezo kamili na mamlaka kamili. Kama mtawala wa ulimwengu, anaweza kutimiza chochote anachotaka (Zaburi 115: 3, Zaburi 135: 5-6).

Yeye hufanya mambo yote kulingana na mapenzi yake mwenyewe, bila kuhitaji kumtii mtu mwingine yeyote (Waefeso 1:11). Chochote anachoamua kufanya hakika kitatendeka, kwa maana hakuna mtu anayeweza kumzuia wala hakuna hali inayoweza kumfanya ashindwe kufanya kile anachotaka. (Soma Isaya 46:9-11.) Yeye hudhibiti matendo ya watawala wa dunia wakati wowote anapotaka (Mwanzo 50:20; Matendo 4:27-28).

Lakini Mungu amewapa watu uwezo wa kufanya maamuzi. Wanaweza kuchagua kati ya mambo mazuri, lakini pia wanaweza kuchagua kati ya mema na mabaya. Wanaweza kuchagua kumtii Mungu au kutomtii. Watu wa kwanza kabisa aliowaumba walifanya uamuzi wa kutenda dhambi. Tangu wakati huo kila mtu amefanya maamuzi, na ingawa wengine wamefanya maamuzi mazuri, wote pia wametenda dhambi.

Ikiwa Mungu ndiye Bwana anayetawala mambo yote, anatimizaje mapenzi yake katika ulimwengu ambapo mabilioni ya viumbe wanafanya maamuzi yao wenyewe?

Ni mapenzi ya Mungu kwamba viumbe wake wafanye maamuzi halisi. Hiyo inamaanisha kwamba hatawafanyia maamuzi yao yote. Inamaanisha pia kwamba lazima kuwe na matokeo halisi kwa kile wanachofanya; la sivyo, hawatakuwa wanafanya maamuzi halisi. Ikiwa kwa njia fulani Mungu angekuwa anadhibiti matokeo ya matendo ya mtu ili mabaya yasitokee, basi atakuwa anachukua kutoka kwa mtu huyo uwezo wa kuchagua uovu.

Haki ya Mungu ni haki ya kweli kwa sababu atakuwa akiwahukumu watu kwa ajili ya matendo yao ya hiari. (Soma Ufunuo 20:12-13.) Ikiwa Mungu angedhibiti matendo yote, isingekuwa jambo la busara kwake kutoa adhabu na thawabu.

Mungu anatamani watu wachague kile kilicho sahihi, lakini zaidi ya yote anatamani wafanye maamuzi halisi. Ndio maana dunia iko jinsi ilivyo. Ulimwengu ni mchanganyiko tata wa mambo mema kutoka kwa Mungu, matokeo ya matendo mema ya wanadamu, matokeo ya matendo mabaya ya wanadamu, na mema ambayo Mungu huleta hata kutokana na matendo mabaya ya wanadamu.

Tunaona vipaumbele vya Mungu katika mpango wa wokovu. Anatoa wokovu kwa wote na anataka wote waokolewe (1 Timotheo 2:3-4). Anampa kila mtu uwezo wa kuitikia injili lakini halazimishi mtu kuitikia. Ndio maana mialiko na ushawishi unatumiwa katika maandiko.[6] Mungu anawapa watu chaguo na kuwaeleza matokeo ya chaguo hilo.

Tunahubiri injili kwa ujasiri tukiwa na uhakika kabisa kwamba kila mtu anaweza kuokolewa. Dhamira yetu ni kushirikiana na Roho Mtakatifu katika kuwashawishi watu kujisalimisha kwa Mungu. (Soma 2 Wakorintho 5:11.)

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Kuna Mungu mmoja, aliyeumba ulimwengu na ni Bwana juu ya vyote. Yeye ni Roho wa milele, asiyebadilika. Yeye ni mwenye uwezo wote, mjua yote na yuko kila mahali. Yeye ni mtakatifu kikamilifu katika tabia yake na mwenye haki katika yote anayofanya. Anabariki uumbaji wake na anampenda kila mtu, akitoa msamaha na uhusiano naye.

6 Kumbukumbu la Torati 30:15, 19; Yoshua 24:15; Isaya 1:18; Isaya 55:1; Ezekieli 18:31; Ufunuo 3:20

## MAZOEZI YA SOMO LA 2

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

   - Zaburi 139:1-4
   - Mithali 9:10
   - Isaya 46
   - Ufunuo 4:9-11

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 2. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 2

1. Je, sifa muhimu zaidi ya mtu ni ipi?

2. Je, fundisho la kwanza la maandiko ni lipi?

3. Taja sifa ya Mungu inayolingana na kila kauli:

   - Hatuwezi kueleza jinsi Mungu anavyoonekana.
   - Mungu amekuwepo siku zote.
   - Mungu ana akili, hisia na nia.
   - Mungu ni yule yule siku zote.
   - Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka.
   - Mungu huona kila kitu.
   - Mungu alimtuma Mwanawe ili tuweze kupata rehema.
   - Mungu ana nafsi tatu katika asili yake.
   - Mungu ni mkamilifu kabisa katika maadili.
   - Mungu hajifunzi chochote.
   - Matendo ya Mungu daima ni ya haki.

## SOMO LA 3

# UTATU WA MUNGU

### MALENGO YA SOMO


1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

   - Jinsi ulimwengu ni kielelezo cha asili ya Utatu wa Mungu.
   - Msingi wa kibiblia wa kanuni ya Utatu wa Mungu.
   - Kwa nini kanuni ya Utatu wa Mungu ni msingi wa injili.
   - Mfumo wa mahusiano ndani ya Utatu wa Mungu.
   - Jinsi Utatu wa Mungu unatoa kielelezo cha mahusiano kati ya wanadamu.
   - Jinsi imani yetu katika Utatu wa Mungu inavyoongoza ibada yetu.
   - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu Utatu wa Mungu.

2. Mwanafunzi ataepuka makosa ya kawaida ambayo watu wamefanya katika kujaribu kueleza Utatu wa Mungu.

## UTANGULIZI


» Someni Yohana 14 pamoja. Jadilini jinsi kifungu hiki kinaonyesha kwamba Mungu ni Utatu.




Watu wengi wamekanganywa na kanuni ya Utatu wa Mungu kwa sababu inasema kwamba Mungu ni watatu katika maana moja, na ni mmoja katika maana nyingine.

Lakini tunapotazama **ulimwengu** tunaona mfano mwingine wa tatu katika moja. Ulimwengu una vipengele vitatu - nafasi, wakati na mata. Bila mojawapo ya vitu hivyo vitatu, kusingekuwa na ulimwengu.

Kila moja ya vipengele  hivyo vitatu pia ina vipengele vitatu.




**Nafasi** inajumuisha urefu, upana, na kimo - tatu katika moja. Bila mojawapo ya vipimo hivyo, kusingekuwa na nafasi.




**Wakati** unajumuisha wakati uliopita, uliopo na ujao - tatu katika moja. Bila mojawapo ya vipengele hivyo, kusingekuwa na wakati.

**Mata** inajumuisha *nishati* iliyo katika *mwendo* inayozalisha *matukio* – tatu katika moja. Kusingekuwa na nishati, kusingekuwa na mwendo au matukio. Kusingekuwa na mwendo, kusingekuwa na nishati au matukio. Kusingekuwa na matukio, ingekuwa ni kwa sababu hakuna nishati au mwendo.

Inaonekana ni kana kwamba ulimwengu umeundwa katika muundo wa tatu katika moja. Labda Mungu kimakusudi aliupatia ulimwengu muundo unaoonyesha asili yake mwenyewe.

Biblia inafundisha nini kuhusu Utatu wa Mungu? Inathibitisha kwa uwazi kuwepo kwa nafsi *tatu* tofauti ambazo zote zinatambuliwa kama Mungu *mmoja* wa ulimwengu. Huu si ukinzani kwa sababu hatusemi kwamba Mungu ni nafsi moja na nafsi tatu kwa wakati mmoja. Wala hatusemi kwamba Mungu ni Mungu mmoja na Miungu watatu. Tunasema kwamba Mungu ni mmoja katika asili na watatu katika nafsi. Kama vile ulimwengu mmoja uko kama nafasi, wakati na mata, Mungu mmoja yuko kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

## USHAHIDI WA KIBIBLIA WA UTATU WA MUNGU

**Kauli ya 1: Kuna Mungu mmoja tu.**

> Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja (Kumbukumbu la Torati 6:4).
>
> Maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi (Isaya 46:9).

**Kauli ya 2: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wote ni Mungu.**

> Mungu Baba (Wagalatia 1:1).
>
> Neno alikuwa Mungu… Neno alifanyika mwili (Yohana 1:1, 14).
>
> Kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu…? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu (Matendo 5:3-4).


**Kauli ya 3: Hawa watatu wanahusiana kati yao kama nafsi tofauti.**

» Je, tunajuaje kwamba nafsi hizi ni nafsi tatu wala si nafsi moja inayotekeleza majukumu tofauti?

Katika Marko 1:10-11, Yesu anabatizwa, Roho Mtakatifu anashuka kama njiwa, na sauti kutoka mbinguni inasema, "Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe." Tunaona hapa kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu hawawezi kuwa nafsi moja; wanatekeleza majukumu tofauti kwa wakati mmoja.

Kuelekea mwisho wa huduma yake, Yesu alisema atamwomba Baba amtume Msaidizi mwingine kwetu — Roho Mtakatifu (Yohana 15:26). Je, unaona nafsi tatu tofauti zikihusika katika ombi hili?

Ukisoma Yohana 14-17, utaona marejeleo mengi ya mwingiliano kati ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.




**Hitimisho: Mungu mmoja wa kweli wa Biblia amejidhihirisha kuwa katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Mungu ni mmoja katika asili, lakini watatu katika nafsi.**

Hivyo, ingawa neno *Utatu* halionekani katika Biblia, kanuni ya Utatu wa Mungu inatokana na kauli zilizo wazi katika kimaandiko. Neno *Utatu* ni neno tunalotumia kusema kwa ufupi yote ambayo Biblia inafundisha kuhusu kanuni hii.

Kanuni hii ya kibiblia imefundishwa na kanisa tangu enzi ya mitume. Huu hapa ni mchoro ambao kanisa limetumia kwa karne nyingi kueleza Utatu wa Mungu.

## KANUNI YA UTATU WA MUNGU NI MUHIMU

» Je, kwa nini ni suala muhimu ikiwa mtu anaamini au haamini Utatu wa Mungu?

Kanuni ya Utatu wa Mungu ni msingi wa mafundisho makuu ambayo ni muhimu kwa injili. Kwa mfano, baadhi ya wale wanaokana Utatu wa Mungu wanakana kwamba Yesu ni Mungu. Lakini ikiwa Yesu unayemwamini si Mungu, basi huna Yesu anayeweza kukuokoa! Ni mtu asiye na dhambi tu ndiye angeweza kufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Angepaswa kuwa dhabihu isiyo na kikomo kwa sababu tumemtenda dhambi Mungu asiye na kikomo. Kwa sababu Yesu ni Mungu, alikuwa dhabihu isiyo na dhambi na isiyo na kikomo ambayo ililipa dhambi za watu wote kwa wakati wote.

Ikiwa tunakana kwamba Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, tunamnyang'anya Mungu sifa zake za asili za kibinafsi au za kiuhusiano. Kwa mfano, Mungu asingekuwa Mungu mwenye upendo tangu asili ikiwa angengoja hadi baada ya uumbaji ili ampende mtu yeyote. Lakini ikiwa Mungu ana zaidi ya nafsi moja, nafsi hizo zingeweza kupendana tangu asili. Ni muhimu kumwamini Mungu huyu wa uhusiano (anayeishi katika upendo wa kujitoa) kwa sababu hilo linaathiri jinsi tunavyohusiana sisi kwa sisi na vilevile jinsi tunavyohusiana na Mungu.

Labda jambo zito zaidi ni kwamba ni lazima tumwabudu Mungu. Watu wanaokana Utatu wa Mungu kwa kawaida hukana kwamba Yesu na Roho Mtakatifu ni Mungu, hivyo hawawaabudu. Mojawapo ya makosa mabaya zaidi ambayo mtu anaweza kufanya ni kumwabudu mtu ambaye si Mungu au kutomwabudu mtu ambaye ni Mungu.

### Sala ya John Stott ya Kila Siku ya Utatu wa Mungu

> Baba uliye Mbinguni, naomba kwamba niweze kuishi siku hii katika uwepo wako na kukupendeza zaidi na zaidi.
>
> Bwana Yesu, naomba kwamba siku hii niuchukue msalaba wangu na nikufuate.
>
> Roho Mtakatifu, naomba kwamba siku hii unijaze na wewe na usababishe matunda yako kukomaa katika maisha yangu: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi.
>
> Utatu ulio Mtakatifu, uliobarikiwa na mtukufu, nafsi tatu katika Mungu mmoja, unirehemu.
>
> Mwenyezi Mungu, Muumba na mhimili wa ulimwengu, ninakuabudu.
>
> Bwana Yesu Kristo, Mwokozi na Bwana wa ulimwengu, nakuabudu.
>
> Roho Mtakatifu, mtakasaji wa watu wa Mungu, ninakuabudu.
>
> Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu,
>
> Kama ilivyokuwa mwanzo, na sasa, na itakuwa hata milele, Amina.

## BABA, MWANA, NA ROHO MTAKATIFU NI *NAFSI* ZINAZOISHI KATIKA UHUSIANO

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kila mmoja ana nafsi na siku zote wameishi katika uhusiano wa kibinafsi wao kwa wao. Tunawaita nafsi kwa sababu wanaishi katika uhusiano wao

kwa wao. Wanapendana, wanatoa kila mmoja kwa wenzake, wanasemezana na kila mmoja anaishi kwa ajili ya wenzake. Hii inaonyesha kuwa wao ni *nafsi.*

## Mfumo katika Utatu wa Mungu

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu siku zote wamekuwa katika mfumo wa mahusiano. Baba ndiye kichwa, kisha Mwana, kisha Roho. Nafsi hizi tatu za milele na zilizo sawa zina nafasi za mamlaka kulingana na mahusiano yaliyopo kati yao. Mfumo huu wa mamlaka unadhihirishwa katika familia na katika kanisa. Kama washiriki wa Utatu wa Mungu, washiriki wote wa familia au kanisa wana thamani sawa, lakini si wote wana nafasi ile ile ya mamlaka.

## Uhusiano Kati ya Mwana na Baba Yake

Mwana anahusianaje na Baba? Yesu alisema kwamba kama Mwana, Baba alimwezesha kuwa na uzima ndani yake, kama vile Baba ana uzima ndani yake (Yohana 5:26). Mwana daima amekuwa Mwana pekee wa Baba (Yohana 3:16). Mwana anaishi milele kama Mungu na ana asili sawa na Baba, lakini kuwepo kwake kunatoka kwa Baba. Mwana daima amehusiana na Baba kama Mwana na Baba daima amehusiana na Mwana kama Baba, ingawa si katika maana ya kimwili.

Yesu ni sawa na Baba katika asili yake. Anapaswa kuabudiwa na kutukuzwa kwa kiwango sawa na Baba. Yesu alisema kwamba wote wanapaswa kumheshimu kama vile wanavyomheshimu Baba (Yohana 5:23).

## Uhusiano Kati ya Roho Mtakatifu na Baba na Mwana

Katika Yohana 15:26, Yesu alisema kwamba atatutumia Roho Mtakatifu, atokaye kwa Baba. Ingawa Roho anatoka kwa Baba, yeye ni sawa na Baba na Mwana, na anapaswa kuheshimiwa kwa kiwango sawa na Baba na Mwana. Kumbuka kwamba Roho kutoka kwa Baba na kutumwa ni mambo yanayotendeka kati ya nafsi tatu zinazoishi katika uhusiano wa upendo.

## Kulinda Umoja wa Mungu

Nafsi tatu za Utatu wa Mungu hazipaswi kuchukuliwa kuwa nafsi tofauti. Umoja wa nafsi hizo unamaanisha kuwa zina asili ile ile *na* kwamba nafsi hizo tatu zinapenyana, kila moja inaishi ndani ya nyingine na zinashiriki sifa zao kati yao. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kila mmoja anaishi ndani ya mwingine kwa njia ambayo haiwezekani katika wanadamu.

Kila mwanadamu ni mtu mmoja tu na nafsi moja tu. Mungu ni nafsi tatu, lakini ni mmoja tu. Ili kusaidia kulinda dhana ya kibiblia ya umoja wa Mungu, hatuzungumzii washiriki wa Utatu wa Mungu kama watu tofauti, bali kama nafsi tofauti.

## TUNAAKISI NAFSI NA MAHUSIANO YA MUNGU

Mungu alituumba kwa mfano wake kama watu — tukiwa na uwezo wa kuhusiana sisi kwa sisi na pia kuhusiana na Mungu. Kila mmoja wetu ana akili, nia na hisia kwa ajili ya kusudi la kuwa na mahusiano.

### Tukiwa Peke Yetu Hatujakamilika

Baada ya Mungu kumuumba Adamu, alisema, "Si vema huyo mtu awe peke yake" (Mwanzo 2:18). Kisha akamuumba Hawa. Adamu hakuwa kamili bila Hawa kwa sababu, bila Hawa, hakuwa na mwanadamu mwingine wa kuhusiana naye. Kwa kweli, andiko moja linapendekeza kwamba Adamu na Hawa *pamoja* waliakisi mfano wa Mungu: "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba" (Mwanzo 1:27). Inaonekana kuna kitu kuhusu uhusiano kati ya Adamu na Hawa ambacho kiliwafanya kwa pamoja waakisi mfano wa Mungu kuliko jinsi Adamu angelifanya akiwa peke yake.

Fikiria hilo linamaanisha nini kwetu. Hatuishi kama watu kamili tusipokuwa katika uhusiano na wengine, kama nafsi za Utatu wa Mungu zilivyo. Hilo halimaanishi kwamba tunapaswa kufunga ndoa (hakuna mtu atakayekuwa katika ndoa mbinguni, lakini bado tutakuwa watu), lakini tunahitaji kuwa na ushirika na wengine.

### Kuhusiana ili Kuakisi Mfano wa Mungu

Kuna ulinganisho wa ajabu kati ya asili ya Mungu na asili ya kanisa. Ndani ya Mungu na kanisa, kuna umoja na utofauti. Kulingana na 1 Wakorintho 12, mwili wa Kristo ni umoja unaojumuisha sehemu nyingi zinazofanya kazi pamoja kwa kusudi fulani. Je, unaweza kuona jinsi mwili wa Kristo unavyoakisi mfano wa Mungu? Paulo alitarajia washiriki wote mbalimbali wa kanisa wakue pamoja kama kitu kimoja katika Kristo. Paulo aliomba kwamba tuweze:

> Kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo (Waefeso 4:15-16).

Sote tunapaswa kutumia karama na uwezo wetu kusaidiana kukua katika umoja wa Kristo. Mungu anatamani kwamba tuakisi asili yake ya kiuhusiano kwa kusaidiana kukua katika neema. Ukuaji wa kiroho hutokea katika jamii, katika ushirika wa karibu na wa kujitolea na waumini wengine. Hilo linaakisi asili ya Mungu ya kijamii.

Ikiwa washiriki wa Utatu wa Mungu wameishi daima katika upendo wa kujitolea kila mmoja kwa mwenzake, tunapaswa kuishi katika mahusiano ya upendo na wengine. Tuliumbwa

kwa mfano wa Mungu kama viumbe wa kijamii na wa kimahusiano, hivyo tunapaswa kuzingatia wengine badala ya sisi wenyewe. Tunapaswa kusisitiza zaidi kuishi kijamii kuliko kuishi kibinafsi. Mungu atatubariki kadiri tunavyojaribu kuakisi mfano wake wa Utatu katika mahusiano yetu na wengine.

## IBADA YA UTATU WA MUNGU

Ibada ya Utatu wa Mungu inatambua kwamba tunakuja kwa Baba kwa usaidizi wa Roho na kwa msingi wa kazi ya upatanisho ya Mwana. Kama watu wanaoamini Utatu wa Mungu, tunapaswa kuomba kwa Baba, katika Roho na kupitia kwa Mwana.

Lengo muhimu la ibada ni sisi kuingia katika uhusiano wa upendo kama ule wa washiriki wa Utatu wa Mungu. Fikiria upendo uliopo kati ya Baba na Mwana. Fikiria kile Kristo alichofanya msalabani ili tuishi katika upendo huo. Baba na Mwana wanaishi katika ushirika wa ajabu, na kwa sababu ya kazi ya upatanisho ya Mwana, Roho anaweza kutusaidia kushiriki katika uhusiano huo wenye upendo wa dhati.

Kama watu wanaoamini Utatu wa Mungu, hatuombi tu kwa Baba, katika Roho na kupitia Mwana, bali pia tunaomba kwa Baba, kwa Mwana na kwa Roho. Kila mmoja wa washiriki wa Utatu wa Mungu anapaswa kuabudiwa na kutukuzwa, kwa kuwa wote ni Mungu na wanapaswa kuheshimiwa kwa kiwango sawa. Ibada ya Utatu wa Mungu huleta utukufu kwa kila mshiriki wa Utatu wa Mungu kwa kiwango sawa, tukitambua jukumu la kila mmoja katika wokovu wetu.

**"Mwenyezi Mungu wa milele, umetupatia sisi watumishi wako neema kwa kukiri imani ya kweli ili tuamini utukufu wa Utatu wa milele, na katika uwezo wa Ukuu wa kiungu kuabudu umoja huo. Utudumishe imara katika imani hii, ili tupate kulindwa daima na maadui wote: katika jina la Yesu Kristo Bwana wetu, anayeishi na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, sasa na hata milele. Amina."**

*Book of Common Prayer*

## MAKOSA YA KUEPUKA: NADHARIA KUHUSU UTATU WA MUNGU

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshiriki wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Hatuelewi kwa nini mbegu hukua kwenye udongo, au jinsi ubongo unavyofanya kazi, au ni nguvu gani zinashikilia nyota mahali pao. Wanasayansi wanaona yale yanayotokea, lakini hawawezi kueleza kwa nini na jinsi yanavyotokea. Si jambo la busara mtu kukataa

kanuni ya Utatu wa Mungu kwa sababu hawezi kuifafanua kikamilifu. Hatuna uwezo wa kueleza kanuni yoyote kuhusu Mungu. Kwa mfano, hakuna mtu anayeweza kueleza jinsi Mungu anavyoweza kuwa kila mahali na kujua mambo yote. Si kwamba mambo ya kweli kuhusu Utatu wa Mungu si ya kimantiki, bali yanapita uwezo wa mwanadamu. Samaki wa baharini, hata kama angekuwa na akili kiasi gani, hawezi kuelewa jinsi ilivyo kuwa mwanadamu, hata kama angeelezwa.

Ukweli wa Utatu wa Mungu ni kwamba kuna Mungu mmoja anayeishi katika nafsi tatu zinazofanana katika asili na ziko sawa katika uungu. Watu wamejaribu kuelezea jambo hili, lakini mara nyingi hupoteza sehemu muhimu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya makosa.

1. **Mungu kwa kweli ni mmoja lakini amechukua majukumu tofauti**. Katika nadharia hii, mbinguni Mungu ni Baba, duniani alikuwa Yesu na sasa ananena nasi kama Roho Mtakatifu. Lakini katika sura zote za Yohana 14-16, maneno ya Yesu yanaeleza mwingiliano kati yake na Baba na Roho Mtakatifu. Maelezo hayo hayangekuwa na maana ikiwa watatu hao si nafsi tatu tofauti.

2. **Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni nafsi tatu tofauti**. Katika nadharia hii, kunaweza kuwa na tofauti katika asili yao. Kwa mfano Baba anaweza kuwa ndiye anayetaka kuhukumu lakini Mwana anataka kuonyesha rehema. Wazo hili linakinzana na kanuni ya Biblia kwamba kuna Mungu mmoja tu.

3. **Nafsi moja katika Utatu wa Mungu ni duni kuliko nyingine**. Mtu anayeamini wazo hili humwona Baba kama Mungu na Mwana na Roho Mtakatifu kama nafsi zingine zilizo chini yake. Anaweza kukana kuwepo kwa nafsi ya Roho na kumwona Mwana kama mtu maalum ambaye Mungu alimtumia. Kosa hili huwafanya watu wasimuabudu Mwana na Roho Mtakatifu kama Mungu na linaweza kusababisha injili ya uwongo.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Mungu anaishi katika Utatu, Mungu mmoja katika nafsi tatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Watatu hawa wanatekeleza majukumu tofauti, lakini wana asili sawa na sifa sawa za kiungu na wote wanastahili kuabudiwa.

## MAZOEZI YA SOMO LA 3

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Yohana 15:26
    - Yohana 17:1-5
    - Waefeso 1:17-23
    - Wakolosai 1:12-19
    - Waebrania 1:1-3, 8

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 3. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 3

1. Je, ulimwengu unaonyeshaje asili ya Mungu?
2. Je, ni kauli gani tatu za kibiblia ambazo ni msingi wa kanuni ya Utatu wa Mungu?
3. Je, mfumo wa mahusiano ndani ya Utatu wa Mungu ni upi?
4. Je, mfumo wa familia au kanisa unalinganaje na mfumo wa Utatu wa Mungu?
5. Kama watu wanaoamini Utatu wa Mungu, tunapaswa kuomba nani?
6. Taja nadharia tatu potovu za kawaida kuhusu Utatu wa Mungu.

## SOMO LA 4

# UBINADAMU

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Jinsi tunavyojua kwamba mfano wa Mungu katika ubinadamu si mfano wa kimwili.
    - Sifa nane za mfano wa Mungu katika ubinadamu.
    - Kwamba watu wameumbwa kimahususi kwa ajili ya kuwa katika uhusiano na Mungu.
    - Maana ya jinsi watu wana uhuru wa kuchagua.
    - Kwamba watu wana thamani isiyo na kipimo zaidi ya thamani yao ya kiutendaji katika maisha ya kidunia.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu ubinadamu.

2. Mwanafunzi ataelewa kwamba hawezi kuridhika akiwa mtu asiye na uhusiano na Mungu.

## UBINADAMU - KUUMBWA KWA MFANO WA MUNGU

» Someni Zaburi 8 pamoja. Je, kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu ubinadamu?

» Je, ni mambo gani yanayofanana kuhusu kila mtu duniani?

Fikiria juu ya kile kinachotupa utambulisho wetu. Je, ni nini hasa maana ya ubinadamu?

» Someni Mwanzo 1:26-27 pamoja.

Kuna kitu kuhusu asili yetu ambacho ni kama Mungu. Sisi si Mungu, lakini kuna kitu kinachotutenganisha na ulimwengu wa wanyama na kutufanya tuwe wa kipekee. Katika Zaburi 8:5, mwandishi anafurahi kwamba tumeumbwa kuwa chini kidogo kuliko viumbe wa mbinguni na tumevikwa taji la utukufu na heshima.

Mungu aliwapa wanadamu jukumu maalum la kusimamia dunia na viumbe wanaoishi duniani (Zaburi 8:6). Watu wanapaswa kusimamia dunia kwa uangalifu ili kuepuka kupotea kwa viumbe hai, kutumia rasilimali kwa hekima na kuacha dunia ikiwa katika hali nzuri kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mtazamo huu unaompa mwanadamu hadhi ya juu kwa hakika ni bora zaidi kwa ajili ya kujiheshimu sisi wenyewe kuliko kanuni ya mageuzi! Kakanuni ya mageuzi hakuna umuhimu maalum katika maisha ya mwanadamu, hakuna kusudi, hakuna maana, hakuna kitu maalum kuhusu kuwa mwanadamu.

Kwa mujibu wa baadhi ya hadithi za kale, watu waliumbwa kwa bahati mbaya, bila kusudi, na hawapendwi na muumbaji yeyote. Lakini Biblia inafundisha kwamba sisi ni viumbe maalum, tulioumbwa kwa mfano wa Mungu. Hiyo inamaanisha nini?

Mfano wa Mungu katika wanadamu haimaanishi kufanana kimwili.

» Je, tunajuaje kwamba mfano wa Mungu katika wanadamu haumaanishi kufanana kimwili?

1. **Mungu ni roho** (Yohana 4:24). Sulemani alitambua kwamba mbingu na dunia yote haiwezi kumtosha Mungu (1 Wafalme 8:27). Mungu angeweza kujidhihirisha kupitia mwonekano wowote aliotaka, lakini hakuna mwonekano wowote unaofanana na Mungu. Hiyo ndio sababu moja kwa nini hatupaswi kutengeneza sanamu za Mungu ili kuziabudu.

2. **Kutengeneza sanamu za Mungu zinazofanana na mwanadamu ni ibada ya sanamu**. (Soma Warumi 1:23.)

3. **Watu wameumbwa kimwili kwa ajili ya maisha duniani**, wakiwa na miguu ya kutembea, mikono ya kusogeza vitu na uwezo wa kuona na kusikia kwa ajili ya kutambua vitu. Mungu alituumba ili tuishi duniani. Lakini Mungu anaishi katika ulimwengu wote. Anaweza kuumba na kusababisha matukio kwa Neno lake. Hana mapungufu yoyote kama yetu. Hakuna sababu ya kufikiri kwamba ana umbo la kimwili la kibinadamu.

## VIPENGELE VYA MFANO WA MUNGU VILIVYOTOLEWA KWA WANADAMU

» Je, ni zipi baadhi ya sifa za wanadamu zinazoakisi mfano wa Mungu?

Wanatheolojia wamefikiria sana kuhusu maana ya mwanadamu kuwa katika mfano wa Mungu, na wengi wanakubaliana kuhusu sifa zifuatazo.

## Silika ya Ubunifu

Tuna silika ya ubunifu inayotokana na mfano wa Mungu ulio ndani yetu. Muumba wetu ametufanya tuwe wabunifu! Wakati mwingine wanyama wamefunzwa kuchora alama ambazo watu wanaziita sanaa. Lakini hiyo ni tofauti sana na sanaa inayochorwa na mtu anayeeleza wazo fulani. Michoro ya kale imepatikana kwenye mapango. Hatujui mengi kuhusu watu waliozichora, lakini hakuna mtu aliye na shaka kwamba zilichorwa na watu wala si wanyama.

Ubunifu pia umedhihirishwa katika muziki. Muziki una uwezo wa ajabu wa kueleza mawazo na hisia zetu. Uwezo wa kuwasilisha mawazo kupitia muziki unatokana na mfano wa Mungu ulio ndani yetu.

## Uwezo wa Kufikiria

Uwezo wa kufikiria ni uwezo mwingine kama wa Mungu. Wanyama pia wana ubongo, lakini kulingana na ufahamu wetu, shughuli za ubongo wa wanyama haziwezi kufanya kazi zaidi ya kiwango cha silika na kutenda pasipo kufikiria. Wanadamu pekee ndio wenye uwezo wa kuchanganua, kutathmini, na kutafakari, kisha kuwasiliana kwa ushawishi.

Hatuwezi kufikiria tu, tunaweza hata kufikiria juu ya kufikiria. Tunaweza kuchanganua michakato ya mawazo. Hatuwezi tu kufikiria kimantiki, pia tunaweza kufikiria juu ya mantiki.

## Uwezo wa Kuwasiliana

Wanadamu wana uwezo wa kuwasiliana. Uwezo huo unadhihirishwa na matumizi ya lugha, ambapo mawazo yanawekwa katika sauti au ishara ambazo watu wengine wanaelewa. Wanyama kama vile mbwa na ndege wanaweza kuwasiliana kupitia sauti, lakini hakuna chochote kinachokaribia uchangamani wa lugha ya mwanadamu kinajulikana kuwepo katika wanyama. Wanyama wana njia za kutishia wanyama wengine, kumiliki eneo fulani au kugawana chakula, lakini hawawezi kuwa na majadiliano kuhusu maana ya maisha.

Uwezo wa kuwasiliana hutegemea uwezo wa kufikiria na kutumia mantiki. Wanyama hawawezi kusema maneno, lakini hata kama wangeweza, hawangekuwa na mengi ya kusema.

## Asili ya Kijamii

Wanadamu wana asili ya kijamii. Tumeumbwa kutangamana na watu wengine, kutoa ahadi kwa wengine na kutegemea wengine. Tunaanza maisha tukiwategemea wengine kikamilifu, na inachukua miaka mingi mtoto kuwa mtu mzima. Hiyo ni kwa sababu mahusiano ni muhimu kwa Mungu.

Mungu amepanga maisha ya mwanadamu ili watu wafanye kazi pamoja na wadumishe mahusiano ili mahitaji yao ya kila siku yakidhiwe. Hata kama mtu angeweza kupata vitu kama vile chakula na makao bila msaada wa mtu yeyote, bado atakuwa na mahitaji muhimu ambayo yanaweza kukidhiwa tu katika uhusiano na wengine. Asili ya kijamii ya mwanadamu inaakisi asili ya Mungu. Mungu ni Utatu na daima yuko katika uhusiano.

Mahusiano ya kibinadamu yana matatizo mengi. Kwa sababu ya matatizo hayo, watu wengine hufikiri wanahitaji kujitegemea zaidi. Wanataka kuishi bila kutegemea mtu yeyote. Kuishi peke yako si suluhisho wala si maisha ambayo Mungu alitupangia. Badala yake, alitupa kanuni za kuishi katika uhusiano. Matatizo huja wakati hatufuati mpango wa Mungu.

## Dhamiri ya Kimaadili

Tuna dhamiri ya kimaadili ambayo ni sehemu ya asili yetu. Kuna kitu ndani yetu ambacho hutuambia kwamba matendo mengine ni sahihi na mengine si sahihi. (Soma Warumi 1:20; Warumi 2:15.) Inatuambia wakati ambapo ni sahihi kufuata tamanio fulani na wakati ambapo hatupaswi kufanya hivyo. Adamu na Hawa waliumbwa wakiwa watakatifu na waliweza kufuata mapenzi ya Mungu kikamilifu.

Kwa sababu wanadamu wameanguka katika dhambi na kuharibu mtazamo huo wa msingi wa kimaadili, bado kumebaki ndani ya kila mmoja wetu uwezo wa kuelewa dhana ya mema na mabaya ingawa uwezo huo si sahihi kikamilifu.

Kwa sababu tuna dhamiri ya kimaadili, tunahisi tuna wajibu wa kufanya mema, na tunahisi kuwa na hatia tukitenda dhambi. Sisi si kama wanyama, ambao hufuata silika zao za asili bila hisia ya hatia.

> **"Leo watu wanajaribu kushikilia hadhi ya mwanadamu, lakini hawajui jinsi ya kufanya hivyo, kwa sababu wamepoteza ukweli kwamba mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu.... Tunatazama utamaduni wetu ukitekeleza ukweli kwamba unapowaambia wanadamu kwa muda wa kutosha kwamba wao ni mashine, hilo huanza kuonekana katika matendo yao baada ya muda mfupi"**
>
> **Francis A. Schaeffer**

## Uwezo wa Kuchagua

Uhuru wa kuchagua, au uwezo wa kuchagua, ni tabia ya wanadamu. Kinyume chake, machaguo ya wanyama yako kwenye kiwango cha msukumo wa muda mfupi na silika. Wanyama hawafanyi maamuzi yaliyofikiriwa kwa uangalifu yanayozingatia maadili au matokeo ya kiutendaji ya matendo yao. Wanadamu wana uwezo wa kufanya maamuzi yenye maana, yenye kubadilisha maisha. (Soma Yoshua 24:15.)

» Kwa nini uhuru wa kuchagua ni kipengele muhimu cha ubinadamu?

Kwa sababu tunafanya maamuzi halisi, tunawajibika kwa Mungu. Ataadhibu dhambi na kutoa thawabu kwa wenye haki (Ufunuo 20:12-13).

Kwa sababu tumezaliwa na asili ya dhambi, hatutumii uhuru wetu wa kuchagua kwa njia inayomheshimu Mungu. Mtu kwa asili yake ni mtumwa wa dhambi (soma Warumi 6:16-17, Waefeso 2:1-3), hawezi kutenda mema, lakini neema ya Mungu inamfikia kila mtu, ikitoa hamu na uwezo wa kuitikia injili. Ndio maana mtu anaweza kuchagua kutubu na kuamini injili. (Soma Marko 1:15.)

## Kutokufa

Kutokufa ni sifa muhimu ya mfano wa Mungu. Kuna wakati ambapo hatukuwepo, lakini kila mtu atakuwepo milele tangu wakati wa utungaji wa mimba yake. Sisi si viumbe wa kimwili tu, bali pia ni roho ambazo zitaishi milele, na hata miili yetu itafufuliwa katika umbo la milele. (Soma 1 Wakorintho 15:16-22, 52-54.) Mungu alimuumba kila mmoja wetu kwa kusudi la milele. Kutokufa kunafanya maamuzi yetu yawe muhimu milele kwa sababu tutaishi milele mbinguni au jehanamu.

## Uwezo wa Kupenda

Uwezo wa kupenda ni sehemu ya mfano wa Mungu. Miongoni mwa wanyama, mahusiano ni machache sana, na yanadhibitiwa zaidi na silika.

Tabia zingine za ubinadamu ni muhimu kwa sifa hii. Upendo usingekuwa na maana kama tusingekuwa na uwezo wa kuwasiliana, uwezo wa kuchagua na kutoa ahadi kwa wale tunaowapenda na uwezo wa kuitikia kwa busara tunapopokea upendo kutoka kwa wengine.

Upendo wa kibinadamu unadhihirishwa kwa furaha katika uhusiano, kutoa na kutimiza ahadi, kutoa na kutumika kwa kujinyima, na msamaha. Yote haya ni madhihirisho ya upendo wa Mungu.

## Uwezo wa Kuabudu

Sifa muhimu sana ni uwezo wetu wa kuabudu. Fikiria nyimbo unazozipenda zaidi za kumtukuza Mungu. Tunaimba, “Mungu wetu ni Mungu wa ajabu.” “Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu” ni wimbo usiopitwa na wakati wa kuabudu kwa dhati. Mtunga Zaburi alisema, “Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu” (Zaburi 103:1). Maneno haya yanawezekana kwa sababu mfano wa Mungu ulio ndani yetu unamtambua na kumwitikia Mungu ambaye tumeumbwa kwa mfano wake!

## KUSUDI LA MFANO WA MUNGU KATIKA UBINADAMU

Ni vizuri kutafakari kwa nini Mungu alituumba kwa mfano wake. Kwa nini sisi ni tofauti sana na viumbe wengine wote? Jibu ni kwamba tumeumbwa kimahususi kuwa katika uhusiano na Mungu na kumwabudu.

Biblia inatuambia kwamba uumbaji kwa ujumla humletea Mungu utukufu. Tunaona ukuu wa Mungu katika vitu alivyoviumba. Lakini viumbe wengine wanamtukuza Mungu bila ufahamu. Hawawezi kuelewa jinsi Mungu alivyo kwa sababu hawana asili inayoweza kuhusiana naye.

Tunaweza kuvutiwa na ubunifu wa Mungu usio na kipimo kwa sababu tuna kiwango fulani cha ubunifu. Tunaweza kuabudu utakatifu na haki yake kwa sababu tuna dhamiri ya mema na mabaya. Tunaweza kustaajabishwa na upendo wake usio na kipimo kwa sababu tuna uwezo wa kupenda.

Kadiri tunavyomjua Mungu vizuri zaidi, si tu katika ufahamu wa kiakili bali katika uhusiano, ndivyo tunavyompenda na kumwabudu zaidi. Tunapata shangwe na uradhi katika uhusiano na Mungu kwa sababu alituumba kwa ajili ya uhusiano huu.

## MAWAZO MENGINE MUHIMU

1. **Wanadamu wote wana mfano wa Mungu** (Mwanzo 1:27)**.** Kuna watu ambao kwa sababu ya mapungufu ya kiakili hawawezi kufikiria kimantiki, kujieleza kwa ubunifu au kutumia uhuru wa kuchagua. Mfano wa Mungu umeumbwa ndani yao, lakini hauwezi kutumika katika maisha yao ya kidunia.

2. **Maisha ya kila mwanadamu yana thamani ya milele na isiyo na kipimo.** Wakati mwingine tunaona thamani ya mtu ya kiutendaji, mambo kama vile akili, elimu, vipawa au nguvu yake. Lakini kila mtu ana thamani ambayo ni muhimu zaidi kuliko thamani yake ya kiutendaji, kwa sababu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Ndio maana kila mtu anastahili heshima kama binadamu, hata kama anakosa vitu vinavyowapa watu thamani ya kiutendaji, na hata kama yeye ni mtu mwovu. Mfano wa Mungu pia ndio sababu kwa nini kila mtoto ni wa thamani kwa Mungu, na kutoa mimba ni dhambi mbaya sana (Mwanzo 9:6, Zaburi 139:13-14, Isaya 44:24).

3. **Malaika pia ni wa kipekee katika uumbaji.** Wana akili nyingi, uwezo wa kufikiria kimantiki, uwezo wa kuwasiliana na uwezo wa kuabudu. Kwa hivyo wana baadhi ya vipengele vya mfano wa Mungu na wanaitwa wana wa Mungu katika maandiko (Ayubu 1:6). Kwa sasa uwezo wetu ni duni ukilinganishwa na uwezo wa malaika (Zaburi 8:5), hata hivyo, wanatutumikia (Waebrania 1:14). Katika uzima wa milele, tutakuwa na nafasi ya juu kuliko malaika (soma 1 Wakorintho 6:3), na tutatawala pamoja na Kristo. Hilo

linamaanisha kwamba wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu kwa ukamilifu zaidi kuliko malaika.

4. **Ulimwengu hauko katika umbo lake la asili.** Fikiria mchoro wa kuvutia, uliochorwa na mchoraji stadi. Fikiria mchoro huo umetupwa sakafuni, na watu wakaukanyaga na viatu vyenye matope. Ukiangalia mchoro huo, bado unaweza kuona ustadi mkubwa uliouchora, lakini mchoro huo hauko jinsi ulivyokuwa wakati mchoraji aliumaliza hapo mwanzoni. Uumbaji uko hivyo. Hauko kama vile Mungu alivyokusudia uwe, lakini utukufu wake bado unaonekana.

5. **Dhambi imepotosha uwezo "kama wa Mungu" ulio ndani ya watu.** Kwa mfano, kazi ya sanaa inaweza kudhihirisha moyo mwovu na inaweza kuwa chombo cha Shetani, ingawa kipawa chenyewe kinatoka kwa Mungu. Hata hivyo, kwa sababu ya neema kuingilia kati, dhambi haijaharibu kabisa mfano wa Mungu ndani yetu. Kwa neema Mfano wa Mungu ndani yetu unaweza kufanywa upya, kukuzwa na kudhihirishwa kwa utukufu wa Muumba wetu! (Soma Wakolosai 3:10; Waefeso 4:22-24; 2 Wakorintho 3:18.)

6. **Mfano wa Mungu ulio ndani yetu ndilo jambo muhimu zaidi kutuhusu.** Mfano wa Mungu ulio ndani yetu unatuwezesha kuitikia injili. Dhamiri yetu ya kimaadili huwezesha neema kuamsha dhamiri zetu na kutusadikisha juu ya dhambi. Uhuru wa kuchagua uliorejeshwa kupitia neema inayofanya kazi ndani yetu unatuwezesha kuchagua ni nani tutakayemtumikia. Kupitia silika yetu ya ubunifu tunaweza kumletea Mungu utukufu na heshima. Kwa kutumia mantiki, tunaweza kuchunguza kweli zilizofichika na kuelewa mambo fulani kumhusu Mungu na njia zake. Kutafuta kumwelewa Mungu kunageuka kuwa ibada kadiri tunavyozidi kufahamu ukuu kamili wa Muumba wetu ambaye kwa neema kubwa ametuvika taji la utukufu na heshima!

## MAKOSA YA KUEPUKA

Wakati mwingine watu hufikiri kwamba uhusiano na Mungu una umuhimu kwa maisha ya baada ya kifo pekee. Wanafikiri kwamba ikiwa mtu anaishi maisha mazuri duniani, si jambo muhimu ikiwa yeye ni Mkristo au la. Lakini ikiwa tunaelewa kwamba asili ya ubinadamu imeumbwa kwa ajili ya kuwa na uhusiano na Mungu, tunatambua kwamba maisha yetu kwa kiasi kikubwa yanakuwa hayana maana ikiwa hatumjui Mungu. Tunahitaji Roho wa Mungu ndani yetu, akituongoza, akitimiza uwezo wetu, na akitupatia mtazamo wa milele kwa yote tunayofanya.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu kwa kusudi la kumpenda na kumwabudu Mungu. Mungu aliumba watu wakiwa na uwezo wa kufikiria, kuwasiliana na kupenda. Mtu ana dhamiri ya kimaadili, nia ya kibinafsi na roho isiyokufa. Neema ya Mungu humpa mtu uwezo wa kufanya maamuzi huru. Maisha ya kila mwanadamu yana thamani ya milele na isiyo na kipimo.

## MAZOEZI YA SOMO LA 4

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Mwanzo 3:1-6
    - Yoshua 24:14-18
    - Warumi 6:12-23
    - Warumi 8:22-26
    - Waefeso 2:1-9
    - 1 Wathesalonike 5:23
    - Yakobo 1:12-15

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 4. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 4

1. Kulingana na Mwanzo 1:26-27, watu ni wa kipekee kwa jinsi gani wakilinganishwa na viumbe wengine wote?

2. Taja sababu tatu zinazotufanya tujue kwamba mfano wa Mungu katika ubinadamu si mfano wa kimwili.

3. Orodhesha vipengele saba vya mfano wa Mungu katika ubinadamu.

4. Je, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu kwa sababu gani mbili?

5. Je, ni uwezo gani unatokana na dhamiri ya kimaadili?

6. Je, uwezo wa watu wa kufanya machaguo halisi una umuhimu gani?

# SOMO LA 5

# DHAMBI

## MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Asili ya dhambi.
    - Maneno ya kibiblia ya dhambi.
    - Ufafanuzi na maelezo kuhusu upotovu wa kurithi.
    - Dhana ya kibiblia ya dhambi ya makusudi.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu dhambi.

2. Mwanafunzi ataelewa uongofu vyema zaidi akiwa na ufafanuzi wa kueleweka wa dhambi ya makusudi.

## UTANGULIZI

» Someni Mwanzo 3 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu dhambi?

» Je, kwa nini tunahitaji kuelewa dhambi?

Lazima tuelewe dhambi:

1. **Ili tuelewe hali ya ulimwengu**. Biblia inatuambia kwamba dhambi ndio chanzo cha mateso ya wanadamu. Ni kupitia dhambi ndio kifo kilikuja ulimwenguni. (Soma Warumi 5:12.) Kwa sababu ya laana ya dhambi, kuna magonjwa, kuzeeka na uchungu. Matendo ya dhambi kama vile kusema uongo, kuiba, kuua, uzinzi, ulevi na ukandamizaji yamejaza dunia mateso. Matendo ya dhambi yanatokana na dhambi iliyo moyoni, kama vile chuki, tamaa ya kimwili, kutamani vitu vya wengine, kiburi na ubinafsi.

2. **Ili tuelewe neema na wokovu**. Mungu anatoa neema ili kutuokoa kutokana na dhambi (Mathayo 1:21; Warumi 5:20-21).

3. **Ili tuelewe utakatifu**. Dhambi ni kinyume cha utakatifu. Ni kinyume cha kujitolea kwa Mungu. Ili mtu awe mtakatifu jinsi Mungu anavyotarajia (1 Petro 1:15-16), ni lazima atengwe na dhambi.

## ASILI YA DHAMBI

Uumbaji wa Mungu ulikuwa kamili, na hakuna kitu alichoumba ambacho kilikuwa na kasoro. Mungu alipomaliza uumbaji, aliona kuwa ni mzuri sana (Mwanzo 1:31). Kwa hivyo, tunajua kwamba dhambi haikuwa kosa la Mungu.

Adamu na Hawa walikuwa katika uhusiano na Mungu. Walitamani kumpendeza Mungu na walikuwa na uwezo wa kufanya kila kitu kilicho sahihi. Shetani alikuja kumjaribu Hawa ili asimtii Mungu. Kupitia tukio hilo tunajua kwamba dhambi tayari ilikuwepo katika ulimwengu. Shetani alikuwa tayari ameanguka katika dhambi. Lakini dhambi ilikuwa bado haijaingia katika mwanadamu au sehemu ya uumbaji ambayo ilikuwa chini ya mamlaka ya mwanadamu.

Adamu na Hawa walikuwa na uhuru wa kuchagua. Dhambi iliwezekana kwa sababu waliweza kufanya chaguo halisi. Walichagua kuvunja sheria ya Mungu, na huo ukawa mwanzo wa dhambi ya wanadamu.

Tendo la kwanza la dhambi lilitenganisha mwanadamu na Mungu. Dhambi pia iliharibu asili ya ubinadamu. (Soma Zaburi 51:5.) Watoto wote watakaozaliwa baadaye watakuwa na asili iliyoharibika na watatenda dhambi. (Soma Warumi 5:12, 14, 18-19.)

Dhambi ilileta laana kwa viumbe wote (Mwanzo 3:16-19). Maisha yalibadilishwa kwa sababu ya dhambi. Uchungu, kuzeeka na kifo vilianza. (Soma 1 Wakorintho 15:22.) Kufanya kazi na kujikimu kimaisha kukawa kugumu. Mahusiano ya kibinadamu yakajaa migogoro. Kadiri miaka ilivyopita na watu kuongezeka, matokeo ya dhambi yaliongezeka zaidi ya vile Adamu na Hawa wangeweza kufikiria.

## MANENO YA KIEBRANIA NA KIGIRIKI YANAYOMAANISHA DHAMBI

Lugha nyingi zina visawe tofauti vya dhambi. Kiebrania na Kigiriki, lugha asili za maandiko, pia zina maneno mengi tofauti yanayoeleza au kufafanua dhambi, ambayo yameelezwa hapa chini. Yanapochukuliwa pamoja, maneno haya yanatoa taswira kamili ya dhambi.

> **"Dhambi na mwana wa Mungu hawaambatani. Wanaweza kukutana mara moja moja lakini hawawezi kuishi kwa amani"**
>
> **John Stott**

- **Dhambi kama kukataa mamlaka—uasi** (Zaburi 51:1). Yakobo alitumia neno hili la

Kiebrania alipomwambia Labani kwa hasira amwambie ni kosa gani alilomtendea (Mwanzo 31:36). Neno hilo pia linaeleza kitendo cha mfalme wa Moabu dhidi ya Mfalme Yehoramu (2 Wafalme 3:7).

- **Dhambi kama upotovu au upotoshaji—kile ambacho kimekunjika au kupindika** (Zaburi 51:2a). Shetani hawezi kuumba kitu chochote, kwa hivyo dhambi zote ni upotoshaji wa kitu kizuri ambacho Mungu ameumba.

- **Dhambi kama kukosa shabaha au kushindwa kufikia lengo**. Neno la Kiebrania la dhambi lililotumika katika Zaburi 51:2b lina maana hii. Neno hilo hilo linatumika kwa maana isiyo ya kimaadili katika Waamuzi 20:16, ambayo inaeleza kuhusu wapiganaji 700 waliotumia mkono wa kushoto ambao waliweza kupiga unywele mmoja kwa jiwe bila kukosa shabaha wakitumia kombeo. Dhambi ni kukosa shabaha ya ukweli, utakatifu, au haki ya Mungu.

  Neno la Kigiriki katika Agano Jipya lina maana sawa na hilo. Neno hilo linaweza kutumika kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima (Mathayo 1:21) au dhambi za mtu mahususi kama vile dhambi za mwanamke aliyeosha miguu ya Yesu (Luka 7:48-50) au dhambi ya mtu binafsi kama vile dhambi ya kumuua Stefano (Matendo 7:60). Dhambi ni kukengeuka kutoka kwenye mapenzi ya Mungu.

- **Dhambi kama kitu kibaya, kinyume cha kitu chema** (Zaburi 51:4). Neno hilo hilo la Kiebrania limetumika kueleza kuhusu wale ng'ombe saba waliokonda katika ndoto ya Farao (Mwanzo 41:19) na tini ambazo hazingeweza kuliwa katika Yeremia 24:2.

- **Dhambi kama kukataa kusikia, na hivyo kusababisha kutotii** (Warumi 5:19). Mfano wa tabia hii umetolewa katika Matendo 7:57, ambapo wale waliokuwa wakimpiga Stefano mawe waliziba masikio yao. Muhtasari bora zaidi wa neno hili la Kigiriki ni kutotii.

- **Dhambi kama kuvunja sheria fulani mahususi—kufanya kinyume cha kile ambacho Mungu anataka** (1 Yohana 3:4). Neno hilo la Kigiriki limeundwa na maneno mawili ambayo kwa pamoja yanamaanisha "hakuna sheria" au "kuasi sheria."

- **Dhambi kama kugeuka kando kwa makusudi au kuvuka mipaka ya kile kinachojulikana na kuhitajika na Mungu** (Kutoka 32:7-8). Katika kifungu hiki, watu walianza kugeuka kando kutoka kwa Mungu wakati Musa alikuwa juu ya Mlima Sinai.

- **Dhambi ambazo si za makusudi** (Mambo ya Walawi 4:2). Aina hii ya dhambi inajadiliwa katika Agano la Kale na Agano Jipya. Neno la Kigiriki linalotumiwa katika Waebrania 9:7 linatokana na kitenzi kinachomaanisha "kutojua," au "kutoelewa," na kwa hivyo linamaanisha "kutenda dhambi kwa kutojua." Kifungu hiki kinaeleza upatanisho ambao Kuhani Mkuu alifanya kwa ajili ya dhambi za watu ambazo si za makusudi.

Kutokana na maneno haya tunaona kwamba dhambi ni tatizo lenye vipengele vingi. Baadhi ya maneno yanaeleza dhambi katika maana yake ya jumla. Maneno mengine yanaonyesha dhambi inayotokana na kukataa kusikia Neno la Mungu, dhambi zinazotokana na kushindwa kuishi kulingana na kiwango fulani, dhambi za makusudi za kudhamiria, au dhambi zinazotokana na kutojua au hata bahati mbaya. Vyovyote ilivyo, ni baraka kukumbuka kwamba Yesu alikufa msalabani ili kuwaokoa watu kutokana na dhambi zao (Mathayo 1:21).

## DHAMBI YA MAKUSUDI

» Dhambi ya makusudi ni nini?

Dhambi ya makusudi ni ukiukaji wa makusudi wa mapenzi ya Mungu yanayojulikana. (Soma 1 Yohana 3:4; Yakobo 4:17.) Ni wakati mtu anachagua kufanya au kuendelea kufanya yale ambayo anajua ni mabaya au kutofanya kile kilicho sahihi. Ni kufanya makosa kwa makusudi.

Katika 1 Yohana 3:5-6 Mtume Yohana anaandika,

> Nanyi mnajua ya kuwa yeye [Yesu] alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua.

Dhambi inayozungumziwa hapa ni mazoea ya kuendelea kutenda dhambi ya makusudi. Tafsiri iliyopanuliwa ya kifungu hicho itakuwa hivi: Yeyote **anayeendelea kukaa** ndani ya Yesu hatendi dhambi **mara kwa mara** au **kwa mazoea**, na yeyote ambaye **anaendelea au ana mazoea ya** kutenda dhambi hajamwona wala hajamjua.

Ikiwa mtu atafasiri kwamba kifungu hiki kinazungumzia dhambi katika maana yake ya jumla (ikijumuisha dhambi kutokana na kutojua na dhambi zisizo za makusudi), kauli hii haina maana. Wakristo bado wana mapungufu ambayo si ya makusudi. Hata hivyo, ikiwa mtu anaelewa kwamba *dhambi* (katika kifungu hiki) inamaanisha "kukataa kwa makusudi sheria ya Mungu," basi kifungu hicho kinaleta maana nzuri kabisa.

## UPOTOVU WA KURITHI

» Je, unaweza kuelezeaje asili ya dhambi ambayo watu huzaliwa nayo?

**Upotovu wa kurithi** ni upotovu wa asili ya kimaadili ya mwanadamu ambao unampa msukumo wa kutenda dhambi tangu anapozaliwa. Wakati mwingine unaitwa dhambi ya asili. Ni asili ya dhambi ambayo tunazaliwa nayo kwa sababu ya dhambi ya Adamu.

Watu wote wana msukumo huo wa kutenda uovu tangu wanapozaliwa. (Soma Zaburi 58:3.) Asili ya mtu tayari imepotoshwa na msukumo wa kutenda dhambi tangu anapozaliwa. Mtu

huanza kutenda dhambi mara tu anapoanza kufanya maamuzi. Msukumo wa kutenda dhambi si kitu anachojifunza kutokana na mazingira yake.

Daudi alisema kwamba alizaliwa katika uovu na mimba yake ilitungwa katika dhambi. (Soma Zaburi 51:5.) Hakumaanisha kwamba mama yake alifanya makosa. Alimaanisha kwamba wakati mtoto mchanga anaumbwa tumboni, asili yake tayari huwa imesharibiwa na dhambi.

Kwa sababu ya asili iliyoharibika, mfano wa Mungu ulio ndani ya watu umeharibiwa. Kila mtu amezaliwa na nia ambayo ni ya ubinafsi na yenye msukumo wa kutenda dhambi (Warumi 3:10-12). Nia zetu hazina uhuru wa kuchagua haki isipokuwa Mungu atupe hamu na nguvu ya kufanya hivyo. (Soma Warumi 6:16-17.)

Upotovu wa kurithi huchochea dhambi za ndani kama vile kiburi, wivu, chuki na kutosamehe. Pia huchochea matendo ya dhambi.

Kwa kawaida watu wana mtazamo wa kuasi mamlaka ya Mungu na wana hasira na sheria yake. Wanaotenda dhambi watahukumiwa si tu kwa ajili ya matendo yao ya dhambi bali pia kwa ajili ya mtazamo wao wa kumuasi Mungu. (Soma Yuda 1:15.)

Mtu aliye na asili ya dhambi kwa kawaida ni mwenye ubinafsi. Anataka kudai mapenzi yake mwenyewe badala ya kujiweka chini ya mamlaka ya Mungu na wengine. Anataka kutosheleza tamaa zake mwenyewe badala ya kumpendeza Mungu. Anajiamini na hataki kumtegemea Mungu. Mafanikio yake mwenyewe ni muhimu zaidi kwake kuliko utukufu wa Mungu.

Watu hawapambanui kwa usahihi mema na mabaya, kwa sababu akili zao zimetiwa giza. (Soma Waefeso 4:17-18.) Kwa sababu ya asili yao, wanafuata mwelekeo wa ulimwengu wenye kuasi, udhibiti wa Shetani, na tamaa zao zilizopotoka; na wanajiweka chini ya ghadhabu ya Mungu. (Soma Waefeso 2:2-3.) Msukumo wao wa asili ni kutenda dhambi kila wakati (Mwanzo 6:5).

Bila msaada wa neema ya Mungu, watu wasingeweza kufanya kitu chochote kizuri; wala wasingetamani hata kutenda mema. Wasingeweza kutubu au kumtafuta Mungu. (Soma Yohana 6:44.) Wamekufa katika makosa na dhambi (Waefeso 2:1). Wanatheolojia wanafafanua hali hii kama “upotovu kamili.”

Ni muhimu kujua jinsi neema ya Mungu inavyoitikia upotovu wa kurithi. Kwanza, nguvu ya Mungu huja na ujumbe wa injili, ikimpa mtu aliyepotea hamu na uwezo wa kuitikia injili. (Soma Warumi 1:16.) Kisha, mtu anapookolewa, anakombolewa kutokana na udhibiti wa dhambi (Warumi 6:11-14). Hata hivyo, ushawishi wa upotovu wa kurithi unaendelea katika maisha ya Mkristo mpya.

Ushawishi wa upotovu wa kurithi katika maisha ya Mkristo unadhihirika kwa njia kadhaa.

1. Mkristo mpya wakati mwingine atapambana na nia yake mwenyewe wakati wa majaribu.
2. Mkristo mpya atahisi nia mbaya ambazo lazima azipinge.
3. Mkristo mpya atakuwa na miitikio na mitazamo mibaya ambayo yatatokea kabla hajaitambua.

Mkristo mpya lazima atiwe moyo ili asiache imani yake kwa sababu anahisi kwamba angali ana msukumo wa kutenda dhambi. Anapaswa kuendelea kutafuta nguvu na mabadiliko yanayotimizwa na Roho wa Mungu.

Mchungaji lazima awe na subira na Wakristo wapya. Ni lazima atambue kwamba hawatakuwa Wakristo thabiti katika yote wanayosema na kufanya. Huenda wasione mapungufu yao mara moja.

## UKIUKAJI USIOKUWA WA MAKUSUDI

Wakati mwingine kwa bahati mbaya au kutojua mtu **anakiuka Neno la Mungu bila kukusudia**. Katika Mambo ya Walawi 4:2-3, tunaona kwamba katika hali hiyo, mtu alihitaji kutoa dhabihu mara tu baada ya kutambua kwamba amefanya makosa. Kwa sababu kifo cha Kristo kinachukua nafasi ya dhabihu zote za Agano la Kale, tunajua kwamba Wakristo wamekombolewa kutokana na ukiukaji usio wa makusudi.

Ukiukaji usiokuwa wa makusudi hauepukiki mradi uelewa wetu ni mdogo. Hauvunji uhusiano wetu na Mungu kwa sababu haupingani na upendo wetu kwa Mungu. Mungu alisema kwamba kumpenda kikamilifu kunatimiza yale anayotaka tufanye. (Soma Mathayo 22:37-40; Warumi 13:8-10.) Hatuwajibiki juu ya mambo ambayo hatuyajui. (Soma Yakobo 4:17.)

Kadiri tunavyoenenda katika nuru (kuishi kulingana na ukweli tunaoujua), tunatakaswa kutokana na dhambi zote. (Soma 1 Yohana 1:7.) Hatuhitaji kuogopa kwamba ukiukaji usiokuwa wa makusudi utavunja uhusiano wetu na Mungu, kwa sababu tunatumainia upatanisho wa Kristo.

> **“Ukuu katika ufalme wa Mungu unapimwa kwa misingi ya utiifu.”**
>
> **John Stott**

Kitabu cha Mambo ya Walawi kinaonyesha kwamba tunapotambua kwamba tumefanya makosa bila kukusudia tunapaswa kutubu, kumwomba Mungu msamaha, na kurekebisha maisha yetu yawe jinsi Mungu anavyotaka.

Kadiri tunavyojifunza Neno la Mungu, kumfuata Roho Mtakatifu, kuwa na ushirika na waumini wengine, na kukua katika ukomavu, tunapaswa kubadilisha tabia zinazotufanya tukiuke mapenzi ya Mungu bila kukusudia.

» Je, kwa nini tunapaswa kutaka kujua na kufanya mapenzi ya Mungu vizuri zaidi?

Sababu kwa nini tunapaswa kutaka kuelewa mapenzi ya Mungu vizuri zaidi na kuyafuata kikamilifu:

1. Hatutaki kufanya jambo lolote lisilompendeza Mungu.
2. Kuna matokeo mabaya ya kutenda mabaya hata kama ni bila kukusudia.
3. Tunahitaji kuwa mifano bora kama Wakristo.
4. Tukijaribu kuepuka mapenzi ya Mungu tunakuwa na hatia ya dhambi.

Kadiri tunavyokua katika kuelewa mapenzi ya Mungu, wakati mwingine tunatambua makosa katika maisha yetu. Ikiwa tunatambua kwamba jambo tunalofanya si sahihi, lakini tukachagua kulifanya hata hivyo, hilo si kosa linalotokana na kutojua tena. Tukikataa kubadilika, kosa hilo linakuwa dhambi ya makusudi.

## HITIMISHO

Wakati mwingine wanatheolojia hawatofautishi kati ya aina za dhambi. Wanaweza kusema kwamba kila kitu ambacho si kamili ni dhambi, au wanaweza kusema kwamba tendo la kukusudia tu ndio dhambi. Tukielewa aina za dhambi, tunaweza kuelewa vizuri zaidi kile ambacho Mungu anataka kutufanyia kwa neema yake.

- **Dhambi ya makusudi** inapaswa kushindwa wakati mtu anazaliwa mara ya pili. Yohana anatangaza kwamba mtu aliyezaliwa mara ya pili hatendi dhambi kwa mazoea (1 Yohana 3:4-9). Dhambi ya makusudi haiambatani na imani katika Kristo. Uasi wa makusudi si sehemu ya tabia ya muumini wa kawaida.

- Utakaso ni kazi ya Mungu ya kushughulikia **dhambi za asili ya mwanadamu**, ili waumini wawe watakatifu kabisa (1 Wathesalonike 5:23). Roho, nafsi, na miili yao yote inakuwa bila lawama. Utakaso hushinda dhambi za asili ya mwanadamu.

- **Dhambi za kutojua** si kutotii kwa makusudi, na hazitokani na asili ya dhambi, bali zinatokana na mwili na akili iliyoanguka. Hakuna uwezekano wa kukombolewa kikamilifu kutokana na aina hii ya dhambi wakati wa maisha ya hapa duniani. Wakati wa ufufuo, mtakatifu aliyetukuzwa atakuwa huru kutokana na aina zote za dhambi kikamilifu na milele.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Dhambi ya mwanadamu ilitokana na uamuzi wa hiari wa kutomtii Mungu uliofanywa na watu walioumbwa kwanza. Watu wote isipokuwa Yesu wamerithi upotovu wa Adamu na pia wana hatia ya kutenda matendo ya dhambi. Huenda makosa ya wanadamu yakakiuka sheria ya Mungu lakini hayavunji uhusiano wetu na Mungu. Kila mtenda dhambi ataadhibiwa milele ikiwa hatapata msamaha wa Mungu kabla ya hukumu ya mwisho.

## MAZOEZI YA SOMO LA 5

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Warumi 1:21-32
    - Warumi 3:10-20
    - Wagalatia 5:16-21
    - Waefeso 5:1-8
    - Tito 1:10-16
    - Yakobo 4:1-4
    - 2 Petro 2:9-17

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 5. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 5

1. Orodhesha sababu tatu kwa nini ni lazima tuelewe dhambi.

2. Je, tunajuaje kwamba dhambi haikuwa kosa la Mungu?

3. Toa ufafanuzi wa sentensi moja kwa kila moja ya yafuatayo: dhambi ya makusudi, upotovu wa kurithi, na ukiukaji usio wa makusudi.

4. Je, ni kwa nini tunapaswa kutaka kuelewa na kutekeleza mapenzi ya Mungu vizuri zaidi?

## SOMO LA 6

# ROHO

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Maelezo fulani kuhusu asili ya malaika.
    - Kuhusika kwa malaika katika maisha ya muumini.
    - Anguko la Shetani na pepo wengine wabaya.
    - Mgogoro wa kiroho uliopo katika ulimwengu wa roho.
    - Ushindi wa mwisho wa Mungu na waumini dhidi ya roho ovu.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu roho.

2. Mwanafunzi atajiepusha na kuvutiwa kwa njia mbaya na ulimwengu wa roho.

## JINSI MALAIKA WALIVYO

» Someni Mathayo 4:1-11 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu pepo waovu?

Watu wanapozungumza kuhusu malaika, mara nyingi swali la kwanza ni, "Malaika wanaonekanaje?" Wachoraji wengi wamejaribu kueleza jinsi walivyo.

» Je, malaika wanaonekanaje?

Je, malaika wana mabawa? Maserafi ambao Isaya aliwaona walikuwa na mabawa sita (Isaya 6:2). Sanamu ya makerubi ambayo Mungu alimwambia Musa aweke juu ya Sanduku la Agano ilikuwa na mabawa (Kutoka 25:20). Makerubi ambao Ezekieli aliwaona walikuwa na mabawa manne (Ezekieli 1:6, Ezekieli 10:15).

Hatujui kwamba malaika kwa ujumla wana mabawa. Kwa ujumla hawahitaji mabawa ili kusafiri, kwa sababu wao ni roho na husafiri kwa kasi kubwa zaidi kuliko kuruka kwa mabawa. Kama roho, pia hawana miili ya nyama. Kwa malaika, mabawa kawaida si lazima.

Kinyume na michoro mingi tunayoona, Biblia haisemi kuwa malaika wanafanana na wanawake au watoto. Wamejitokeza katika umbo la kiume, lakini hawana jinsia katika maana ya kibinadamu. Hawana uhusiano wa ndoa au mahusiano ya kifamilia. (Soma Mathayo 22:30.) Kila mmoja wao aliumbwa kibinafsi.

Malaika kwa kawaida hawaonekani na watu, lakini wanaweza kujitokeza wakati kuna kusudi la kufanya hivyo. Wakati mwingine malaika alipojitokeza, mwanzoni watu walifikiri kwamba yeye ni mtu wa kawaida (Mwanzo 19:1-2). Wakati mwingine malaika walijitokeza wakiwa na mng'ao mkubwa kiasi kwamba watu walianguka chini kwa hofu (Mathayo 28:2-4). Malaika alipomtokea mtu, kwa kawaida alimsalimu mtu huyo kwa kusema "Usiogope." (Soma Luka 1:13, 30; Luka 2:10.)

Malaika ni roho (Waebrania 1:14),[7] lakini hatupaswi kufikiria kuwa wao si viumbe halisia kwa sababu ya hilo. Biblia inadokeza kwamba roho zina nguvu zaidi kuliko kitu chochote chenye mwili unaoonekana. (Soma Isaya 31:1, 3.)

Malaika wanaitwa wana wa Mungu (Ayubu 1:6) na wana asili ya Mungu, lakini si kama ilivyo katika wanadamu. Malaika wana nguvu na akili kuliko wanadamu kwa sasa, lakini siku moja wanadamu watakuwa juu ya malaika. (Soma 1 Wakorintho 6:3.)

Uumbaji wa malaika haujatajwa katika kitabu cha Mwanzo. Waliumbwa kabla ya dunia, na walisherehekea walipomwona Mungu akiiumba (Ayubu 38:4-7).

Malaika hawafi (Luka 20:36). Ukweli kwamba waliumbwa kabla ya dunia unamaanisha kwamba malaika wote wameishi kwa maelfu ya miaka na wameona historia yote ya wanadamu.

Malaika wana nafsi. Wanaweza kusema na kuwa na mazungumzo (Luka 1:18-20). Wanamwabudu Mungu, kumaanisha kwamba wanaweza kuelewa asili yake na wanaweza kuiitikia kwa heshima kuu (Waebrania 1: 6). Wanafurahi wakati mtenda dhambi anatubu, kuonyesha kwamba wana hisia. (Soma Luka 15:10.) Wana hamu kubwa ya kuelewa mpango wa wokovu, kuonyesha kwamba wana uwezo wa kiakili. (Soma 1 Petro 1:12.) Walisherehekea tangazo la kuzaliwa kwa Yesu (Luka 2:13-14).

Malaika wote hawafanani, kwa sababu kuna wengine wanaoitwa makerubi (Zaburi 80:1) na maserafi (Isaya 6:2). Pia kuna viwango vya malaika, kwa maana Biblia inazungumza juu ya malaika aina mbili na angalau malaika mkuu mmoja na pia inataja "Ibilisi na malaika wake" (Mathayo 25:41). Kuna mfumo wa mamlaka kati ya malaika, unaojulikana kama falme, mamlaka, na enzi. (Soma Waefeso 6:12; Wakolosai 1:16.)

Katika utamaduni wa Kiyahudi na wa Kikristo mengi yameandikwa kuhusu malaika, zaidi ya kile tunachojua kutoka kwenye maandiko.

---


7 Pepo pia wanaitwa "roho" katika Mathayo 8:16, Mathayo 12:45; Matendo 19:12; na katika vifungu vingine.

Si mengi yamesemwa katika maandiko kuhusu tofauti kati ya malaika. Neno *malaika mkuu* limetumika mara mbili pekee katika Biblia. Mikaeli anaitwa malaika mkuu, na kutakuwa na sauti ya malaika mkuu wakati wa kurudi kwa Yesu (1 Wathesalonike 4:16; Yuda 1:9). Neno *malaika mkuu* kimsingi linamaanisha "mkuu wa malaika." Hatujui ni malaika wangapi wakuu waliopo.

Maserafi wametajwa katika Biblia katika Isaya 6 pekee. Wana mabawa sita. Mbali na mabawa yao, huenda ikawa walionekana kama wanadamu, kwa sababu wana mikono, miguu na nyuso.

Makerubi na upanga wa moto viliwekwa kwenye Bustani ya Edeni baada ya Adamu na Hawa kufurushwa (Mwanzo 3:24). Hilo lilikuwa ni ili kufanya bustani isiweze kufikiwa. Maelezo ya Ezekieli kuhusu makerubi aliowaona ni tofauti sana na kiumbe mwingine wowote tunaomjua. Walikuwa na mabawa manne, nyuso nne ambazo zote zilikuwa tofauti, mikono kadhaa, mng'ao kama moto, miale ya umeme, na kasi kama umeme (Ezekieli 1:5-14, Ezekieli 10:15).

Sanamu za makerubi wawili ziliwekwa kwenye ncha za Sanduku la Agano, Kiti cha Rehema kikiwa katikati yao.[8] Mungu anaitwa tena na tena Yeye aketiye juu ya makerubi.[9] Hilo lilimtambulisha kuwa Mungu wa Israeli ambaye aliabudiwa Hekaluni na pia lilionyesha kwamba hakuweza kufikiwa isipokuwa kwa njia alizoagiza.



Nguvu na ukuu wa Mungu unaonekana katika aina ya watumishi alionao. Makerubi ni viumbe ambao mtu akimwona mmoja wao atafikiri anamwona Mungu, na atataka kumwabudu, kumbe ni mtumishi wa Mungu tu.

Ukweli kwamba Mungu anahudumiwa na malaika wengi unaonyesha ukuu wake. Mtume Yohana aliona umati wa malaika uliokuwa umezunguka kiti cha enzi cha Mungu. Alisema "hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu" (Ufunuo 5:11).

Nguvu za malaika zina kikomo, kwa kuwa tunasoma kwamba malaika mmoja alicheleweshwa na mzozo alipokuwa amebeba ujumbe kwa Danieli. (Soma Danieli 10:12-13.) Hata hivyo, Mungu anaweza kuwapa nguvu nyingi kadiri wanavyohitaji kwa ajili ya kazi yoyote anayowapa, kama vile wakati ambapo malaika mmoja aliwaua wanajeshi 185,000 (2 Wafalme 19:35).

8 Picha: "Nakshi ya Sanduku la Agano", *Illustrated Bible Dictionary* (1893), imetolewa kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/File: Ark_of_the_Covenant_engraving.jpg, kikoa cha umma.

9 Kwa mfano, 2 Wafalme 19:15, 1 Mambo ya Nyakati 13:6; Isaya 37:16

Inaonekana kwamba malaika hupewa majukumu. Biblia inatuambia kwamba huwa wanatumwa kuwatumikia wale wanaopokea wokovu. (Soma Waebrania 1:14.) Malaika huwazunguka na kuwalinda watu wanaomtumikia Mungu (Zaburi 34:7). Tunaweza kuchukulia kwamba malaika wengi wako pamoja nasi wakati wote. Yesu alisema kwamba watoto wana malaika wanaowatumikia. (Soma Mathayo 18:10.) Malaika mkuu Mikaeli anaitwa jemedari mkuu anayetetea taifa la Israeli (Danieli 12:1).

Biblia haisemi kamwe kwamba tunapaswa kuomba kwa malaika. Haisemi kwamba tujaribu kuwasiliana nao. Malaika si wapatanishi kati yetu na Mungu. Kuna onyo kuhusu watu wanaoabudu malaika na kujihusisha na mambo ya ulimwengu wa roho ambayo hawayaelewi. (Soma Wakolosai 2:18.) Tukijaribu kushirikiana na malaika kwa njia ambayo Mungu hataki, kuna uwezekano kwamba roho waovu watatuitikia badala ya malaika wa Mungu.

## SHETANI NA MALAIKA WALIOANGUKA

» Je, asili ya pepo waovu ni ipi?

Pepo waovu ni malaika waliomuasi Mungu. Tukio hilo lilitokea kabla ya kuumbwa kwa wanadamu, na Biblia haisemi mengi kulihusu. Shetani alikuwa kiongozi wa uasi, na theluthi moja ya malaika walimfuata (Ufunuo 12:4). Yuda anazungumza kuhusu malaika walioacha nafasi yao ya kwanza (Yuda 1:6). Tayari wameshahukumiwa na hukumu ya Mungu. (Soma Yohana 16:11; 2 Petro 2:4.)

Kuna vifungu viwili katika vitabu vya manabii ambavyo huenda vinazungumzia anguko la Shetani (Isaya 14:12-17 na Ezekieli 28:12-19). Kila kifungu kinazungumza juu ya mfalme mwanadamu wa dunia, lakini huenda vinalinganisha anguko la wafalme na anguko la Shetani.

Inaonekana Shetani alishikwa na kiburi na alitaka kuwa huru kutokana na Mungu. Mtume Paulo alionya kwamba mtu anaweza kuwa na kiburi na kuanguka katika hukumu kama ya shetani. (Soma 1 Timotheo 3:6.) Hilo lilikuwa jaribu lile lile ambalo Ibilisi aliwatolea Adamu na Hawa aliposema, “Mtakuwa kama Mungu.” Ni jaribu la kukataa mamlaka ya Mungu na kuwa mungu wako mwenyewe.

> **“Shetani hujifanya kuwa mtawala wa moyo, macho, na ulimi wa mwenye dhambi. Hujaza moyo wake na upendo wa dhambi; hupofusha macho yake ili asione hatia na adhabu inayomngoja; na ulimi wake huuzuia kuomba.”**
>
> **Adam Clarke**
> *Christian Theology*, “Good and Bad Angels”

» Je, baadhi ya mambo tunayojua kuhusu Shetani ni yapi?

Shetani bado anaongoza uasi dhidi ya Mungu. Anaitwa mfalme wa uwezo wa anga (Waefeso 2:2). Shetani anaitwa mtawala wa ulimwengu huu kwa sababu watu wa ulimwengu huu kwa kiasi kikubwa wanamuasi Mungu (Yohana 12:31). Anadai umiliki wa falme za ulimwengu, akizitoa kwa muda mfupi kwa yeyote anayetaka (Luka 4:4-6). Anapofusha akili za wenye dhambi ili kuwazuia wasikubali injili. (Soma 2 Wakorintho 4:4.) Wenye dhambi ambao hawajatubu hakika ni wafungwa wake (2 Timotheo 2:26). Anaondoa Neno la Mungu kutoka kwenye akili za watu ili lisiwe na ushawishi wowote maishani mwao. (Soma Marko 4:15.) Aliweka ndani ya mioyo ya Anania na Safira mpango wa kudanganya kanisa na Roho Mtakatifu (Matendo 5:3), na alimpa Yuda nia ya kumsaliti Yesu (Luka 22:3). Anabuni kanuni potovu za kidini na kuwahimiza watu wazifundishe. (Soma 1 Timotheo 4:1.)

Shetani anamchukia Mungu na kwa hivyo anawachukia watu kwa sababu wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wanapata kibali kikuu zaidi cha Mungu. Anatafuta kuwaleta watu wengi iwezekanavyo chini ya hukumu ile ile ambayo amepokea kwa kuwashawishi wamuasi Mungu.

Wale wanaomtumikia Shetani kwa kudhamiria ndio watu waliodanganyika zaidi ulimwenguni, kwa kuwa wako katika uasi usioweza kufanikiwa, na wanamtumikia bwana ambaye anawachukia na nia yake ni kuwaangamiza tu (1 Petro 5:8). Anatoa ahadi ambazo anajua hawezi kuzitimiza (Yohana 8:44).

Wengine wanamfuata Shetani pasipo kudhamiria wanapochagua kuishi katika dhambi (Waefeso 2:2-3). Ndio maana anatumia muda na nguvu nyingi katika majaribu na udanganyifu (2 Wakorintho 4:4, 2 Wakorintho 11:3, 14). Anataka kuwafanya watu wakatae kuweka imani katika Mungu, wakifanya vitu vilivyoumbwa kuwa sanamu zao badala ya kumwabudu Mungu (Warumi 1:25). Majaribu yake ni udanganyifu, kwa sababu hana chochote cha kutoa isipokuwa kupotosha kile ambacho Mungu ameumba. Ibilisi hajaumba furaha wala raha; Mungu aliumba yote hayo. Ibilisi anaweza tu kutoa raha kwa njia potovu ambazo ziko nje ya mapenzi ya Mungu. Kwa kweli, Shetani hawezi kuumba chochote; anaweza tu kupotosha vitu vizuri ambavyo Mungu ameumba.

Inaonekana kwamba pepo fulani waovu hulenga maeneo mahususi ya kijiografia au vikundi vya watu. Kama vile malaika Mikaeli alivyoitwa jemedari mkuu anayelinda Israeli, kulikuwa na roho waovu walioitwa wakuu wa Uajemi na Uyunani (Danieli 10:13, 20). Roho fulani zikawa miungu ya mataifa fulani.

Shetani anatamani kuabudiwa. (Soma Mathayo 4:9.) Roho waovu hufanya kazi kupitia dini za uongo. Biblia inatuambia kwamba watu wanapoabudu sanamu wanaabudu pepo. (soma Kumbukumbu la Torati 32:17; 1 Wakorintho 10:20-21.) Pepo huitikia ibada ya watu wasiojua kile wanachoabudu. Kama vile mwabudu Mungu anavyokuwa zaidi kama Mungu na kufurahia utakatifu, mwabudu pepo waovu anakuwa mwovu zaidi na kufurahia maovu. Labda ibada mbaya zaidi ambayo imewahi kutokea ni wakati watu walipotoa watoto wao wenyewe kuwa dhabihu kwa roho waovu. (Soma Zaburi 106:37-38.)

Shetani na roho waovu wengine hujaribu kuchukua udhibiti wa akili na tabia za watu kikamilifu. Hilo linaitwa "kupagawa na pepo." Baadhi ya watu wamejitoa wenyewe kwa kudhamiria kwa aina hiyo ya kupagawa; pengine wengine wameruhusu hali hiyo bila kujua walichokuwa wakifanya. Watu wengine wameingia hatua kwa hatua katika hali hiyo, wakifikiri kwamba wanapata nguvu za kutumia kwa malengo yao wenyewe. Mtu aliyepagawa kwa namna hiyo anakuwa mtumwa wa pepo waovu, anasukumwa kwenye maangamizi yake mwenyewe, na kuteseka vibaya sana kiakili na kihisia. (Soma Marko 5:2-5.) Ni Yesu pekee ndiye anayeweza kumkomboa mtu kutoka katika utumwa huo.

## USHINDI WA MUNGU

Katika nchi ambazo injili imehubiriwa sana, kazi ya pepo waovu kwa kawaida huwa imefichika. Kinyume na matarajio, ni katika nchi hizi "zilizostaarabika" ndiko watu hawazingatii dini kwa kiasi kikubwa, wakikejeli kitu chochote kisicho cha kawaida na kukana uwepo wa roho. Katika mazingira kama hayo, pepo wabaya hawafanyi kazi waziwazi, kwa sababu wakiwatia hofu watu ambao wamesikia injili, wengi wa watu hao watamgeukia Mungu kwa ajili ya ukombozi na ulinzi.

Katika nchi ambapo injili haijulikani sana, pepo wabaya hufanya kazi kwa uwazi zaidi. Watu walio katika nchi hizo hawajui kwamba wanaweza kumgeukia Kristo kwa ajili ya ukombozi, kwa hivyo nguvu za pepo huwatishia na kuwafanya wanyenyekee. Watu hao hutumikia roho, si kwa hiari wala kwa furaha, bali kwa hofu. Injili huja kwao kama ujumbe wa ajabu wa ukombozi na uhuru.

Kwa sababu ya mashambulizi ya ibilisi ya mara kwa mara, tuko katika vita vya kiroho. Tunaonywa kwamba tukumbuke vita vyetu ni katika ulimwengu wa roho na si dhidi ya maadui wa kimwili. (Soma Waefeso 6:12.) Tunaambiwa tujivike silaha za kiroho, ili tuweze kujilinda (Waefeso 6:13). Tunaweza kuwa na uhakika kwamba tutapata ushindi, kwa sababu ibilisi hawezi kupinga nguvu za Mungu zilizo ndani yetu, na tunapompinga ibilisi, atatukimbia (Yakobo 4:7).

> **"Ibilisi hawezi kukushinda ukiendelea kumpinga. Ingawa yeye ni mwenye nguvu, Mungu hamruhusu kamwe kumshinda mtu anayeendelea kumpinga. Hawezi kulazimisha nia ya mwanadamu."**
>
> **Adam Clarke**
>
> *Christian Theology*, "Good and Bad Angels"

» Je, ibilisi ni kinyume cha Mungu?

Ibilisi ana nguvu zaidi ya zile walizo nazo wanadamu katika hali yao ya sasa wakiwa na miili inayoweza kufa. Hata hivyo, nguvu zake si kitu zikilinganishwa na za Mungu. Hapaswi kufikiriwa kuwa kinyume cha Mungu, kana kwamba ana nguvu sawa na Mungu.

Wanafalsafa wengine wanafikiri kwamba nguvu za mema na mabaya duniani ziko sawa. Hiyo si kweli kabisa. Shetani hayuko kila mahali, si mjua yote, na hufanya makosa. Mungu ndiye Muumba wa roho, na haziwezi kumshinda. Kipindi cha majaribio ya mwanadamu kitakapokamilika, pepo wote waovu watahukumiwa, kufungiwa, na kuadhibiwa, pamoja na wenye dhambi.

Kushindwa kwa Shetani kuliahidiwa zamani sana. Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kuponda kichwa cha nyoka (Mwanzo 3:15). Yesu alikuja kuharibu kazi za ibilisi na kutupa ushindi dhidi ya dhambi. (Soma 1 Yohana 3:8.) Yesu, kwa kifo na ufufuo wake, hamruhusu Shetani kuwa na nguvu dhidi ya mauti (Waebrania 2:14; Ufunuo 1:18). Hatima ya mwisho na ya milele ya Shetani na pepo wengine waovu ni ziwa la moto. (Soma Mathayo 25:41.)

Tayari Mungu ameweka mipaka katika kile ambacho Shetani anaweza kufanya (Ayubu 1:12, Ayubu 2:6). Hilo linamaanisha kwamba hatuhitaji kuishi tukiogopa yale ambayo Shetani anaweza kutufanyia. Hakuna kinachoweza kutokea isipokuwa Mungu akiruhusu, na anajua kile tunachoweza kustahimili (1 Wakorintho 10:13).

Hatujalindwa tu dhidi ya mashambulizi ya Shetani, bali pia tuna uwezo wa kuendeleza ufalme wa Mungu dhidi ya ufalme wa Shetani. Yesu aliwapa wanafunzi wake nguvu, si mitume tu, kuwafukuza pepo waovu. (Soma Luka 10:17.) Kadiri tunavyohubiri injili, Mungu anaupatia nguvu ukweli wake, na kuwakomboa kutokana na Shetani wale wanaoitikia injili.

## MAKOSA YA KUEPUKA: KUVUTIWA NA ULIMWENGU WA ROHO KWA NJIA MBAYA

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshirika wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Watu wengine huvutiwa na ulimwengu wa roho. Wanaanza kusoma kuhusu malaika na wanaweza kujaribu kuingiliana nao. Biblia haisemi kamwe tuombe kwa malaika au tujaribu kuwa na uhusiano nao. Biblia inatuonya tusiwaabudu au kujaribu kujua zaidi ya kile tunachoweza kuelewa (Wakolosai 2:18).

Ni hatari zaidi ikiwa mtu atavutiwa sana na roho waovu. Watu wengine huvutiwa na nguvu zao na mambo wanayofanya. Kuna michezo inayoingiliana na roho waovu. Kuna njia ambazo watu hutumia kupata habari kutoka kwa roho waovu. Hatupaswi kamwe kujihusisha na roho waovu isipokuwa kuwapinga kwa nguvu za Mungu (Yakobo 4:7, 1 Petro 5:8-9).

Baadhi ya watu wamebuni maelezo tata na ya kina kuhusu ulimwengu wa roho na jinsi unavyofanya kazi. Hata hivyo, Mungu amefunua katika Biblia yote tunayohitaji kujua kuhusu ulimwengu wa roho.

- » Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Mungu aliumba roho wote. Malaika watakatifu wanamwabudu Mungu na kuwalinda waumini. Malaika ni viumbe wasioweza kufa, ambao wanaweza kuzungumza, kuabudu, na kutumia mantiki. Wamewahi kufanya maamuzi ya kimaadili. Shetani na malaika wengine walianguka katika dhambi na ni maadui wa Mungu na wanadamu. Mungu amewekea nguvu za Shetani mipaka na amemhukumu adhabu ya milele.

## MAZOEZI YA SOMO LA 6

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Mathayo 12:43-45
    - Luka 8:27-35
    - Matendo 12:7-11
    - 2 Wakorintho 11:13-15
    - 1 Petro 5:8-9

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 6. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 6

**1.** Je, tunajuaje kwamba malaika kwa kawaida hawana miili ya nyama?

**2.** Je, malaika waliumbwa wakati gani?

**3.** Je, malaika hufa?

**4.** Taja njia nne zinazotufanya tujue kuwa malaika wana nafsi.

**5.** Taja maneno manne yanayotumiwa katika Biblia kurejelea malaika.

**6.** Je, ni jambo gani ambalo malaika huwafanyia watu wanaomtumikia Mungu?

**7.** Je, asili ya pepo waovu ni ipi?

**8.** Je, mwabudu sanamu anaabudu nini hasa?

**9.** Je, hatima ya mwisho ya Shetani na pepo wengine waovu ni ipi?

**10.** Je, waumini wanapaswa kufanya nini ili kujilinda kutokana na mashambulizi ya kiroho?

# SOMO LA 7

# KRISTO

## MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:
    - Inamaanisha nini kwamba Yesu ni Masihi.
    - Kauli ya imani iliyo katika kirai “Bwana Yesu Kristo.”
    - Ushahidi na umuhimu wa ubinadamu wa Yesu.
    - Ushahidi na umuhimu wa uungu wa Yesu.
    - Utoshelevu wa kifo cha Kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi.
    - Umuhimu wa ufufuo kwa imani ya Kikristo.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu Kristo.
2. Mwanafunzi atajifunza yale ambayo watu wa dini nyingine husema kuhusu Kristo.

## UTANGULIZI

» Someni Ufunuo 5:11-14 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu Yesu?

## MAKRISTO WA UONGO

Biblia inatabiri kwamba katika siku za mwisho, makristo wa uongo na manabii wa uongo watadanganya wengi. Watu wengi wanaweka imani yao katika makristo wa uongo au wa kjibunia ambao hawawezi kuwaokoa. Huenda ukakutana na wawili kati ya makristo hao wa uongo, waliotambulishwa kwako na Wamormoni na Mashahidi wa Yehova.

### Yesu wa Wamormoni

Ikiwa Mormoni atabisha hodi kwenye mlango wako, atamletea Yesu ambaye ni ndugu wa kiroho wa Lusifa. Wamormoni wanafundisha kwamba huyu Yesu ni mmoja wa mabilioni

ya watoto wa kiroho ambao “Baba yetu wa Mbinguni” na “Mama yetu wa Mbinguni” waliwaleta katika ulimwengu huu. Kulingana na Wamormoni, Yesu alipoishi duniani, alikuwa na wake kadhaa, mmoja wao akiwa Maria Magdalene. Baada ya kifo na ufufuo wake, alienda Amerika kuwahubiria Wenyeji wa Amerika.

### Yesu wa Mashahidi wa Yehova

Mashahidi wa Yehova watakuambia kwamba Yesu ni Malaika Mkuu Mikaeli, kiumbe wa kwanza aliyeumbwa, ambaye alifanywa akawa mwanadamu na akafa kwenye nguzo badala ya msalaba. Alifufuliwa kama kiumbe wa kiroho, akawa Malaika Mkuu Mikaeli tena, huku mwili wake ukiyeyushwa na kuwa gesi.

## YESU WA KWELI

Nina hakika unatambua kwamba madhehebu haya potovu yana Yesu ambaye ni tofauti na Yesu wa Biblia, lakini, je, unaweza kueleza jinsi Yesu wa kweli, wa Biblia, alivyo? Mamilioni ya watu wana dhana ya kiakili ya Kristo wa uongo, ambaye hawezi kuwaokoa.

Ni muhimu kwako kuwa na uhakika na yale unayoamini juu ya Yesu ili usidanganywe, na hivyo unaweza kumtambulisha kwa wengine.

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Kwa habari zaidi kuhusu kile ambacho dini zingine zinafundisha kuhusu Yesu, tazama sehemu iliyo mwishoni mwa somo hili yenye kichwa “Kile Ambacho Dini Zingine Zinasema.”*

### Yesu Masihi

» Je, baadhi ya tabiri za Biblia kuhusu Masihi ni zipi?

Injili nne zinamwonyesha Yesu kama Masihi aliyetarajiwa wa Israeli. Mambo kadhaa yalitabiriwa kuhusu Masihi. Atakuwa mzao wa Mfalme Daudi na hivyo atastahili kuwa mfalme. Atawaokoa watu wake kutokana na ukandamizaji na utumwa. Atatiwa mafuta maalum na Mungu ili kutimiza utume wake. Neno *Masihi* linamaanisha “Mtiwa-Mafuta” ambalo lilikuwa jina la heshima la wafalme katika nchi ya Israeli.

Baadhi ya maelezo muhimu zaidi kuhusu Masihi katika Agano la Kale hayakuelezwa kwa uwazi hadi wakati Agano Jipya lilipoandikwa. Kipaumbele chake kilikuwa kuwakomboa watu wake kutokana na dhambi. (Soma Mathayo 1:21; Luka 1:74-75.) Ufalme wake haukuwa wa kidunia, bali wa kiroho na wa mbinguni (soma Yohana 18:36), Hata hivyo, hatimaye ufalme wake utaenea katika dunia yote (Wafilipi 2:10-11; Ufunuo 19:11-16; Ufunuo 20:6).

Neno *Masihi* ni neno la Kiebrania. Neno la Kigiriki lenye maana sawa ni *Christos*, ambalo linatupatia neno *Kristo.* Kutumia kirai “Yesu Kristo” ni kusema kwamba Yesu ndiye Masihi.

## Yesu ni Bwana

Kanisa la awali lilitumia neno *Bwana* kumaanisha kwamba Yesu ndiye mwenye mamlaka makuu zaidi ambaye mtu lazima ajinyenyekeze kwake. Waliposema "Yesu ni Bwana," walikuwa wakimaanisha kwamba yeye ni Bwana wa wote, Muumba na Mungu wa ulimwengu wote. Kauli hii ya imani iliwatofautisha Wakristo na wengine, kwa sababu ni Wakristo pekee ndio walioamini kwamba mwanadamu Yesu ambaye alitembea duniani pia ndiye Mungu mmoja juu ya wote.

Maneno "Bwana Yesu Kristo" yanatoa kauli kuu. Yanasema kwamba Yesu ndiye Masihi na kwamba yeye pia ni Mungu. Maneno yote matatu yako katika Wafilipi 2:10-11. Kifungu hicho kinatuambia kwamba wakati utafika ambapo kila mtu ulimwenguni atalazimika kukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana.

## Siku Tatu Maalum

Kanuni zetu za msingi kuhusu Yesu zinaweza kugawanywa katika vikundi vitatu, vinavyohusiana na siku tatu maalum.

> **"Nasadiki...**
> **kwa Bwana mmoja**
> **Yesu Kristo,**
> **mwana wa pekee**
> **wa Mungu;**
> **aliyezaliwa kwa Baba**
> **tangu milele yote,**
> **Mungu aliyetoka**
> **kwa Mungu, mwanga**
> **kwa mwanga,**
> **Mungu kweli kwa**
> **Mungu kweli,**
> **aliyezaliwa bila kuumbwa;**
> **mwenye umungu mmoja**
> **na Baba; ambaye vitu**
> **vyote vimeumbwa naye."**
>
> Kanuni ya Imani ya Nisea

## TUNASHEREHEKEA KRISMASI KWA SABABU YA UMWILISHO

Krismasi husherehekea kuzaliwa kwa Yesu na mama bikira, kwa maana Yesu alichukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. (Soma Luka 1:34-35.) Ingawa Yesu alikuwa mwanadamu kwa sababu alizaliwa na mwanamke, yeye pia ni Mungu mwenyewe, Muumba wa ulimwengu alioingia. Hili ni jambo la ajabu lakini ni kweli: Yesu alipokuwa mtoto, mama yake Maria alimshika yule ambaye alimuumba.

Neno *wana wa Mungu* linatumika kwa waumini na malaika (Yohana 1:12; Ayubu 1:6), lakini Yesu ni Mwana wa Mungu kwa njia ya kipekee (Yohana 3:16). Yeye ndiye kiumbe pekee aliye na asili kama ya Baba kikamilifu. Yeye ni mfano kamili wa Baba kiasi kwamba yeye ni Mungu kama vile Baba alivyo. (Soma Waebrania 1:2-3.)

Asili ya Mungu na asili ya mwanadamu zilikuja pamoja katika nafsi ya Yesu. Huu unaitwa *umwilisho*, ambayo inamaanisha Mungu kuchukua mwili wa mwanadamu, na kuwa

mwanadamu. Yesu pekee ndiye angeweza kuwa Mwokozi wetu kwa sababu yeye ndiye mtu pekee katika ulimwengu ambaye ni mwanadamu na Mungu.

## Yesu ni Mwanadamu

Si vigumu kumtambua Yesu wa Agano Jipya kama mwanadamu halisi. Alitungwa mimba katika tumbo la mama, akakua, akajifunza, na akakomaa kama mtu. (Soma Luka 2:52.) Alichoka, alilala, alijaribiwa, na alifanya karibu kila kitu ambacho wanadamu hufanya, isipokuwa dhambi (Waebrania 4:14-15). Hata alikufa. Kwa kweli alijitambulisha na jamii ya wanadamu kwa kuwa mmoja wetu. (Soma Yohana 1:14.)

» Je, kwa nini ni muhimu kwamba Yesu ni mwanadamu?

Kwa sababu Yesu ni mwanadamu:

1. **Angeweza kuteseka na kufa kama dhabihu** (Waefeso 5:2, Waebrania 7:26-27). Ikiwa angekuwa Mungu lakini si mwanadamu, hangeweza kuteseka kimwili na kufa.

2. **Haki yake inaweza kutufanya tuwe wenye haki na kutupa uzima.** Adamu wa kwanza aliwakilisha wanadamu wote alipofanya dhambi na kutenganishwa na Mungu. Tukio hilo ilileta mauti kwa watu wote. Yesu aliishi maisha yasiyo na dhambi na alitimiza matakwa yote ya Mungu. Anawapa uzima wa milele wote wanaojitambulisha naye. Anaitwa Adamu wa mwisho katika maandiko (1 Wakorintho 15:22, 45-49; Warumi 5:17-19).

3. **Anaweza kuwa kuhani wetu anayetuwakilisha mbele za Mungu.** Akiwa mpatanishi wetu, hazungumzi tu kwa niaba yetu, bali pia anatuwakilisha kikweli. Ilikuwa ni lazima kwake kuwa mwanadamu ili kuleta upatanisho kati yetu na Mungu. (Waebrania 2:17.) Jukumu lake kama kuhani linatoa wokovu wa milele (Waebrania 5:9, Waebrania 10:5-7). Ubinadamu wa Yesu ni sehemu muhimu ya injili. (Soma 1 Yohana 5:1.)

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Kwa ushahidi zaidi wa Biblia kwamba Yesu alikuwa mwanadamu, tazama sehemu ya "Uthibitisho wa Kimaandiko wa Ubinadamu wa Yesu" mwishoni mwa somo hili.*

## Yesu ni Mungu

### Yesu alidai kuwa Mungu.

Yesu wa Biblia ni mwanadamu lakini si mwanadamu tu. Yeye pia ndiye Mungu mmoja asiye na kikomo wa ulimwengu. Yesu alitoa dai hili mwenyewe. Alisema, "Mimi na Baba tu umoja" (Yohana

> **"Kama vile Baba anavyotumia usemi huu MIMI NIKO, Kristo pia anautumia, kwani unamaanisha uwepo unaoendelea, usiyoathiriwa na wakati."**
>
> **John Chrysostom**

10:30). Aliposema hivyo, Wayahudi walianza kumpiga mawe kwa sababu walielewa kuwa alisema kwamba yeye ni sawa na Mungu. Je, Yesu aliwaambia, "Hapana, hamkunielewa. Mimi si Mungu kikweli!"? Hapana, Yesu alikubali ufasiri wao wa maneno yake. Alifundisha kwamba alikuwa sawa na Mungu Baba.

Yesu aliposema, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO," (Yohana 8:58) alikuwa anadai kuwa yeye ni MIMI NIKO wa Kutoka 3:14, Mungu wa ulimwengu ambaye hakuumbwa. Wayahudi walijaribu kumpiga mawe kwa sababu ya dai hilo pia (Yohana 8:59).

### Yesu alifanya matendo ya kiungu alipokuwa duniani.

Yesu alifanya matendo ya kiungu alipokuwa duniani. Alitoa uzima wa milele. (Soma Yohana 10:28.) Alisamehe dhambi (Marko 2:10). Haya ni mambo ambayo Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya.

Yesu aliposamehe dhambi za yule mtu aliyepooza, alimponya mtu huyo ili kuthibitisha kwamba alikuwa na mamlaka duniani ya kusamehe dhambi (Marko 2:5, 10-12). Tendo moja lilikuwa thibitisho la lingine, likionyesha wazi kwamba Yesu hakuwa amefanya muujiza wa uponyaji kama tu nabii aliyetiwa mafuta na Mungu. Yesu alikuwa na mamlaka na uwezo wa kiungu wa kusamehe na kuponya pia.

Yesu pia alimfufua Lazaro baada ya kusema, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima" (Yohana 11:25). Hili lilikuwa ni tendo lingine la kiungu lililoambatana na dai la kiungu. Mungu pekee ndiye anayeweza kudai kwa haki kuwa yeye ndiye Ufufuo kwa sababu ni nguvu ya Mungu pekee ndio inayoweza kumfufua mtu kutoka kwa wafu. Yesu alidai kuwa mwenye kutoa Uhai kisha akampa Lazaro uhai, akionyesha kwamba yeye ni Mungu kama alivyodai. Katika tukio hili, Yesu alijitofautisha kwa uwazi na manabii wengine na mitume waliofufua watu kutoka kwa wafu kwa uwezo wa Mungu. Hakuna hata mmoja wao aliyedai kuwa na uwezo ndani yake mwenyewe wa kufanya miujiza. Walikuwa tu vyombo vya Mungu. Katika Yohana 5:21, Yesu alisema kwamba yeye huwafufua wafu kama vile Baba huwafufua wafu.

Yesu alipofanya miujiza yake, alidhihirisha utukufu wake, (Yohana 2:11) utukufu wa Mwana pekee aliyetoka kwa Baba, amejaa neema na ukweli (Yohana 1:14). Miujiza hiyo ilikuwa madhihirisho ya nguvu tukufu za Mungu Mwana, ikithibitisha kwamba alikuwa na asili ya uungu.

### Yesu ni Muumba na Mhimili.

Kulingana na Mitume Yohana na Paulo, Yesu aliumba kila kitu na anashikilia kila kitu pamoja, na kila kitu kipo kwa ajili yake. (Soma Yohana 1:3; Wakolosai 1:17.) Hakika hayo hayangeweza kusemwa juu ya yeyote ila Mungu.

- » Je, kwa nini ni muhimu kwetu kujua kwamba Yesu ni Mungu?

Kwa sababu Yesu ni Mungu,

1. Kifo chake kama dhabihu kina thamani isiyo na kikomo — kimetosha kwa ajili ya msamaha wa dhambi za ulimwengu (1 Yohana 2:2).

2. Ana uwezo wa kutuokoa; yeye ndiye njia, kweli na uzima (Yohana 14:6).

3. Ni lazima tumwabudu kama tunavyomwabudu Baba (Soma Yohana 5:23).

Tukikosa kumwona Yesu kama Mungu, hatutamheshimu kama Mungu. Hatuwezi kuokolewa ikiwa hatuheshimu Baba na Mwana kama Mungu.

Msingi wa Ukristo si mafundisho na matendo ya Yesu pekee, bali pia nafsi ya kipekee ya Yesu. Yeye si tu mwalimu wa ujumbe wa wokovu. Yeye mwenyewe ndiye Mwokozi, na ni yeye tu—Mungu-mwanadamu— ndiye angeweza kuwa Mwokozi.

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Kwa ushahidi zaidi wa Biblia kwamba Yesu ni Mungu, tazama sehemu ya "Uthibitisho wa Kimaandiko wa Uungu wa Yesu" mwishoni mwa somo hili.*

## Yesu ni Nafsi Moja

Ingawa Yesu ana asili yote ya Mungu na asili yote ya mwanadamu, yeye si nafsi mbili zilizowekwa pamoja. Asili hizo mbili zinaunda nafsi moja ndani yake, zikiwa na upatano kamili. Yesu ndiye Mungu-mwanadamu mmoja, na kila tendo la Yesu linapaswa kueleweka kwa mtazamo wa ubinadamu wake kamili na uungu wake kamili. Kanisa siku zote limefundisha kwamba asili mbili ndani ya Yesu haziwezi kutenganishwa, hata hivyo hazijachanganyika kwa njia ambayo inasababisha asili yoyote ipoteze sifa zake.[10]

Huenda ikasaidia kulinganisha asili ya Yesu na asili ya Maandiko Matakatifu. Kama Yesu, Biblia ni ya kiungu kikamilifu na ni ya kibinadamu kikamilifu. Kikiwa kitabu cha kibinadamu, kina sifa za kitabu chochote kingine cha kibinadamu, isipokuwa haina makosa. Kwa kuwa ni ya kitabu cha kiungu, kinaonyesha sifa ambazo hakuna kitabu kingine kinaweza kuonyesha. Vivyo hivyo, Yesu anaonyesha sifa za kibinadamu na za kiungu. Ukweli kwamba Biblia inaonyesha sifa za kiungu hauondoi sifa yake kama kitabu cha kibinadamu. Vivyo hivyo, ukweli kwamba Yesu anafanya kazi katika uungu wake hauondoi ubinadamu wake. Na ukweli kwamba Yesu anafanya kazi katika ubinadamu wake hauondoi uungu wake.

## Makosa ya Kikanuni Yanayojitokeza Sana

Makosa ya kikanuni yanayofanywa sana na watu wanapozungumza kuhusu Kristo ni haya:

---

10 Kanuni ya Imani ya Chalsedonia (451 B.K.), ambayo imejumuishwa katika Somo la 15, inasema kwamba asili mbili za Kristo hazibadiliki, hazigawanyiki, hazitenganishwi, na hazina mkanganyo.

- Kukana kwamba Yesu ni Mungu
- Kukana kwamba Yesu ni mwanadamu
- Kupunguza uungu wake au ubinadamu wake kana kwamba si muhimu
- Kuukana umoja wa nafsi ya Kristo

Yoyote kati ya makosa haya ni kuukana umwilisho. Umwilisho ulihitajika kwa ajili ya wokovu wetu, hivyo ikiwa mtu anakana umwilisho ataamini injili ya uongo na njia ya uongo ya wokovu.

## KILE AMBACHO DINI ZINGINE ZINASEMA

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshiriki wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Mashahidi wa Yehova wanasema kwamba Yesu alikuwa mwanadamu. Wanaamini kwamba alikuwa mtu mkuu zaidi aliyewahi kuishi, lakini bado ni mwanadamu tu. Ndio maana hawaamini kwamba kifo chake ni dhabihu tosha kwa ajili ya wokovu wetu. Wana injili ya wokovu kwa matendo. Wanadai kuwa Wakristo, lakini wao ni dini tofauti.

Wamormoni wanaamini kwamba Yesu awali alikuwa roho aliyeumbwa na Mungu, kama ndugu wa Lusifa. Alitumwa ili azaliwe duniani akiwa mwanadamu Yesu. Wamormoni hawaamini kwamba Yesu ni Mungu.

Waislamu wanaamini kwamba Yesu alikuwa nabii aliyetumwa na Mungu. Hawaamini kwamba yeye ni Mungu au kwamba kuna Utatu wa Mungu. Hawaamini kwamba alisulubiwa au alifufuka kutoka kwa wafu.

Wahindu na Wabudha wanaamini kwamba Yesu alikuwa mtu mtakatifu ambaye alifanya miujiza. Hana umuhimu katika dini zao. Hawamwamini Mungu ambaye ni Muumba na Bwana, kwa hivyo hawaamini kwamba Yesu ni umwilisho wa Mungu.

## TUNASHEHEREKEA IJUMAA KUU KWA SABABU YA UPATANISHO

Ijumaa Kuu ni siku ambapo Yesu alisulubiwa. Katika siku hii ya kuogofya na ya ajabu, Yesu alipeleka dhambi zetu msalabani. Alikufa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu ili sisi tupate kusamehewa.

### Dhabihu Ilihitajika

Dhabihu ilihitaji kutolewa ili Mungu aweze kutusamehe na bado abaki kuwa mwenye kuzingatia haki na mtakatifu. Kanuni hii ilifundishwa katika Agano la Kale kupitia dhabihu ambazo Mungu alihitaji (Waebrania 9:22). Ikiwa Mungu angesamehe tu dhambi bila msingi wowote, hiyo ingeonyesha kwamba yeye si mwenye kuzingatia haki na kwamba dhambi si jambo zito sana. Lakini hakuna mtu angeweza kutazama kifo cha Yesu kwa kusulubiwa

na kusema kwamba dhambi si mbaya. Kujitoka kwake kama dhabihu yake kulitoa msingi wa msamaha wetu.

## Yesu Pekee Ndiye Angeweza Kuwa Dhabihu ya Kutosha

» Kwa nini Yesu pekee ndiye angeweza kuwa dhabihu ya dhambi?

Haki ya Mungu na uzito wa dhambi ulihitaji dhabihu kubwa kuliko kitu chochote kilichoumbwa. (Soma Waebrania 10:4.) Tumetenda dhambi dhidi ya Mungu asiye na kikomo, jambo linalotuletea hatia isiyo na kikomo. Ndio maana Yesu pekee ndiye angeweza kuwa dhabihu. Alistahili kwa sababu yeye ni Mungu na kwa sababu yeye ni mwanadamu. Kwa sababu ya uungu wake, hakuwa na dhambi, na kujitoa kwake kama dhabihu kulikuwa na thamani isiyo na kikomo. Kwa sababu ya ubinadamu wake, angeweza kutuwakilisha na kufa kwa niaba yetu.

## Damu ya Yesu Inawakilisha Kifo chake cha Kujitoa kama Dhabihu

Mungu aliwafundisha watu kuhusu upatanisho kwa kuanzisha utoaji dhabihu. Makuhani walichinja wanyama na kutoa damu yao kuwakilisha kifo cha wanyama hao. Kitabu cha Waebrania kinasema kwamba pasipo kumwaga damu hakuna msamaha wa dhambi (Waebrania 9:18-22).

Mungu aliwaamuru watu washughulikie damu kwa njia maalum kwa sababu iliwakilisha uhai wa kiumbe (Mambo ya Walawi 17:11, 14). Kumwaga damu kulimaanisha kuua (Mwanzo 9:5-6). Damu iliyotumika Hekaluni ilimaanisha kwamba mnyama alikuwa ameuawa.

Kifo cha Kristo kilikuwa dhabihu kuu zaidi ambayo ilifanya wokovu upatikane kwa kila mtu wakati wote. (Soma Waebrania 10:4, 12.) Aliwasilisha damu yake mbinguni ili kuwakilisha kifo chake cha kujitoa kama dhabihu. (Soma Waebrania 9:12, 24.) Damu ya Yesu, ikiwakilisha kifo chake, inatoa wokovu kwa sababu alikufa kama dhabihu ili tupate kuokolewa.

Kwa nini Yesu alikufa msalabani badala ya kufa kwa njia nyingine? Katika enzi ya Agano la Kale, mtu kutundikwa kwenye mti kulikuwa ni ishara ya laana ya Mungu (Kumbukumbu la Torati 21:23). Mtume Paulo anatuambia kwamba Yesu alijitwika laana ya Mungu kwa kusulubiwaa kwenye mti (Wagalatia 3:13).

## Yesu Alipatanisha Mungu na Mwanadamu

Yesu alikuja kupatanisha pande mbili zilizotengana — Mungu na mwanadamu. Kama mpatanishi, Yesu alipaswa kuwakilisha pande zote mbili kwa wakati mmoja. Kama Mungu, alimwakilisha Mungu kwa mwanadamu. Kama mwanadamu, alimwakilisha mwanadamu kwa Mungu. Kwa kuwakilisha pande zote mbili kikamilifu, Yesu alipatanisha mwanadamu na Mungu. Alifanya kile ambacho kila upande ulipaswa kufanya ili kuleta upatanisho.

## TUNASHEREHEKEA PASAKA KWA SABABU YA UFUFUO

Kuna njia nyingi za kitamaduni za kusherehekea Pasaka, lakini watu wengi hawatambui maana ya mambo wanayofanya, na huenda hawajui ni nini lililo muhimu kuhusu ufufuo wa Yesu. Yesu alifufuka kutoka kaburini asubuhi ya Pasaka, siku ya tatu baada ya kusulubiwa. Alionyesha kwamba ana nguvu ya kushinda dhambi, mauti na ibilisi. Hakujitwika tu kifo chetu tu, bali pia alikishinda kwa uzima. Kwa sababu alishinda, sisi pia tunaweza kushinda!

### Yesu Alifufuka Kimwili

Kuna wakati Yesu aliwaambia Wayahudi, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Ingawa Wayahudi walifikiri kwamba alikuwa akimaanisha hekalu ambalo Herode alijenga, Injili ya Yohana inaeleza kwamba Yesu alikuwa anazungumzia mwili wake (Yohana 2:19-21). Injili zote zimerekodi ukweli kwamba kaburi la Yesu lilikuwa tupu siku tatu baada ya yeye kuzikwa humo. Yesu aliwatokea wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake, akisema, "Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo" (Luka 24:39). Alikuwa anathibitisha kwamba alikuwa amefufuka kimwili kutoka kwa wafu.

» Je, ingeleta tofauti gani kama Yesu hangefufuka kutoka kwa wafu?

1. **Ufufuo wa Yesu kimwili ulionyesha ushindi wake kamili dhidi ya dhambi na mauti**. (Soma Wakolosai 2:12-15; Ufunuo 1:17-18.)

2. **Ufufuo wa Yesu kimwili ulithibitisha kwamba alikuwa kile alichodai kuwa** (Mathayo 17:22-23, Yohana 2:16-22). Hivyo, tukio hilo pia lilithibitisha injili. Watu wanaokana kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu pia wanakana injili. (Soma 1 Wakorintho 15:17.)

3. **Ufufuo wa Yesu unatuhakikishia kwamba sisi pia tutafufuliwa kutoka kwa wafu**. Yesu aliahidi kwamba atawafufua wafu. Ahadi hiyo isingeaminika isipokuwa yeye mwenyewe afufuke (Yohana 5:28-29). Tutafufuliwa kuwa na miili kama mwili wa Yesu uliotukuzwa. (Soma 1 Yohana 3:2.)

### Yesu Bado Ni mwanadamu

Ufufuo unatuonyesha kwamba umwilisho ni hali ya kudumu. Yesu daima atakuwa mwanadamu na pia Mungu. Yesu, ambaye bado ni Mungu-mwanadamu, sasa anatuombea mbele za Baba (Warumi 8:34), na siku moja atarudi kutupeleka mbinguni (1 Wathesalonike 4:16-17).

## TUNAJISALIMISHA KWA YESU KWA SABABU YA YEYE NI NANI NA KILE ALICHOFANYA

Kama waumini, tunaishi katika uhusiano wa kila siku na Kristo. Yeye si mtu wa kihistoria tu, wala si Mungu aliye mbinguni tu, bali yuko pamoja nasi. Aliahidi kuwa pamoja na wanafunzi wake daima (Mathayo 28:20).

Yuko kanisani kwa namna maalum. Yeye ndiye kichwa cha kanisa, na kanisa linaitwa mwili wake (Waefeso 1:22-23). Analiongoza kanisa, analishikilia pamoja, na kukidhi mahitaji yake. (Soma Wakolosai 2:19.)

Mtu anayekubali ukweli kuhusu Yesu anapaswa kuliitikia kwa imani na utiifu. Unaweza kuwasaidia wengine kuwa waumini kwa sala kama hii hapa chini.

> Baba, nakushukuru kwa kunipenda vya kutosha ili kumtuma Mwanao Yesu duniani kwa ajili yangu. Ninaamini kwamba Yesu ni Mungu-mwanadamu asiye na dhambi ambaye alikufa na kufufuka ili niweze kusamehewa dhambi zangu na kurejeshwa katika uhusiano na wewe. Naomba msamaha kwa dhati kwa ajili ya dhambi zote nilizotenda. Najua kwamba dhambi zangu zilimsulubisha Yesu msalabani. Sasa, ninajitenga na kila kitu ninachojua si sahihi, na ninampokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wangu. Niongoze kuanzia sasa. Nitaishi kwa ajili yako milele! Asante kwa kunisamehe. Nakupenda. Amina.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Yesu ndiye Masihi na Bwana wa wote, Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira, akiwa na asili ya kibinadamu kikamilifu na asili ya kiungu kikamilifu katika nafsi moja. Aliishi maisha yasiyo na dhambi na akafa kama dhabihu ili dhambi zetu ziweze kusamehewa. Alifufuka kutoka kwa wafu na atawafufua waumini wote atakaporudi. Ufalme wake ni wa ulimwengu wote na hauna mwisho.

## UTHIBITISHO WA KIMAANDIKO WA UBINADAMU WA YESU

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Sehemu hii na sehemu inayofuata ni za hiari. Wanafunzi wanaweza kuzizingatia ikiwa wanataka uthibitisho zaidi wa kibiblia kuhusiana na hoja hizi.*

Yesu alikuwa mzao wa Hawa (Mwanzo 3:15), mzao wa Abrahamu (Mwanzo 22:18 - linganisha na Matendo 3:25), aliyezaliwa na mwanamke (Wagalatia 4:4), aliyezaliwa na Mariamu (Mathayo 1:21 -25), aliyeitwa Mwana wa Adamu (Mathayo 13:37), na alipitia mchakato wa kawaida wa kukomaa (Luka 2:40, 52).

Aliporudi katika mji wake wa nyumbani, itikio la watu linaonyesha kwamba utoto wake ulikuwa wa kawaida (Mathayo 13:54-56).

Alikuwa na mwili ili aweze kutii jinsi mwanadamu anavyopaswa kutii (Waebrania 10:5-9); alifanyika mwili na damu (Waebrania 2:14); aliumbwa kama sisi ili apate kuteseka kama sisi (Waebrania 2:10-18); alifanywa kuwa kamili kwa njia ya mateso (Waebrania 2:9-10); na alipitia majaribu ya wanadamu (Waebrania 4:15).

Alichukua mfano wa mwanadamu (Wafilipi 2:6-8).

Alikuwa Neno la milele la Mungu na alifanyika mwili na kuishi duniani (Yohana 1:14).

Ubinadamu wa Yesu ni kauli muhimu ya imani ya Kikristo (Yohana 1:14; 1 Yohana 4:2-3).

## UTHIBITISHO WA KIMAANDIKO WA UUNGU WA YESU

Yesu anathibitishwa kuwa Mungu kwa njia tatu:

1. Anaitwa Mungu.
2. Anaonyeshwa kuwa na sifa za Mungu.
3. Anaonyeshwa katika majukumu ya Mungu.

### Yesu anaitwa Mungu

- Yohana 1:1, 14, inasema kwamba Neno la milele ni Mungu.
- Yohana 12:41 inatuambia kwamba Isaya alimwona Yesu.
- Matendo 20:28 inasema kwamba kanisa la Mungu lilinunuliwa kwa damu yake mwenyewe.
- Warumi 9:5 inasema kwamba Kristo alikuja, ambaye ni Mungu mwenye kuhimidiwa milele.
- Tito 2:13 inamtaja kuwa Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristo.
- Mathayo 1:23 (ikinukuu Isaya 7:14) inasema kwamba jina lake linamaanisha “Mungu pamoja nasi.”
- Isaya 9:6 inasema kwamba ataitwa jina lake Mungu Mwenye Nguvu.

- 1 Timotheo 3:16 inasema kwamba Mungu alidhihirishwa katika mwili, akahubiriwa katika mataifa, na akachukuliwa juu katika utukufu.
- Katika Yohana 10:30, 33, Yesu alisema kuwa yeye na Baba ni kitu kimoja.
- Katika Yohana 5:17-18, Wayahudi walijua kwamba alisema yeye ni sawa na Mungu.
- Katika Yohana 14:9 alisema, "Aliyeniona mimi amemwona Baba."
- Katika Yohana 20:28-29, Tomaso aliona majeraha yake na akasema, "Bwana wangu na Mungu wangu," kisha Yesu akawabariki wale wanaoamini.
- Katika Yohana 8:58, Yesu alijiita MIMI NIKO, na Wayahudi walijua kwamba hilo likuwa dai kuwa yeye ni Mungu.
- Katika Ufunuo 1:17, Ufunuo 2:8, na Ufunuo 22:13, Yesu alidai kuwa wa Kwanza na wa Mwisho, na Isaya 44:6 inaonyesha hilo lilikuwa jina la Mungu.
- Waebrania 1:2-3 inatuambia kwamba yeye ni mfano kamili wa Baba.
- Katika Waebrania 1:8, anaitwa Mungu.

## Yesu Ana Sifa za Mungu

**Yuko kila mahali.** Katika Mathayo 18:20, Yesu alisema kwamba yuko mahali popote ambapo waumini wawili au watatu wanakutana. Katika Mathayo 28:20, aliahidi kwamba atakuwa pamoja na waumini daima.

**Ana uwezo wote.** Waebrania 1:3 inasema kwamba ameshikilia kila kitu kwa uwezo wake. Wafilipi 3:21 inasema kwamba ameweka vitu vyote chini yake.

**Ni wa milele.** Waebrania 13:8 inatuambia kwamba yeye ni yule yule milele. Waebrania 1:12 pia inasema kwamba yeye ni yeye yule yule milele. Kifungu hiki ni nukuu ya Zaburi 102:25-27 inayozungumza kuhusu Mungu.

**Mjua yote.** Yohana 2:24-25 inatuambia kwamba anawajua watu wote, na anajua yale yaliyo mioyoni mwao. Katika Yohana 10:15, alidai kwamba anamjua Baba jinsi Baba anavyomjua.

## Yesu Ana Majukumu ya Mungu

- Yesu ndiye Muumba (Wakolosai 1:16; Waebrania 1:10).
- Yesu alisamehe dhambi (Luka 5:20-24, Luka 7:48).
- Yesu atakuwa hakimu katika hukumu ya mwisho (Mathayo 25:31-46; 2 Wakorintho 5:10).
- Yesu anaabudiwa kama Baba (Yohana 5:22-23; Waebrania 1:6; Ufunuo 5:12-13).

## MAZOEZI YA SOMO LA 7

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Marko 1:1-12
    - Yohana 5:19-26
    - Yohana 6:44-51
    - Yohana 8:51-59
    - Matendo 2:22-36
    - Ufunuo 1:12-18

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 7. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 7

1. Je, kipaumbele cha Masihi kilikuwa kipi?
2. Je, kanisa la awali lilimaanisha nini waliposema "Yesu ni Bwana"?
3. Je, ni jinsi gani Yesu ni Mwana wa pekee wa Mungu?
4. Je, umwilisho ni nini?
5. Orodhesha sababu tatu zinazofanya iwe muhimu kwamba Yesu ni mwanadamu.
6. Orodhesha sababu tatu zinazofanya iwe muhimu kwetu kujua kwamba Yesu ni Mungu.
7. Je, ni sababu gani mbili zilizofanya dhabihu ihitajike?
8. Je, kwa nini Yesu alikufa msalabani badala ya kufa kwa njia nyingine?
9. Orodhesha sababu tatu zinazofanya ufufuo wa Yesu kimwili uwe muhimu.

## SOMO LA 8

# WOKOVU

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Kwa nini msalaba ni chukizo kwa watu wengi.
    - Hali ya mwenye dhambi.
    - Umuhimu wa upatanisho kwa ajili ya msamaha.
    - Maana ya toba.
    - Vipengele vya imani inayookoa.
    - Kwa nini upatanisho unatosha kwa watu wote na dhambi zote.
    - Msingi wa uhakikisho wa kibinafsi wa wokovu.
    - Ukombozi wa uumbaji kwa ujumla.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu wokovu.

2. Mwanafunzi ataelewa kosa la dini bila toba.

## UTANGULIZI

» Someni Zaburi ya 85 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu wokovu?

## MSALABA

Ishara muhimu zaidi ya Kikristo ni msalaba. Msalaba unawakilisha tukio ambalo ni kitovu cha historia yote. Msalaba unawakilisha tofauti kati ya imani ya Kikristo na imani zingine zote.

Msalaba ni fumbo kwa watu wengi. Hawaelewi kwa nini Yesu alikufa. Hata wakisikia kwamba alikufa kwa sababu anatupenda na anataka kutuokoa, hawaelewi kwa nini hilo lilihitajika. Wanauliza, “Ikiwa Mungu alitaka kutusamehe, kwa nini hakufanya tu hivyo?”

Mkanganyiko kuhusu msalaba ulianza tangu mwanzo, wakati Wakristo wa kwanza walianza kuhubiri injili. (Soma 1 Wakorintho 1:22-23.) Wayahudi walifikiri kwamba Mungu

angejionyesha kuwa mwenye nguvu. Walifikiri wokovu waliohitaji ni ukombozi kutokana na ukandamizaji, lakini msalaba ulionekana kuonyesha udhaifu na kushindwa.

Wagiriki walifikiri kwamba Mungu angejionyesha kuwa mwenye hekima. Walifikiri wokovu waliohitaji ulikuwa ni maelezo kuhusu jinsi ya kupata kilicho bora zaidi maishani, lakini msalaba ulionekana kuwa upumbavu na kushindwa.

» Je, kwa nini baadhi ya watu wanachukizwa na msalaba?

Msalaba ni chukizo kwa watu wengi. Watu wengi wako tayari kushikilia dini. Wako tayari kuamini mambo fulani, kufuata desturi za kidini, na kupata ushauri. Lakini wanakasirishwa na wazo kwamba wao ni wenye dhambi sana kiasi kwamba msalaba ulihitajika ili wapate msamaha. Wanafikiri Mungu hapaswi kupinga matendo au tabia zao. Msalaba unawachukiza kwa sababu unamaanisha kwamba wao ni wenye dhambi wanaohitaji msamaha.

Ili kuelewa kifo cha Yesu kama dhabihu msalabani, ni lazima tuelewe kwamba hali ya mwanadamu mwenye dhambi na asili takatifu ya Mungu vilisababisha mtanziko mkubwa. Ni lazima tuelewe kwa nini upatanisho ulimfanya Mungu aweze kusamehe.

## HALI YA MWANADAMU

Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, kila mtu tayari ametenganishwa na Mungu anapozaliwa (Warumi 5:12). Hiyo ina maana kwamba kila mtu ni mbinafsi na anafuata njia zake mwenyewe.

Mara tu mtu anapoanza kufanya maamuzi, anaanza kutenda dhambi. **Kila mwenye dhambi ana hatia ya kutenda matendo mengi ya dhambi**. (Soma Warumi 3:23.)

Dhambi ni ukiukaji wa sheria ya Mungu (1 Yohana 3:4; Yakobo 2:10-11). Kwa sababu Mungu ni mwenye kuzingatia haki kikamilifu, hapuuzi dhambi, na kila mtu atahukumiwa kwa kile alichokifanya (2 Wakorintho 5:10; Ufunuo 20:12-13). Hakuna shaka yoyote kuhusu hatia ya mtu yeyote au hukumu anayostahili. Kila mtu asiyeamini tayari ameshahukumiwa. (Soma Yohana 3:18-19.)

**Mwenye dhambi ambaye hajatubu ni adui wa Mungu** (Warumi 5:10). Mwenye dhambi hawezi kuingia katika uhusiano na Mungu isipokuwa makosa yake dhidi ya Mungu yaondolewe.

> **“Jinsi mwenye dhambi anavyoweza kuhesabiwa haki mbele za Mungu ni suala muhimu kwa kila mtu, kwani hakuwezi kuwa na amani ya kweli au furaha ya kudumu wakati sisi ni maadui wa Mungu, iwe ni wakati wa sasa au katika umilele.”**
>
> **John Wesley**
> “Kuhesabiwa Haki kwa Imani”

Mwenye dhambi pia yuko katika hali inayomfanya asistahili kuwa na uhusiano na Mungu. **Mwenye dhambi amepotoka katika matamanio yake** (Waefeso 2:3). Kwa sababu yeye ni mtumwa wa dhambi, **mwenye dhambi hana uwezo wa kubadilisha hali yake**. (Soma Warumi 6:20; Warumi 7:23.)

Hivyo, mwenye dhambi anahitaji wokovu gani? Kwa sababu mwenye dhambi ana hatia, wokovu unamaanisha msamaha. Kwa sababu yeye ni adui wa Mungu, wokovu unamaanisha upatanisho. Kwa sababu amepotoka, wokovu unamaanisha utakaso. Kwa sababu hana uwezo, wokovu unamaanisha ukombozi. Hivi ni baadhi tu ya vipengele vichache vya wokovu ambavyo mwenye dhambi anahitaji.

## MTANZIKO

Watu hawangeweza kulipia gharama ya dhambi zao wenyewe. Sababu moja ni kwamba kila kitu tulicho nacho tayari ni cha Mungu. Sababu muhimu zaidi ni kwamba dhambi ni kosa dhidi ya Mungu asiye na kikomo, na wanadamu hawana kitu chochote chenye thamani isiyo na kikomo wanachoweza kutumia kulipia dhambi zao.

Hakukuwa na chochote kabisa ambacho watu wangeweza kufanya kuhusu hitaji lao; hivyo, hakuna sharti lolote lingeweza kuwekwa ambalo lingeweza kutimiza wokovu. (Soma Wagalatia 3:21.) Ikiwa watu wangeweza kutimiza wokovu wao wenyewe, Yesu asingehitaji kufa msalabani. (Soma Wagalatia 2:21.)

» Ikiwa Mungu alitaka kusamehe, kwa nini hakusamehe tu bila msalaba?

Kwa sababu Mungu ni mtakatifu na mwenye kuzingatia haki, lazima ahukumu kulingana na ukweli na haki (Warumi 2:5-6). Neno *upatanisho* linarejelea ukweli kwamba kujitoa kwa Yesu kama dhabihu ndio njia yetu ya kupatanishwa na Mungu.

Fikiria kama Yesu asingejitoa kama dhabihu. Je kama Mungu angesamehe tu dhambi bila upatanisho?

Ikiwa Mungu angesamehe dhambi bila upatanisho, ingeonekana kana kwamba dhambi si muhimu. Ingeonekana kana kwamba Mungu si mwenye kuzingatia haki, wala si mtakatifu. Ingeonekana kana kwamba machoni pa Mungu kuna tofauti ndogo kati ya mtu anayefanya mema na mtu anayefanya maovu.

Kama msamaha ungetekelezwa bila upatanisho, Mungu asingeweza kuabudiwa kama Mungu anayezingatia haki na mtakatifu jinsi alivyo. Msamaha bila upatanisho hatimaye ungemkosea Mungu heshima badala ya kumheshimu, hivyo hilo lisingeweza kufanyika.

Lakini Mungu ni mwenye upendo na anataka kusamehe. Hakutaka kuwaacha wanadamu wote katika hali ya dhambi, wapotee milele, ingawa hilo ndilo walilostahili.

Kujitoa kwa Yesu kama dhabihu msalabani kulitoa dhabihu yenye thamani isiyo na kikomo ambayo ilihitajika. **Yesu alistahili (1) kwa sababu ya kutokuwa na dhambi** (mkamilifu na asiyehitaji wokovu yeye mwenyewe, 2 Wakorintho 5:21), na **(2) kwa sababu ya kuwa Mungu na mwanadamu**.

Upatanisho unatoa kile kinachohitajika kama msingi wa msamaha. Sasa Mungu anaweza kumsamehe mtu anayetubu na kuamini ahadi yake. Hakuna mtu anayeelewa dhabihu ya msalabani anaweza kufikiri kwamba dhambi si jambo zito kwa Mungu.

Upatanisho unatoa njia ambayo kwayo Mungu anayezingatia haki anaweza kumhesabia haki mwenye dhambi anayeamini ahadi yake. (Soma Warumi 3:26.) Warumi 3:20-26 inatoa maelezo ya kimantiki kuhusu jinsi upatanisho unavyofanya kazi.

Biblia inatuambia kwamba njia ya wokovu ambayo Mungu alitoa ndio njia pekee kabisa. Ikiwa mtu anakataa wokovu kwa neema kwa njia ya imani katika Kristo, hawezi kuokolewa. (Soma Marko 16:15-16; Matendo 4:12; Waebrania 2:3.)

Ndio maana ni muhimu kujua kanuni ya wokovu kwa neema pekee, unaopokewa kwa imani pekee. Wokovu ni kwa neema pekee kwa sababu hakuna tunachoweza kufanya ili kuustahili. Ni kwa imani pekee kwa sababu hakuna kitu tunachoweza kufanya ili kuutimiza. Tunaweza tu kuamini ahadi ya Mungu.

## NEEMA YA KWANZA

» Je, ni nani anayechukua hatua ya kwanza kwa ajili ya wokovu wa mtu, Mungu au mtu mwenyewe?

Mungu amechukua hatua za kwanza za kumleta mwenye dhambi kwenye wokovu. Alionyesha nia yake ya kusamehe kwa kutoa dhabihu ya Yesu msalabani. Sasa neema ya Mungu inafika ndani ya moyo wa mwenye dhambi, ikimsadikisha juu ya dhambi zake na kumfanya atamani msamaha. (Soma Tito 2:11; Yohana 1:9; Warumi 1:20.) Mwenye dhambi hana uwezo wa kuacha dhambi zake bila msaada wa Mungu (Yohana 6:44). Mungu humpa mwenye dhambi uwezo wa kuitikia injili. Ikiwa mtu hajaokoka, si kwa sababu hakupewa neema, bali ni kwa sababu amekataa kutikia neema ambayo Mungu amempa.

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote, na Mungu anataka kila mtu aokolewe. (Soma 2 Petro 3:9; 1 Yohana 2:2; 1 Timotheo 4:10.) Neema ya Mungu humpa kila mtu uwezo wa kuitikia, lakini hamlazimishi yeyote. Ndio maana Mungu anamhamasisha mwenye dhambi kuchagua kutubu na kuamini (Marko 1:15).

## TOBA

» Toba ni nini?

Kutubu ni kugeuka na kuchukua mwelekeo tofauti. Kitheolojia, ina maana kwamba mwenye dhambi anajiona kuwa ana hatia na anastahili adhabu, lakini yuko tayari kuacha dhambi zake.

> Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie BWANA, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa (Isaya 55:7).

Kutubu hakumaanishi kwamba mwenye dhambi ni lazima arekebishe maisha yake na awe mwenye haki kabla ya Mungu kumsamehe. Hilo haliwezekani. Lakini mwenye dhambi lazima awe tayari kumruhusu Mungu amkomboe kutokana na dhambi zake.

» Wokovu hupokewa kwa neema, basi kwa nini toba ni muhimu kwa wokovu?

Imani ndio sharti pekee la msamaha, lakini imani kwa ajili ya wokovu haiwezi kuwepo bila toba. Ikiwa mtu hataki kutubu, hataki kuokolewa kutokana na dhambi.

Ikiwa Mungu angewasamehe watu wanaoendelea kutenda dhambi na wamekataa kutubu, hilo lingemwondolea heshima yake kama hakimu wa dunia anayezingatia haki. Toba inahitajika, kwa sababu ikiwa mtu hatatubu, basi hakubali uovu wa dhambi. Ikiwa haoni kwa nini anapaswa kujitenga na dhambi, basi haoni kwa nini anahitaji msamaha.

Ikiwa mtu hajaona kuwa kweli ana hatia, hawezi kujitetea, na anastahili adhabu, hajatubu kikamilifu. Ikiwa anakiri kwamba yeye ni mwenye dhambi lakini anataka kuendelea kutenda dhambi, toba yake haijakamilika, kwa sababu anataka kuendelea kufanya yale ambayo alisema hayataki.

## IMANI INAYOOKOA

» Ikiwa mtu ana imani inayookoa, anaamini nini?

Ikiwa mtu ana imani inayookoa, anaamini kwamba:

1. **Hawezi kufanya lolote ili kujihesabia haki.**

> Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu (Waefeso 2:8-9).

Anatambua kwamba hakuna chochote anachoweza kufanya (matendo) kitamfanya astahili kuokolewa, hata kwa kiasi fulani.

> **"Imani inayookoa ni imani inayopumzisha, tumaini ambalo linamtegemea Mwokozi kikamilifu."**
>
> **John Stott**

2. **Dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.**

> Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:2).

*Kipatanisho* inamaanisha dhabihu inayotuwezesha kusamehewa. Hakuna kitu chochote kinachohitajika mbali na kujitoa kwa Yesu kama dhabihu kwa ajili ya msamaha wetu.

3. **Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, akishinda dhambi na mauti.**

> …Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka (Warumi 10:9).

Njia pekee ambayo kwayo dhambi na mauti vingeweza kushindwa ilikuwa ni kufufuka kwa Yesu. Yesu alifufuka, akithibitisha ushindi wake kamili dhidi ya vitu hivyo viwili.

4. **Mungu anamsamehe kwa msingi wa imani pekee.**

> Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:9).

Ikiwa mtu anafikiri kuna masharti mengine ya wokovu, anatarajia kuokolewa kwa kiasi fulani kwa matendo badala ya kuokolewa na neema pekee.

## Hakikisho

» Je, ni jinsi gani watu wanaweza kujua kwa uhakika kwamba ameokoka?

Watu wengine hutegemea hisia zao, lakini hisia zinaweza kubadilika na zinaweza kupotosha.

Biblia inatuambia kwamba tunaweza kujua kwa hakika kwamba tumeokolewa (1Yohana 5:13). Tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ametukubali. Hatupaswi kuishi kwa hofu, kwa sababu Roho wa Mungu anatuhakikishia kwamba tumekuwa watoto wa Mungu. Mtume Paulo anasema kwamba Roho Mtakatifu hushuhudia roho zetu za kibinadamu kwamba sisi ni watoto wa Mungu (Warumi 8:15-16).

Hakikisho hili ni kamili sana kiasi kwamba hatupaswi kuogopa Siku ya Hukumu. (1 Yohana 4:17) Watu wengine husema kwamba wanatumaini kwamba watakubaliwa mbinguni, lakini tunaweza kuwa na hakikisho bora zaidi kuliko hilo. Haitoshi kuamini kwamba wokovu umetolewa kwa wanadamu kwa ujumla; mtu lazima ajue kwamba yeye mwenyewe ameokolewa.

Maisha yaliyobadilika ni ushahidi kwamba mtu ameokolewa, lakini ushahidi huo hauonekani hapo mwanzoni. Matokeo ya wokovu hayajapata wakati wa kuonekana. Hivyo, wakati wa kutubu, maisha yaliyobadilika si msingi wa uhakikisho.

Muumini anaweza kuwa na uhakika na wokovu wake kwa kujua kwamba amefuata njia ya kimaandiko ya wokovu. Ikiwa mtu ametubu kikweli na kuamini jinsi Biblia inavyoelekeza, ana haki ya kuamini kwamba Mungu amemsamehe na amekuwa mtoto wa Mungu.

Ikiwa mtu anajaribu kuhisi kwamba ameokoka wakati hajatubu kikweli, atachanganyikiwa na anaweza kujidanganya mwenyewe.

Ikiwa mtu (1) ametubu kikweli, (2) anatumainia ahadi za Mungu katika maandiko, na (3) amepokea ushuhuda wa Roho, hatadanganyika. Msingi wa hakikisho hilo ni Neno la Mungu, ambalo linategemeka kabisa. Mungu daima hutimiza ahadi zake.

## MANENO 10 YA VIPENGELE VYA WOKOVU

**Upatanisho**: Neno hili linamaanisha kwamba wale waliokuwa maadui hapo awali sasa wana amani kati yao. Katika wokovu, Mungu hutupatanisha na yeye na tunakuwa na amani naye. (Soma 2 Wakorintho 5:19; Warumi 5:1. Vifungu hivi vinazungumza kuhusu kuhesabiwa haki na upatanisho.)

**Kufidia**: Neno hili linamaanisha kuwa rekodi fulani imefutwa. Katika wokovu, rekodi yetu ya dhambi inafutwa. (Soma Waebrania 8:12.)

**Uridhisho**: Neno hili linarejelea kitu ambacho kilitolewa ili kuzuia ghadhabu ya mtu fulani. Katika wokovu, kujitoa kwa Yesu kama dhabihu kunazuia ghadhabu ya Mungu ya haki iliyokuwa dhidi yetu. (Soma 1 Yohana 2:2.)

**Kuwekwa Huru**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu ameokolewa kutoka kwenye nguvu za mwingine. Katika wokovu, tumeokolewa kutoka kwenye nguvu za Shetani na dhambi. (Soma Luka 1:74; Waroma 6:6, 12-18.)

**Ukombozi**: Neno hili linamaanisha kwamba kuna gharama ililipwa ili mtu awe huru. Katika wokovu, kifo cha Yesu ndio gharama iliyolipwa ili tuwe huru kutokana na utumwa na adhabu ya dhambi. (Soma Waefeso 1:7; Tito 2:14.)

**Kuhesabiwa Haki**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu fulani anatangazwa kuwa mwenye haki, au hana hatia. Katika wokovu, mwenye dhambi aliye na hatia anahesabiwa kuwa mwenye haki kwa sababu Yesu aliteseka kwa niaba yake. (Soma Warumi 5:1; 2 Wakorintho 5:19. Vifungu hivi vinazungumza kuhusu kuhesabiwa haki na upatanisho.)

**Utakaso**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anafanywa mtakatifu. Katika wokovu, mwenye dhambi aliye na hatia anabadilishwa kuwa mtoto mtakatifu wa Mungu. Nyaraka nyingi zinawarejelea waumini kuwa “watakatifu.” (Soma Waefeso 1:1, Wafilipi 1:1, Wakolosai 1:2.)

**Kufanywa Wana**: Neno hili linamaanisha mtu anakuwa mtoto halali wa mtu mwingine. Katika wokovu tunafanyika watoto wa Mungu. (Soma Yohana 1:12; Waroma 8:15.)

**Kuongoka / Kuzaliwa Upya**: Neno hili linamaanisha mtu anaanza maisha upya. Katika wokovu muumini huanza maisha mapya kupitia ufufuo wa maisha ya kiroho ndani yake. (Soma Waefeso 2:1; Yohana 3:3, 5.)

**Kutiwa Muhuri**: Neno hili linamaanisha kitu kilichotiwa alama ili kuonyesha ni nani anayekimiliki. Katika wokovu, Roho Mtakatifu ndani yetu hututambulisha kama watu wa Mungu. (Soma Waefeso 1:13-14.)

## MAKOSA YA KUEPUKA: DINI BILA TOBA

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshirika wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Kuna aina ya mtu anayefikiri kwa urahisi kwamba ameokolewa anaposikia kwamba wokovu ni kwa neema kupitia imani. Hajatubu kikweli kwa sababu hakuona kwamba anahitaji kufanya hivyo. Hakujiona kamwe kuwa mwenye dhambi anayestahili hukumu ya Mungu. Anafikiri neema inamaanisha kwamba anaweza kufuata njia zake mwenyewe. Kwa sababu anakubali ukweli wa Ukristo, anafikiri yeye ni Mkristo, ingawa maisha yake hayajabadilika. Hakusalimisha mapenzi yake; badala yake, alimkubali Mungu kama sehemu ya maisha yake, na bado anaishi kwa kiwango kikubwa kulingana na mapenzi yake mwenyewe. Huu si mwanzo wa uhusiano unaookoa na Mungu, kulingana na maelezo ya maandiko.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Maisha, kifo na ufufuo wa Yesu Kristo vinatoa upatanisho kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Kila mtu ana hatia ya dhambi na hana uwezo wa kujiokoa. Kila mwenye dhambi anayetubu anaweza kupokea neema ya Mungu kwa imani. Muumini anasamehewa na kuwekwa huru kutokana na nguvu na adhabu ya dhambi. Roho Mtakatifu humbadilisha muumini kutoka kuwa mwenye dhambi na kuwa mwabudu mtakatifu wa Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu. Uumbaji kwa ujumla umekombolewa na hatimaye utarejeshwa na Mungu.

## WOKOVU KATIKA AGANO LA KALE

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Sehemu hii na sehemu inayofuata ni za hiari. Wanafunzi wanaweza kuzizingatia ikiwa wanataka kushughulikia mada hizi.*

Katika Agano la Kale, Mungu alitoa utaratibu wa ibada na dhabihu. Dhabihu hazikutoa wokovu kwa njia sawa na kifo cha Yesu. Biblia inatuambia kwamba "haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi" (Waebrania 10:4). Basi kwa nini dhabihu zilitolewa? Zilikuwa ni aina za ibada zilizoashiria dhabihu ya Kristo itakayokuja katika siku zijazo (Waebrania 10:1).

Hiyo haimaanishi kwamba wokovu haukupatikana hadi katika enzi ya Agano Jipya. Mtume Paulo alipoeleza kanuni ya kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani, alitoa mifano ya Abrahamu na Daudi kuonyesha kwamba hilo halikuwa wazo jipya (Warumi 4:1-8). Yesu alisema kwamba Nikodemo alipaswa kujua kuhusu kuzaliwa upya kwa sababu alikuwa mwalimu wa Agano la Kale (Yohana 3:10). Paulo alimwambia Timotheo kwamba maandiko ya Agano la Kale yanaweza kumfanya awe na hekima kuhusu wokovu (2 Timotheo 3:15). Kwa hivyo, injili ilipatikana katika Agano la Kale ingawa haikuelezwa kwa uwazi kama katika Agano Jipya.

Kulikuwa na watu katika enzi ya Agano la Kale ambao walielewa neema. Hawakujua kwa kina kuhusu upatanisho au jinsi unavyofanya kazi, lakini waliamini kwamba Mungu alikuwa akitoa msingi wa msamaha. Dhabihu zilikuwa namna ya kuonyesha imani hiyo, kama vile tuna aina za ibada leo (kwa mfano, Meza ya Bwana). Dhabihu hazikuwa na thamani kama hazikutolewa kwa imani na utiifu, kama vile ibada zetu hazina thamani ikiwa hazidhihirishi moyo na maisha ambayo yamejinyenyekeza kwake Mungu. Zaburi 51 na Isaya 1:11-18 zinaonyesha kwamba toba na imani zilikuwa muhimu katika enzi ya Agano la Kale.

Zaburi 85, iliyoandikwa miaka mingi kabla ya kutokea kwa wa Kristo kutokea, inaeleza kwa uzuri neema ya Mungu na jinsi Mungu anavyosamehe dhambi. Inazungumza juu ya hasira yake kumalizika. Zaburi 85:10 inasema, "Fadhili na kweli zimekutana, haki na amani zimehusiana." Hii ni taswira nzuri sana ya wokovu kupitia upatanisho. Bila upatanisho, rehema ya Mungu ingezuiwa na ukweli kwamba tuna hatia. Haki ya Mungu ingetufanya tuwe maadui wake badala ya kuruhusu amani kati yetu na yeye. Katika upatanisho, haki inatimizwa, na rehema inaonyeshwa.

## WOKOVU WA UUMBAJI WOTE

Maneno *kuokolewa* au *wokovu* yanatumika kwa mapana katika Biblia. Yanarejelea zaidi ya wokovu wa kibinafsi tu, ambao umeelezwa katika somo hili. Maneno haya yanarejelea kile kilichotekelezwa hapo zamani (Waefeso 2:8), kile kinachotendekea sasa (1 Wakorintho 1:18), na kile kitakachotendeka siku zijazo (Marko 13:13). Dhana ya wokovu inaweza kurejelea kile kinachowatendekea watu binafsi (ambacho ndicho kilichosisitizwa katika somo hili)

lakini pia inaweza kurejelea kile kinachotendekea vikundi vya watu, kama vile Wayahudi (Warumi 1:16), Mataifa (Warumi 11:11), nyumba (Luka 19:9), au familia (Waebrania 11:7), au inaweza kurejelea mtu anayeokolewa kutokana na hatari inayoweza kumdhuru kimwili (Mathayo 14:30).

Watu wa kwanza walipofanya dhambi, laana ilingia juu ya uumbaji wote (Mwanzo 3:17). Wokovu utakapokamilika, uumbaji pia utarejeshwa.

Wokovu huanza na kufanywa upya kiroho. Waumini wanaokolewa kutokana na dhambi, na wanaishi katika baraka za Mungu. Hata hivyo, bado hawajapata kuwekwa huru kutokana na athari za kimwili za laana ya dhambi. Bado wana miili inayozeeka na kufa.

Asili bado iko chini ya laana ya dhambi. Hatujaona ulimwengu jinsi Mungu alivyouumba hapo mwanzoni. Tunaona asili ambayo imejaa viumbe hatari na viumbe walio na migogoro kati yao. Katika ulimwengu wetu, viumbe wengi lazima wafe ili wengine waishi.

Wakati unakuja ambapo uumbaji wote utafanywa upya (Ufunuo 21:1; Waebrania 1:10-12). Warumi 8:18-25 inaeleza tumaini la Kikristo la ulimwengu uliowekwa huru kutokana na laana ya dhambi.

## MAZOEZI YA SOMO LA 8

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Zaburi 51
    - Isaya 1:11-18
    - Warumi 3:20-26
    - Warumi 8:19-25
    - Waefeso 2:1-10

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 8. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 8

1. Je, kwa nini msalaba ni chukizo kwa watu wengi?
2. Orodhesha mambo manne ambayo ni ya kweli kuhusu kila mwenye dhambi asiyetubu.
3. Je, kwa nini msamaha bila upatanisho haumletei Mungu heshima?
4. Je, ni kwa njia gani mbili Yesu alistahili kipekee kuwa dhabihu?
5. Je, mtazamo wa mwenye dhambi anayetubu ni upi?
6. Mtu akiwa na imani inayookoa, anaamini nini?
7. Je, mtu anawezaje kujua kwa uhakika kwamba ameokoka?

# SOMO LA 9

# MASUALA YA WOKOVU

## MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Fursa na umuhimu wa ushindi wa muumini dhidi ya dhambi.
    - Neema ambayo Mungu hutoa kwa ajili ya kuishi kwa ushindi.
    - Maisha ya kiroho yanayotokana na uhusiano na Kristo.
    - Maonyo ya kimaandiko kuhusu kuanguka kutoka katika neema.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu masuala mahususi ya wokovu.

2. Mwanafunzi atakuwa na matarajio makubwa ya kuishi katika ushindi dhidi ya dhambi.

## UTANGULIZI

» Someni Warumi 6 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu athari za wokovu?

## USHAHIDI WA WOKOVU

Uhakikisho wa kibinafsi wa wokovu ni mojawapo ya mada kuu za waraka wa 1 Yohana. Yohana alieleza sababu yake ya kuandika waraka huu; “Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu” (1 Yohana 5:13).

» Je, mtu anapaswa kufanya nini ikiwa ana shaka kwamba ameokoka?

Mtume alijua kwamba kutakuwa na wakati ambapo muumini atahitaji hakikisho kwamba ameokoka. Anaonyesha kwamba muumini anafaa kutafuta ushahidi wa hakikisho lake. Katika waraka wake wote, anatoa mifano kadhaa ya ushahidi, akisema “hivi ndivyo

tunavyojua".[11] Alisema kwamba waumini wanaweza kutumia ushahidi huo ili kutuliza mioyo yao (1 Yohana 3:19).

Tabia ya muumini ambayo imesisitizwa zaidi katika waraka wote wa 1 Yohana ni ushindi dhidi ya dhambi. Mtume anasema, "Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi" (I Yohana 2:1). Kwa kauli hii, mtume anaonyesha kwamba muumini anapaswa kuishi maisha ya kuwa huru kutokana na dhambi ya makusudi.[12] Anaandika ili kuwaonyesha umuhimu wa kuishi kwa ushindi.

> …Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:1-2).

Hapa Yohana anatambua kwamba dhambi inaweza kutokea, ingawa si lazima. Anatuhakikishia kwamba muumini akitenda dhambi, dhabihu ya Kristo inaweza kulipia dhambi hiyo. Hilo halimaanishi kwamba muumini anaweza kutenda dhambi tena na asemehewe moja kwa moja bila kutubu. Kifungu hiki kinasema kwamba dhabihu inapatikana, kwa vile ni ya ulimwengu wote na dhambi zote. Tunajua kwamba ulimwengu wote haujaokolewa moja kwa moja. Muumini akitenda dhambi, ni lazima atubu kwa ajili ya uhusiano wake na Mungu.

Vifungu vifuatavyo kutoka 1 Yohana vinaonyesha kwamba sifa bora zaidi ya muumini ni ushindi dhidi ya dhambi ya makusudi. Maneno yaliyo ndani ya mabano ni maoni ya kuongezwa.

> Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. [Mtu asiyemtii Mungu hadhihirishi ushahidi huu]. Yeye asemaye, "Nimemjua," wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake (1 Yohana 2:3-4).
>
> Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi. Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua (1 Yohana 3:4-6).
>
> Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki [Si mtu ambaye kwa namna fulani anahesabiwa haki huku akiendelea kutenda dhambi], kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi (1 Yohana 3:7-8).

---

11 1 Yohana 2:3, 5, 29; 1 Yohana 3:10, 14, 19, 24; 1 Yohana 5:2, 18

12 Dhambi ya makusudi imejadiliwa kwa kina katika Somo la 5.

> Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu (1 Yohana 3:9).
>
> Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa. (1 Yohana 3:24). [Kukaa ndani ya Kristo hakuambatani na kuendelea kuvunja amri za Mungu.]
>
> Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito (1 Yohana 5:2-3). [Upendo wa kweli huchochea utiifu. Kutotii kunaonyesha ukosefu wa upendo.]
>
> Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu [majaribu yake na roho yake]; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (1 Yohana 5:4).
>
> Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi (1 Yohana 5:18).

» Ni sifa gani kuu ya muumini inayojitokeza wazi katika vifungu hivi?

Kutokana na vifungu hivi, inaonekana wazi kwamba sifa kuu ya muumini ni kwamba anaishi kwa kumtii Mungu. Ushindi dhidi ya dhambi ya makusudi ni fursa kubwa ya muumini.

## MAELEZO KUHUSU 1 YOHANA 1:8

Wakati mwingine watu wanaokana kwamba muumini anaweza kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi ya makusudi hunukuu 1 Yohana 1:8: "Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu." Lakini maana ya kuwa na dhambi ni nini? Je, ina maana hata waumini wanaendelea kutenda dhambi kwa makusudi? Hilo haliwezi kuambatana na kauli zilizo katika 1 Yohana 3 ambazo zimenukuliwa hapo juu. Yohana angewezaje kusema maneno hayo katika sura ya 3 kama angesema hapo awali kwamba, "Kila mtu, ikiwemo kila muumini, huendelea kutenda dhambi"? Hilo halingeweza kuwa na maana.

Muktadha unaonyesha maana. Katika 1 Yohana 1:7, utakaso wa dhambi umeahidiwa. Utakaso huu ni kwa wale wanaotembea katika nuru, ambayo inamaanisha kuishi kulingana na ukweli, kwa kumtii Mungu. Wale ambao sasa wanaishi kwa kumtii Mungu wanatakaswa kutokana na dhambi zao za zamani kwa damu ya Kristo.

Lakini kunaweza kuwa na watu wanaokana kwamba wametenda dhambi na wanahitaji kutakaswa. Hao ndio wanaosema kuwa hawana dhambi na wanajidanganya. Wanadai

kwamba hawajawahi kamwe kutenda dhambi, au kwamba wametatua tatizo lao la dhambi bila Kristo.

Tena katika 1 Yohana 1:9, msamaha na utakaso vimeahidiwa. Katika 1 Yohana 1:10, Yohana anasema tena kwamba wale wanaosema kwamba hawajatenda dhambi wanampinga Mungu mwenyewe.

Yohana alikuwa anaandika ili kusahihisha kosa la wale ambao wanafikiri hawahitaji utakaso na msamaha unaotolewa na Kristo—wale wanaofikiri kwamba hawakuhitaji kuokolewa. Hakuwa akisema kwamba hata waumini wanaendelea kutenda dhambi, kwa kuwa hilo lingepingana na msisitizo wake mkuu na kauli za moja kwa moja katika waraka huu.

## NEEMA YA MUNGU KWA AJILI YA MAISHA YA USHINDI

Kuishi katika ushindi si rahisi siku zote kwa sababu ya upotovu wa kurithi na udhaifu wa kibinadamu. Kwa sababu ya hayo, watu wengi wanaamini kwamba haiwezekani kuishi bila kufanya dhambi ya makusudi. Lakini neema ya Mungu ina suluhu ya matatizo yote mawili.

» Upotovu wa kurithi ni nini?

***Upotovu wa kurithi*** ni upotovu wa asili ya kimaadili ya mwanadamu ambayo inamsukuma kutenda dhambi tangu anapozaliwa. Baada ya kuongoka, muumini hupambana na msukumo huo wa kutenda dhambi. Lakini Mungu hutoa neema si tu kwa ajili ya ushindi wa kila siku, bali kwa ajili ya utakaso wa upotovu wa kurithi (Matendo 15:9; 1 Wathesalonike 5:23; 1 Yohana 1:7).

Asili ya dhambi si hali ambayo lazima itutawale maisha yetu yote hapa duniani. Ili kuishi kwa ushindi, muumini anahitaji kufikia hatua ya kumkabidhi Mungu moyo wake kikamilifu (Warumi 12:1). Roho Mtakatifu anapomjaza muumini, anamwezesha muumini huyo kumpenda Mungu kikamilifu.

> **“Watu hawana mwelekeo wa Utakatifu. Kando na juhudi zinazosukumwa na neema, watu hawana mwelekeo wa utauwa, maombi, kutii maandiko, imani, na kumfurahia Bwana. Tuna mwelekeo wa kulegeza msimamo na tunauita stahamala; tuna mwelekeo wa uasi na tunauita uhuru; tuna mwelekeo wa ushirikina na tunauita imani. Tunathamini utovu wa nidhamu wa kupoteza uwezo wa kujidhibiti na tunauita kujivinjari; tuna mwelekeo wa kuwa wavivu katika maombi na kujidanganya kwamba tumeepuka mtazamo wa kuzingatia sheria; tunateleza katika mwelekeo wa kutomcha Mungu na kuamini kuwa tumewekwa huru.”**
>
> **D.A. Carson**

» Udhaifu wa kibinadamu ni nini?

***Udhaifu wa kibinadamu*** ni mapungufu ya kimwili au kiakili. Kwa sababu ya anguko la Adamu katika dhambi, na kuzorota kwa hali ya wanadamu kupitia dhambi inayoendelea, sisi ni dhaifu kiakili, kimwili, na kihisia kuliko jinsi Mungu alivyotuumba kuwa.

Udhaifu wa kibinadamu hutufanya tufanye makosa. Huenda tusijue jambo sahihi la kufanya katika hali fulani. Huenda tukawa na maoni yasiyo sahihi kuhusu watu wa matabaka fulani au makabila fulani. Mawazo potovu hayarekebishwi moja kwa moja mtu anapookolewa. Mawazo potovu husababisha matendo mabaya kwa sababu mtu akiwa na wazo potovu kuhusu kile anachopaswa kufanya, atafanya jambo baya.

Udhaifu unaweza kusababisha mtu awe na matatizo kwa sababu kadhaa. Labda hajajifunza jinsi ya kutumia kanuni za kimaandiko. Labda hajakuza nidhamu ambazo zingemsaidia kupinga misukumo yake. Labda hana tabia za kila siku ambazo zingemsaidia kuwa na nguvu. Labda haelewi umuhimu wa kuenenda katika Roho.

Hatupaswi kuwa wepesi kuwahukumu wengine, kwa sababu hatuwezi kujua wakati wote wakati wanapofanya dhambi kwa makusudi. Mara nyingi watu hufanya makosa kwa sababu ya ukosefu wa ufahamu na ukomavu wa kiroho.

Je, umewahi kukabiliwa na jaribu ambalo ulifikiri hakuna mtu mwingine amewahi kukabiliwa nalo? Je, umewahi kujiuliza kama kweli inawezekana kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi kikamilifu? Mungu ameahidi neema inayowezesha ambayo inatosha kabisa kufidia udhaifu wetu katika majaribu:

> Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. (1 Wakorintho 10:13).

» Je, ni mambo gani tunajua kutokana na kifungu hiki?

Kifungu hiki kinatuambia mambo kadhaa muhimu.

1. **Majaribu huja kwa sababu ya ubinadamu wetu**. Hiyo ina maana kwamba mapambano yako si ya kipekee.

2. **Mungu anajua mipaka yetu**. Anaelewa tunaweza kustahimili kwa kiwango gani. Hatujui tunaweza kustahimili kwa kiwango gani, lakini yeye anajua.

3. **Mungu huweka mipaka katika majaribu yanayotujia**. Anataka tuishi kwa ushindi. Kulingana na kifungu hiki, ushindi wakati wote unawezekana.

4. **Mungu hutoa kile tunachohitaji kwa ajili ya ushindi**. Anatuandalia njia ya kujinasua. Mungu anataka tuishi kwa ushindi. Anatoa neema kwa ajili ya kuishi kwa ushindi.

## MAISHA KATIKA ROHO

» Nenda katika Warumi 8 na uangalie vifungu vilivyotumiwa katika sehemu hii.

Warumi 8 inatoa maelezo mazuri sana kuhusu kazi ya Roho katika maisha ya muumini. Warumi 8:26 inatuambia kwamba hata hatujui jinsi ya kuomba ipasavyo, lakini Roho Mtakatifu huomba kupitia sisi.

Sura hii inatueleza jinsi ya kuishi maisha ya ushindi. Hatutahukumiwa ikiwa tunafuata Roho badala ya mwili (Warumi 8:1, 4). Tunaweza kutimiza haki ambayo Mungu anatarajia tutimize, kwa sababu nguvu ya Roho inafanya kazi ndani yetu (Warumi 8:4).

Ikiwa mtu anatawaliwa na asili ya dhambi, hawezi kumpendeza Mungu (Warumi 8:8), amehukumiwa (Warumi 8:1), na amehukumiwa na Mungu ("kufa" katika Warumi 8:13). Lakini kwa uwezo na mwongozo wa Roho Mtakatifu, tunaweza kukomesha matendo ya dhambi (Warumi 8:13-14).

## MAISHA NDANI YA KRISTO

Katika Yohana 15:1-10 kuna sitiari maarufu ya mzabibu na matawi. Inajibu maswali muhimu.

Je, ni jinsi gani tunakaa ndani ya Kristo? "Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake" (Yohana 15:10). Kuacha kukaa ndani ya Kristo kunamaanisha kwamba mtu ameacha kumtii Kristo. Basi nini kitatokea?

"Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea" (Yohana 15:6). Ikiwa mtu ataacha kutii, na hivyo basi akaacha kukaa ndani ya Kristo, anakataliwa. Mfano wa matawi yanayoteketezwa unaonyesha kukataliwa kabisa.

"Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu" (Yohana 15:4). "Kila tawi ndani yangu lisilozaa

> **"Lazima iwe muhimu kwa Mungu, kwani anatuambia kwamba 'pasipo utakatifu hakuna mtu atakayemwona Bwana' (Waebrania 12:14). Utakatifu si orodha ya mambo unayopaswa kufanya na usiyopaswa kufanya. Badala yake, ni kufanana na Kristo."**
>
> **Jim Cymbala**

huliondoa" (Yohana 15:2). Ikiwa hatutakaa ndani ya Kristo kwa kumtii, hatuwezi kuzaa matunda. Kuzaa matunda kunamaanisha kuishi maisha yaliyobadilishwa, yenye baraka, na yanayoongozwa na neema ya Mungu. Mtu asipomtii Mungu, anajitenga na mtiririko wa uzima ambao Mungu anatoa na hawezi tena kuishi chini ya neema ya Mungu. Asiyezaa matunda anakataliwa.

Kristo ni kama mzabibu unaotupatia uzima (Yohana 15:6). Wokovu unapatikana kwa njia ya uhusiano. Kutengwa na Kristo ni kutengwa na wokovu. Tunadumisha uhusiano unaookoa na Kristo kwa kumwamini na kumtii Mungu (Yohana 15:10).

Balbu za mwanga na umeme ni kielelezo cha kisasa cha dhana hiyo ya uhusiano na Kristo. Balbu huwa na mwanga wakati nguvu ya umeme inapita ndani yake. Balbu haiwezi kuendelea kuwaka ikiwa imetenganishwa na chanzo chake cha nguvu za umeme. Vivyo hivyo, tuna uzima wa milele kupitia uhusiano wetu na Kristo (Yohana 17:3). Uzima wake unatiririka ndani yetu. Hatuwezi kudumisha uzima huo tukijitenga naye.

## MAONYO KATIKA MAANDIKO

Watu wengine husema kwamba jina haliwezi kuondolewa kutoka kwenye kitabu cha uzima kwa njia yoyote baada ya kuandikwa humo. Lakini kuna angalau njia moja ambayo kwayo jina linaweza kuondolewa:

> Na mtu ye yote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki (Ufunuo 22:19).

Kuna watu wachache sana ambao wana hatia ya kuondoa sehemu ya kitabu cha Ufunuo. Hata hivyo, hoja inatolewa kwamba inawezekana jina kuondolewa kutoka kwenye kitabu cha uzima.

Yesu alitoa ahadi na onyo aliposema, "Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima" (Ufunuo 3:5).

Kuna wakati ambapo Paulo alikuwa na wasiwasi kwamba waongofu wake katika mji wa Thesalonike huenda wameacha imani yao. Alisema kwamba kama hilo lingetokea, juhudi zake za kuwahubiria Injili zingekuwa kazi bure (1 Wathesalonike 3:5). Hii inaonyesha kwamba inawezekana muumini kuanguka kutoka katika imani yake kabisa kiasi kwamba uongofu wake wa awali unakuwa hauna thamani yoyote.

Katika 2 Petro 2:18-21 tunaona kwamba kuna walimu wa uongo wanaowapotosha baadhi ya waumini ambao walikuwa wameepuka uchafu wa dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Waumini hao wa awali walikuwa wameijua njia ya haki lakini wakaiacha. Andiko hili linasema kwamba afadhali wasingejua njia ya Kristo kuliko kurudi kwenye

maisha ya dhambi. Hii inaonyesha kwamba inawezekana mtu kupoteza wokovu wake kwa kurudi katika dhambi. Kama isingewezekana mtu kupoteza wokovu wake, mtu asingeweza kuwa katika hali mbaya zaidi kuliko kabla ya kuokoka.

Uwana unaweza kubadilishwa. Wakati mmoja tulikuwa watoto wa Ibilisi (Yohana 8:44) na wana wa ghadhabu (Waefeso 2:2), lakini uwana huo unabadilishwa tunapofanywa wana wa Mungu (Warumi 8:15). Mwana mpotevu alipoteza faida zote za uwana alipokuwa amejitenga na baba yake. Aliporudi, baba yake alisema kuwa alikuwa amekufa (Luka 15:32).

Mungu anataka waumini wajihisi salama, lakini si kwa kuruhusu hisia zao zishawishiwe na hakikisho la uongo linalofanya wajiweke hatarini. Hatupaswi kuwaahidi waumini kitu ambacho Mungu hajaahidi. Hajaahidi kwamba tutakuwa salama kutokana na kupoteza wokovu wetu haijalishi tunafanya nini. Anaahidi kwamba atatuongoza na kutuwezesha kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi. Hilo ni hakikisho linalotosha kutufanya tusiwe na hofu.

Wakati mwingine waumini huwa na shaka na wokovu wao. Wanaweza kuwa na uhakika kwamba waliwahi kuokoka, lakini wana shaka kwamba bado wako katika uhusiano unaookoa na Mungu. Biblia haituachi na shaka yoyote kuhusu suala hili muhimu. Ni mapenzi ya Mungu kwamba muumini awe na uhakika kabisa na wokovu wake kiasi kwamba awe na ujasiri kwa ajili ya siku ya hukumu, (1 Yohana 4:17) bila kujiuliza kama atapita mtihani wa Mungu au la.

Muumini anapokuwa na shaka, hatakiwi kuipuuza kwa sababu ana uhakika kwamba aliwahi kuokoka wakati fulani. Unafaa kujichunguza ili uone kama uko katika imani (2 Wakorintho 13:5). Ikiwa mtu anajua kwamba aliokolewa kwa kufuata hatua za maandiko za wokovu, na kwamba anakaa ndani ya Kristo kwa kuenenda katika uhusiano wa utiifu naye, anaweza kuwa na uhakika kwamba ana uzima wa kiroho.

## MAKOSA YA KUEPUKA: MATARAJIO DUNI

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Washirika wawili wa darasa wanaweza kueleza sehemu hii na sehemu inayofuata.*

Ushindi dhidi ya dhambi unaonekana hauwezekani kwa watu kwa sababu ya mambo mawili: udhaifu wa kibinadamu na upotovu wa kurithi. Ni lazima tukumbuke kwamba Mungu hatuhukumu kwa kuwa tuna mapungufu ya kibinadamu. Mungu hutoa nguvu kwa Roho wake ili tuweze kutimiza mapenzi yake. Si dhambi kuwa na udhaifu, na si lazima mtu yeyote atende dhambi kwa sababu ya udhaifu.

Ushawishi wa upotovu wa kurithi huendelea baada ya kuongoka, lakini Mungu hutoa neema kwa ajili ya utakaso. Hatulaumiwi kwa kuzaliwa na upotovu wa kurithi, lakini ni kosa letu ikiwa tutaendelea kuathiriwa nao. Kwa hivyo, udhaifu wa kibinadamu na upotovu wa kurithi havipaswi kutufanya tupoteze tumaini la kuishi kwa ushindi.

Kupitia imani katika Kristo, tunaunganishwa naye. Tunajitambulisha naye katika kifo na ufufuo wake, na kwetu hilo linamaanisha kuwa wafu kwa dhambi na ufufuo katika maisha mapya (Warumi 6:3-11). Yuko ndani yetu, nasi tuko ndani yake. Maisha ya Kikristo si tu kwamba tujaribu kufuata mfano wake, tukijaribu kadiri tunavyoweza. Tunaishi maisha ya Kikristo kwa kuwa na Kristo ndani yetu. Alipata ushindi dhidi ya dhambi alipotembea duniani, na bado anaishi kwa ushindi ndani yetu.

## KWA NINI HILO NI MUHIMU

Mwanamke maskini aliyevalia matambara ameketi kando ya barabara ya jiji kubwa. Nywele zake zimesokotana na kuchanganyikana na uchafu. Ngozi yake ni chafu. Ameketi katika hali ya kukata tamaa na kukosa tumaini. Ghafla, kuna mtafaruku mkubwa na anayejitokeza barabarani akiwa kwenye gari la farasi ni mwanafalme mkuu wa ufalme pamoja na watu wake wakuu. Mwanafalme huyo ni mwenye sura ya kuvutia, mwenye nguvu, na mkarimu! Gari lake lilipokuwa linapita mahali ambapo mwanamke huyo mchafu alikuwa amekati, mwanafalme huyo anamwambia dereva wake, “Simama!”

Gari linaposimama, mwanamfalme anawaambia watumishi wake, “Yule mwanamke aliyeketi kando ya barabara ndio mwanamke ninayetaka kumwoa!”

Sasa eneo linabadilika. Tunatazama ikulu ya mfalme siku ya harusi. Tunaona nini? Mwanamke mchafu akiwa bado amevalia matambara na mwenye nywele chafu zilizosokotana. Amezungukwa na wahudumu wake wa kibinafsi, wakiwa wameshika rinda la harusi, sabuni, na manukato, lakini bibi harusi hana haja na kujitayarisha kwa ajili ya siku yake ya harusi. Mmoja wa wanawake hao anauliza, “Bibi yangu, hutaki kujitayarisha kwa ajili ya harusi?” Bibi harusi anajibu, “Hivi ndivyo nilivyokuwa mwanafalme aliponiona na akataka kunioa, kwa hivyo nadhani haijalishi nitaonekanaje leo.”

Mtazamo huo ungetushtua. Kwa sababu mwanafalme anampenda, hataki abaki katika hali yake. Kwa sababu mwanamfalme alimpenda wakati hakuvutia, mwanamke huyo anapaswa kutaka kuonekana wa kuvutia zaidi kwake.

Mungu anatupenda wakati sisi ni wenye dhambi, lakini hilo halimaanishi kwamba dhambi si jambo zito. Kwa sababu anatupenda, anataka kubadilisha hali yetu. Kwa sababu anatupenda, tunapaswa kutaka kuwa na taswira na tabia inayompendeza.

## MAAGIZO YA KIUTENDAJI YA KUISHI KWA USHINDI

Kote ulimwenguni ukweli wa Kikristo unachanganywa na ushirikina. Watu wengine hufundisha ushindi dhidi ya dhambi kupitia maombi ya kurudiwarudiwa, matukio ya kihisia, kukemea roho waovu (ambao wanafikiriwa kuwa chanzo cha dhambi fulani), kujiumiza, kuvaa hirizi fulani, kuweka ishara za kiroho sehemu mbalimbali za nyumba, au kupaka mafuta maalum kwenye mwili. Ni makosa kutarajia ushindi kupitia mazingaombwe ya kiroho!

Wengine pia hufundisha ushindi dhidi ya dhambi kwa mtazamo rahisi sana. Wanasema kwamba wokovu na ujazo wa Roho utavunja nguvu za dhambi milele. Hawasisitizi hitaji la kukua wa kiroho, nidhamu, na kuwa macho siku zote.

Wale ambao wanashindwa kupata ushindi thabiti dhidi ya ulimwengu na dhambi wanapaswa kujiuliza maswali yafuatayo:

1. **Je, kweli nimezaliwa upya?** Je, mimi ni mfu kwa maisha yangu ya zamani; nimetubia na kuiacha nyuma maisha yangu ya zamani? Je, nina maisha mapya katika Kristo—mitazamo mipya, matamanio mapya, shauku mpya kwa mambo ya Mungu (2 Wakorintho 5:17)? Je, Kristo amekuja kukaa ndani ya moyo wangu kwa njia ya Roho Mtakatifu? Je, ninajaribu kushinda dhambi kupitia nguvu za kibindadmu, au ninategemea nguvu ya Mungu inayokaa ndani yangu (Wagalatia 2:20)?

2. **Je, nahifadhi Neno la Mungu moyoni mwangu?** Mwandishi wa Zaburi alishuhudia akisema, "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi" (Zaburi 119:11). Tunahitaji kula Neno la Mungu kama vile mtoto mchanga anavyokunywa kwa hamu maziwa ya mama yake (1 Petro 2:2).

3. **Je, kweli ninajiona kuwa mfu kwa dhambi na hai kwa Mungu?** "Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu" (Warumi 6:11). Je, ninakataa majaribu nikiwa na uhakika kwamba hayana nguvu juu yangu?

4. **Je, ninamtegemea Mungu kwa ajili ya ushindi?** Mtume Yohana alitangaza kwamba mtu aliyezaliwa katika familia ya Mungu huushinda ulimwengu. "Na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." (1 Yohana 5:4). Mtume Paulo alisema kwamba hataweka imani katika kitu chochote isipokuwa msalaba wa Yesu, kwani ni kupitia msalaba ndio mambo ya kidunia yanapoteza uwezo wao wa kutuvutia na kututawala (Wagalatia 6:14). Haiwezekani sisi kuishi maisha ya ushindi thabiti ikiwa tutasahau chanzo cha haki yote, Yesu.

5. **Je, ninajivika Bwana Yesu kwa imani kila siku na kutopatia dhambi nafasi hata kidogo?** Haijalishi tuko katika hatua gani katika safari yetu ya Kikristo, ushindi hauji moja kwa moja. Lazima nidhamirie kuchukua mtazamo wa Yesu juu ya dhambi na kufuata mfano wake. (Warumi 13:14; Waefeso 4:24)

6. **Je, ninajivika silaha za kiroho za Mungu?** Katika uwanja wa vita vya maisha waumini wengi hujeruhiwa na mishale ya Shetani yenye moto kwa sababu wamekosa kuwa waangalifu kuhusu ulinzi wao wa kiroho (Waefeso 6:11).

7. **Je, ninazingatia nidhamu ya kibinafsi?** Haijalishi tumekomaa kiasi gani katika imani yetu, siku zote tutahitaji kuzingatia nidhamu ya kibinafsi. Je, ninauzoeza mwili wangu na kuufanya uwe na nidhamu? Tamaa za asili nilizopewa na Mungu

(kama vile hamu ya chakula, usingizi, au ngono) lazima zidhibitiwe, ili zitumike kwa makusudi ya nafsi yangu iliyozaliwa upya. Kwa sababu mwili wangu umeharibiwa na dhambi, tamaa zake hazina usawa.Ni lazima mwili usiruhusiwe kutawala; lazima utumikie roho. Paulo alisema kwamba aliutia mwili nidhamu wake na kuufanya umtii ili asiwe mtu aliyekataliwa kiroho (1 Wakorintho 9:25-27). Nidhamu hii ni muhimu kwa kila Mkristo.

8. **Je, ninaishi kwa utiifu?** “Tuenende nuruni” ni himizo la Mtume Yohana (1 Yohana 1:7). Kwa sababu kuna mitego mingi, mawe ya kukwaza, na sehemu hatari kwenye barabara ya kwenda mbinguni, lazima tuenende katika nuru ya Neno la Mungu (Zaburi 119:105) na uwepo wa Roho Mtakatifu (Yohana 14:26). Utiifu unabeba ahadi kwamba damu ya Yesu itatudumisha katika usafi. Kutembea gizani hufanya tukajikwaa na kuanguka na hatimaye kifo kwa wale wanaokataa kuirudia njia ya nuru.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Ni fursa na wajibu wa kila muumini kuishi maisha ya Kikristo yenye ushindi. Muumini ana uzima kutokana na uhusiano alionao na Kristo. Muumini anayekataa mapenzi ya Mungu na kurudi kwenye dhambi hudhoofisha na anaweza kuharibu imani yake, ambayo ndio inayotuunganisha na Mungu. Mungu hutoa neema ya kutia nguvu, ili muumini aweze kushinda kila jaribu.

## MAZOEZI YA SOMO LA 9

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Mathayo 13:18-23
    - Waebrania 10:23-39
    - Yakobo 1:21-27
    - 2 Petro 1:1-11
    - Ufunuo 3:14-22

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 9. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 9

1. Je, mojawapo ya mada kuu za 1 Yohana ni ipi?
2. Je, 1 Yohana inasisitiza zaidi sifa gani ya muumini?
3. Je, ni mambo gani manne tunayojua kutoka katika 1 Wakorintho 10:13?
4. Je, muumini huendeleaje kukaa ndani ya Kristo?
5. Je, tunadumishaje uhusiano unaookoa na Kristo?

## SOMO LA 10

# ROHO MTAKATIFU

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:
   - Sifa zinazoonyesha kwamba Roho Mtakatifu ni mtu.
   - Ushahidi wa Biblia wa utu na uungu wa Roho Mtakatifu.
   - Kwa nini utu na uungu wa Roho Mtakatifu ni kanuni muhimu.
   - Kazi ya Roho Mtakatifu ya kihistoria na ya sasa.
   - Vipengele vya kiutendaji vya uhusiano wa muumini na Roho Mtakatifu.
   - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu Roho Mtakatifu.
2. Mwanafunzi atatumia kanuni fulani kuhusu karama za Kiroho.

## UTANGULIZI

» Someni Zaburi 139 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu Roho wa Mungu?

Watu wengine hufikiri kwamba Roho Mtakatifu ni kitu kinachochochea tu hisia zao, nguvu wanayojaribu kutumia, nguvu isiyo na utu, au uwepo fulani tu. Kwa mfano, Shahidi wa Yehova atasema hivi: "Roho mtakatifu si mtu, wala si sehemu ya Utatu wa Mungu. Roho mtakatifu ni nguvu ya Mungu anayotumia kutimiza mapenzi yake…. Kwa kiasi fulani, inaweza kulinganishwa na umeme."[13]

» Ni nini ambacho si sahihi kuhusu maoni ya Mashahidi wa Yehova kuhusu Roho Mtakatifu?

Mashahidi wa Yehova wanamwona Roho Mtakatifu kama nguvu isiyo na utu. Kwa sababu hawana ufahamu wa kibiblia juu ya Mungu, hawawezi kuwa na uhusiano sahihi naye.

---

13 *Should You Believe in the Trinity?* (New York: The Watchtower Bible and Tract Society, 1989)

Hatupaswi kutarajia kuelewa mambo yote kuhusu Roho Mtakatifu. Yesu alisema kwamba kazi ya Roho ni kama upepo; unaisikia, lakini hujui itokako wala iendako (Yohana 3:8). Lakini kuna mambo fulani ambayo tunaweza kujua kuhusu Roho, na ni muhimu katika uhusiano wetu na Mungu.

Sehemu ya maandiko inayotupa maelezo mengi zaidi kuhusu mwingiliano kati ya Roho Mtakatifu na kanisa ni kitabu cha Matendo. Hapo tunaona mfano wa jinsi kanisa la hapo mwanzoni lilivyomwitikia Roho Mtakatifu.

1. Walimheshimu Roho Mtakatifu katika uungu wake. (Soma Matendo 5:3-4.)

2. Walikuwa na ufahamu wa uwepo, mwongozo, na kazi ya Roho Mtakatifu. (Soma Matendo 15:28.)

3. Walitambua utegemezi wao kwa Roho Mtakatifu na wajibu wao wa kumwitikia. (Soma Matendo 4:24, 31.)

Ili kuwa na uhusiano wa aina hiyo na Roho Mtakatifu, ni lazima tutambue kwamba yeye ni mtu na kwamba yeye ni Mungu.

> **"Na ninamwamini Roho Mtakatifu, Bwana na mtoa uzima, atokaye katika Baba na Mwana, anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana; aliyenena kwa midomo ya manabii."**
>
> Kanuni ya Imani ya Nisea.

## Roho Mtakatifu ni Mtu

Roho Mtakatifu hana mwili wa nyama kama Yesu, lakini yeye *ni* mtu. Mtu halisi ana sifa za utu, ambazo ni pamoja na akili, nia na hisia. Je, Roho Mtakatifu ana nia? Anagawa karama za kiroho kwa Wakristo kama apendavyo (1 Wakorintho 12:11). Je, Roho Mtakatifu ana akili? Yeye huchunguza kila kitu, hata mafumbo ya Mungu na kuyajua (1 Wakorintho 2:10). Je, Roho Mtakatifu ana hisia? Tunaambiwa tusimhuzunishe Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30). Ikiwa Roho Mtakatifu anaweza kuhuzunishwa, basi ana hisia. Kwa sababu Roho Mtakatifu ana akili, nia na hisia, tunajua kwamba yeye ni mtu.

» Je, kwa nini ni muhimu kwetu kujua kwamba Roho Mtakatifu ni mtu?

Mtu mwenye utu ana uwezo kuwa na mahusiano na wengine. Kama Roho Mtakatifu ingekuwa nguvu isiyo na utu, tusingeweza kuwa na uhusiano naye. Lakini kulingana na Wafilipi 2:1 na 2 Wakorintho 13:14, Roho anaweza kuwa na ushirika nasi, hivyo lazima awe ni mtu.

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Kwa ushahidi zaidi wa Biblia kuhusu utu wa Roho Mtakatifu, tazama sehemu ya "Ushahidi wa Biblia Kuhusu Utu wa Roho Mtakatifu" mwishoni mwa somo hili.*

## Roho Mtakatifu Ni Mungu

Roho Mtakatifu ni Mungu mjua yote, anayeona yote na aliye kila mahali. Unakumbuka simulizi ya Anania na Safira? Kabla Anania hajauawa, Petro alimwambia, “Kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu…? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu” (Matendo 5:3-4). Kutokana na hayo, tunaona kwamba kumdanganya Roho Mtakatifu ni sawa na kumdanganya Mungu; kwa hivyo, Roho Mtakatifu ni Mungu.

**Roho Mtakatifu anajua mambo yote**. Tunaona katika 1 Wakorintho 2:10-11 kwamba anajua mambo yote ya Mungu. Hiyo inahitaji akili isiyo na kikomo. Alihamasisha maandiko ya Agano la Kale, ikiwemo unabii, ambayo ingehitaji maarifa yote. (Soma 2 Petro 1:21.) Tunaambiwa kwamba maandiko yana pumzi ya Mungu (2 Timotheo 3:16), hivyo Roho Mtakatifu ni Mungu.

**Roho Mtakatifu yuko kila mahali**. Zaburi 139:7-10 inatuambia kwamba hakuna mahali ambapo mtu anaweza kwenda ili kuepuka uwepo wa Roho wa Mungu. Yupo pamoja na kila muumini, kwa sababu Biblia inasema kwamba ikiwa mtu hana Roho wa Kristo, yeye si wa Kristo (Warumi 8:9). Muktadha unaonyesha kwamba Roho wa Kristo ni Roho Mtakatifu.

> **“Tunamwamini Roho Mtakatifu aliyenena katika torati, na ambaye manabii walifundisha kumhusu, aliyeshuka Yordani, aliyezungumziwa na Mitume, na anakaa ndani ya watakatifu; hivi ndivyo tunavyoamini kumhusu: kwamba yeye ni Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho kamili, Msaidizi, ambaye hakuumbwa, atokaye kwa Baba na kupokewa na Mwana, ambaye tunamwamini.”**
>
> Kanuni ya Imani ya Epifania,
> Mwaka wa 374 B.K.

**Roho Mtakatifu ana nguvu zote**. Anafanya mambo ambayo Mungu pekee ndiye anaweza kufanya. Anasadikisha ulimwengu juu ya dhambi, haki, na hukumu (Yohana 16:8). Ili kufanya hivyo, lazima aweze kufikia dhamiri ya kila mtu na kushawishi akili zao kuhusu kweli fulani. Pia ana uwezo wa kumpa kila muumini nguvu ya ndani. (Soma Waefeso 3:16.) Roho huzaa matunda ya kiroho katika maisha ya kila muumini, kila mahali ulimwenguni. (Soma Wagalatia 5:22-23.) Hakuna kitu kingine kingeweza kufanya hivyo isipokuwa nguvu za kiungu.

Tunaambiwa katika Luka 12:10 kwamba **Roho Mtakatifu anaweza kukufuriwa**. Mungu pekee ndiye anayeweza kukufuriwa, kwa hivyo Roho Mtakatifu lazima awe ni Mungu.

**Roho Mtakatifu ni wa milele** (Waebrania 9:14).

Miili yetu inaitwa hekalu **la Mungu** kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi humo (1 Wakorintho 3:16).

Kutokana na ushahidi wa Biblia, tunajua kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu mwenyewe, nafsi ya tatu ya Utatu wa Mungu.

» Je, kwa nini ni muhimu kwetu kuamini uungu wa Roho Mtakatifu?

Ni muhimu kuamini uungu wa Roho Mtakatifu ili uweze kumpa heshima anayostahili. Ni kosa kubwa sana kukataa kumwabudu Roho Mtakatifu.

## ROHO MTAKATIFU NI TOFAUTI NA BABA NA MWANA

Kusema kwamba Roho Mtakatifu ni tofauti na Baba na Mwana hakumaanishi kwamba wao ni tofauti kama vile ilivyo katika wanadamu. Kila mtu wa Utatu wa Mungu anaishi ndani ya mtu mwiingine na watu wote ni Mungu mmoja, lakini wako tofauti vya kutosha kiasi kwamba wanaweza kusemezana, kupendana, na kuwa na mahusiano ya kweli na ya kibinafsi kati yao na kati yao na sisi.

Maandiko yanafundisha tofauti kati ya nafsi za Utatu wa Mungu. Kwa mfano, tena na tena katika Yohana 14-16, Yesu alizungumza kuhusu Msaidizi atakayemtuma atakaporudi kwa Baba. (Soma Yohana 14:16-17, 26; Yohana 15:26; Yohana 16:7, 13-15.) Msaidizi huyo atawaongoza na kuwafundisha wanafunzi. Ikiwa Yesu na Roho Mtakatifu wangekuwa mtu mmoja, Yesu kumtaja Roho Mtakatifu kama msaidizi *mwingine* kusingekuwa na maana. Bila shaka Yesu alikuwa akimzungumzia mtu mwingine aliye tofauti naye.

Yesu alisema kwamba Roho Mtakatifu hatanena kwa mamlaka yake mwenyewe bali atafunua mambo ya Kristo, ambayo Kristo aliyapokea kutoka kwa Baba (Yohana 16:13-15). Ikiwa Yesu na Baba wangekuwa mtu mmoja na Roho Mtakatifu, kauli hii isingekuwa na maana.

Yesu alipobatizwa, sauti kutoka mbinguni ilisema, “Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu,” na Roho Mtakatifu, kama njiwa, akashuka juu ya Yesu (Marko 1:10-11). Washiriki wote watatu wa Utatu wanahusika kwa wakati mmoja katika tukio hili, kila mmoja akiwa tofauti na wenzake.

Kama mtu tofauti, Roho Mtakatifu siku zote ameishi katika uhusiano wa upendo na Baba na Mwana. Mungu alituumba ili tushiriki katika uhusiano huo. Mungu anataka tufurahie ushirika naye (1 Yohana 1:3-4), kwani kila mshiriki wa Utatu wa Mungu amefurahia ushirika na wale washiriki wengine tangu kabla ya mwanzo wa wakati. (Soma Yohana 17:22-23.)

## ROHO MTAKATIFU ANAFANYA KAZI

Tangu wakati wa Uumbaji, Roho Mtakatifu amekuwa akifanya kazi ulimwenguni. Alikuwepo na alihusika dunia ilipoumbwa (Mwanzo 1:2, 26). Alitoa uwezo maalum kwa watu walioitwa

kufanya kazi maalum (Kutoka 35:30-31; Waamuzi 3:9-10; Waamuzi 15:14-15). Alitoa jumbe kwa manabii (Isaya 61:1). Alihamasisha maandiko (2 Petro 1:21). Siku zote amekuwa akifanya kazi katika mioyo ya watu, akijaribu kuwaelekeza kwa Mungu (Matendo 7:51).

Anaitwa Roho wa uzima. (Soma Waroma 8:2.) Yeye ndiye Roho aliyetuumba na kutupa uhai. Kama angejiondoa kutoka katika ulimwengu, uhai wote ungekoma, na mwanadamu angerudi mavumbini. (Ayubu 33:4; Ayubu 34:14-15.)

Agano Jipya lilianzisha kipengele kipya cha kazi ya Roho Mtakatifu. Yohana Mbatizaji alisema kwamba Yesu atawabatiza watu kwa Roho Mtakatifu (Mathayo 3:11). Yesu aliwaambia wanafunzi wake watarajie ahadi ya Baba, ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao ulifanyika siku ya Pentekoste (Matendo 1:4-5, 8).

Yesu aliwaahidi wanafunzi kwamba Roho Mtakatifu atakuwa pamoja nao, akiwakumbusha mambo ambayo Yesu alifundisha na kuwaongoza katika ukweli (Yohana 14:26, Yohana 16:13). Yesu alisema kwamba Roho Mtakatifu atakuwa Msaidizi mwingine (Yohana 14:16, 26; Yohana 15:26; Yohana 16:7). Neno la Kigiriki ambalo Yesu alitumia linarejelea mtu aliye pamoja nasi, anayetutia moyo na kutusaidia. Neno hilo linaweza pia kurejelea mwakilishi. Roho Mtakatifu anamwakilisha Yesu na hutukumbusha maneno yake.[14]

» Je, baadhi ya mambo yanayofanywa na Roho Mtakatifu ni yapi?

Kazi ya Roho Mtakatifu ulimwenguni haiwezi kuelezwa kikamilifu, lakini hii hapa ni orodha ya baadhi ya kazi zake.

1. Anasadikisha juu ya dhambi (Yohana 16:8; 1 Wakorintho 2:4; 1 Wathesalonike 1:5). Vinginevyo isingewezekana mtu kutambua kwamba anahitaji kutubu na kusamehewa.

2. Anamwezesha mtu kuzaliwa upya, akimpa uzima mtu ambaye alikuwa mfu katika dhambi (Tito 3:5; Waefeso 2:1; Yohana 3:5).

3. Anampa muumini hakikisho la kibinafsi kwamba ameokolewa (Warumi 8:16).

4. Anaishi ndani ya kila muumini (kila mtu aliyeokoka ana Roho Mtakatifu) (Warumi 8:9; 1 Wakorintho 6:19).

5. Anawezesha uelewa wa ukweli wa Mungu (1 Wakorintho 2:9-10, 13-14; 2 Wakorintho 3:14-17; Waefeso 6:17).

6. Anawaita watu kwenye huduma maalum na kuongoza maamuzi katika huduma (Mdo 13:2-4, Mdo 15:28, Mdo 16:6-10).

---

14 Neno hilo hilo liko katika 1 Yohana 2:1, inayosema kwamba Yesu ni mwakilishi wetu kwa Baba.

7. Anamtakasa muumini, akiusafisha moyo wake ili kumfanya awe mtakatifu (Matendo 15:8-9; 1 Petro 1:2).

8. Anatoa uwezo wa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi (Warumi 8:1, 5, 13; Wagalatia 5:16).

9. Anazaa matunda ya kiroho katika maisha ya muumini (Wagalatia 5:22-23).

10. Anatoa karama kwa ajili ya huduma (1 Wakorintho 12:4-10, 28-30; Warumi 12:6-8; 1 Petro 4:10-11).

11. Anatoa upako maalum wa nguvu kwa ajili ya huduma (Matendo 1:8, Matendo 13:9; Wagalatia 3:5; 1 Petro 1:12).

12. Anamsaidia muumini kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu (Warumi 8:26-27; Waefeso 6:18).

13. Anakuza umoja na ushirika wa kanisa (Waefeso 4:3; Wafilipi 2:1).

## BAADHI YA KANUNI KUHUSU KARAMA ZA KIROHO

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshirika wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

1. Roho hufanya kazi kupitia karama, shughuli na usimamizi mbalimbali (1 Wakorintho 12:4-6).

2. Karama za kiroho zinagawanywa kulingana na mapenzi ya Mungu, si kulingana na hali ya kiroho ya mtu (1 Wakorintho 12:11, 1 Wakorintho 4:7).

3. Kila mtu ana uwezo fulani aliopewa na Roho (1 Wakorintho 12:7).

4. Hakuna karama ambayo kila muumini anatarajiwa kuwa nayo (1 Wakorintho 12:8-11, 14-30).

5. Karama siku zote zinapaswa kutumiwa kwa ajili ya kuwatumikia wengine kwa utukufu wa Mungu (1 Wakorintho 12:21-22, 25; 1 Petro 4:10-11).

## KARAMA YA LUGHA

Si Wakristo wote wanakubaliana kuhusu matumizi ya karama ya lugha. Wakristo wengine wanaamini kwamba kila muumini atanena kwa lugha atakapopokea Roho Mtakatifu.

Wakristo wengine wanaamini kwamba karama ya lugha hutolewa kwa baadhi ya waumini kwa ajili ya mawasiliano na watu wanaozungumza lugha tofauti. Wanaamini hivyo kwa

sababu siku ya Pentekoste wasemaji walieleweka katika lugha nyingi (Matendo 2:6). Wanaamini kwamba Mungu hutoa karama hiyo, na karama nyingine yoyote ya kiroho, kwa yeyote kama apendavyo (1 Wakorintho 12:4-11). Wanaamini kwamba hakuna karama moja ambayo kila muumini anapaswa kuwa nayo (1 Wakorintho 12:29-30), na kwa hivyo karama ya lugha haithibitishi kitu chochote kuhusu muumini husika (1 Wakorintho 14:22), ingawa kila muumini ana Roho Mtakatifu (Warumi 8:9).

Maoni tofauti kuhusu karama ya lugha yanaweza kuwazuia waumini kushirikiana kwa karibu katika aina fulani za huduma, lakini waumini hawapaswi kuhukumiana kuhusu maoni yao juu ya suala hili.

## ROHO MTAKATIFU YUKO KATIKA UHUSIANO NA MUUMINI

Ikiwa uko katika uhusiano na Mungu, uko katika uhusiano na Roho Mtakatifu. Haiwezekani kujua nafsi moja tu ya Utatu wa Mungu. (Soma Waefeso 2:18; Yohana 6:44.)

Si lazima mtu aelewe kanuni ya Roho Mtakatifu kabla ya kuokoka. Wanafunzi hawakujua mengi kuhusu Roho, lakini Yesu aliwaambia kwamba wanamjua Roho na kwamba alikuwa pamoja nao tayari. (Soma Yohana 14:17.)

Kujua kanuni sahihi kuhusu Roho Mtakatifu hutusaidia kuhusiana naye kwa njia sahihi na humruhusu afanye mengi zaidi maishani mwetu. Kujua kwamba yeye ni mtu kunaturuhusu kujua kwamba tunaweza kuwa na uhusiano naye. Tunaweza kuzungumza naye, naye atazungumza nasi. Kwa kawaida haneni nasi kwa sauti inayosikika, lakini anatusaidia kuelewa mapenzi ya Mungu na upendo wa Mungu. Ikiwa kweli tunataka kufanya mapenzi ya Mungu, Roho Mtakatifu atatuongoza ingawa hatutahisi akifanya hivyo kila wakati.

Kujua kwamba yeye ni mtu kunamaanisha kwamba hatutatenda kana kwamba yeye ni nguvu au hisia fulani tu. Tunapomwabudu Mungu, tunafikiria yeye ni nani na jinsi alivyo, si kufurahia tu hisia fulani bila kutafakari. Tunapoomba, tunazungumza tukitumia akili na tunajaribu kuelewa kile anachoweza kutuonyesha badala ya kutumia maneno bila kufikiria, kwa njia ya kimazingaombwe, kama wanavyofanya watu wa dini nyingine.

Kujua kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu kunapaswa kutupatia mtazamo wa ibada yenye heshima kuu. Tunapoomba na kuhisi mwongozo wake, tunahitaji kukumbuka kwamba yeye ndiye Mungu anayetupenda, anatujua kikamilifu, na anajua mustakabali wetu. Yeye pia ndiye mwenye mamlaka ya juu zaidi, ambaye tunapaswa kumtii.

Yuko nasi wakati wote. Maandiko yanasema kwamba tunaishi katika Roho na tunapaswa kuenenda kwa Roho (Wagalatia 5:25). Tunapaswa kuishi kana kwamba tuko mbele zake, na tusifikiri kwamba tunakuja mbele zake kanisani tu. Hayuko pamoja nasi tu, bali pia anaishi ndani yetu. Hiyo ni sababu ya kutufanya tufahamu kwamba tunapaswa kuishi maisha safi na matakatifu. (Soma 1 Wakorintho 6:19.)

Ni lazima tukumbuke kwamba kipaumbele kikuu zaidi cha Roho ni kutupa ushindi dhidi ya dhambi na kutakasa mioyo yetu (Warumi 8:13; Wagalatia 5:16; Matendo 15:8-9). Hatupaswi kuomba kwa ajili ya mambo mengine ikiwa hatumruhusu atimize kipaumbele chake kikuu zaidi. Tunapaswa kuomba kwa imani, tukiamini kwamba atatufanya tuwe watakatifu kikamilifu. (Soma 1 Wathesalonike 5:23.)

Katika mapambano ya maisha, anatupa nguvu ya ndani (Waefeso 3:16). Anatuelewa, anaelewa hali zetu, na anaweza kutupa kile tunachohitaji.

Katika huduma, ni lazima tumtegemee ili atupe mwongozo, alipe nguvu Neno lake, na kutimiza matokeo ya kiroho katika mioyo ya wengine. Tunaona hayo katika kitabu cha Matendo. Hakuna uwezo wa kibinadamu unaoweza kuchukua nafasi ya kazi ya Roho.

Hata kama tayari umejazwa Roho, hupaswi kusahau kudumisha uhusiano naye. Amri ya kujazwa Roho ni amri ya kujazwa *wakati wote*. (Waefeso 5:18.) Tunahitaji kujazwa wakati wote, na hilo linatokea kupitia uhusiano wetu naye.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Roho Mtakatifu ni nafsi ya tatu ya Utatu wa Mungu, nafsi yenye uungu kikamilifu kama Baba na Mwana. Anasadikisha juu dhambi, anawezesha kuzaliwa upya na anaishi ndani ya kila muumini, akiwezesha ushidi dhidi ya dhambi na utakaso wa moyo. Yeye ndiye uhai unaounganisha kanisa, na hulibariki kanisa kwa tunda la Roho na karama za kiroho kwa ajili ya huduma.

## USHAHIDI WA BIBLIA KUHUSU UTU WA ROHO MTAKATIFU

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Sehemu hii ni ya hiari na inaweza kuzingatiwa ikiwa wanafunzi wanahisi kwamba wanahitaji ushahidi zaidi wa Biblia kuhusiana na hoja hii.*

Watu wengine wanakana utu wa Roho na husema yeye ni nguvu isiyo na utu kama umeme au nguvu ya uvutano. Hata hivyo, haiwezekani kwamba nguvu isiyo na utu ingeelezwa kama vile Biblia inavyomweleza Roho Mtakatifu. Umeme hauzungumzi wala haufikirii sababu; nguvu ya uvutano haiwezi kudanganywa. Nguvu isiyo na akili haiwezi kuelewa mapenzi ya Mungu.

Watu wengine husema kwamba maandiko yanatumia tamathali ya tashihisi, yakizungumza juu ya kitu kisicho na utu kana kwamba kina utu bila kumaanisha hivyo. Hata hivyo, maandiko yanazungumza juu ya Roho kwa kutumia maneno yanayoashiria utu, na watu walimwitikia kana kwamba ana utu. Katika sehemu chache, Roho anazungumziwa kitamathali kana kwamba yeye ni kitu, kwa mfano mahali ambapo Biblia inasema kwamba Roho atamwagwa (Matendo 2:17). Mifano hii inapaswa kuzingatiwa kuwa ya kitamathali kwani kwa kawaida Biblia huzungumza kuhusu Roho kama mtu mwenye utu.

Ushahidi wa Biblia wa uutu wa roho mtakatifu:

- Katika Mathayo 28:19, tunaambiwa tubatize kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ambayo inamaanisha kwamba wote watatu wana mamlaka.
- 2 Wakorintho 13:14 inataja ushirika wa Roho Mtakatifu, ambayo inamaanisha mawasiliano yanayotumia akili.
- Katika Marko 13:11, waumini waliahidiwa kwamba Roho Mtakatifu atanena kupitia kwao wakati wa mateso.
- Katika Yohana 14:17, 26, Roho Mtakatifu anaitwa Roho wa kweli atakayefundisha na kukumbusha.
- Katika Yohana 16:7-11, Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu atasadikisha ulimwengu juu ya dhambi, haki, na hukumu, ambayo inahitaji mawasiliano yanayotumia akili.
- Yohana 16:13-15 inasema kwamba Roho Mtakatifu hatanena kwa mamlaka yake mwenyewe, bali atatangaza mambo ya Kristo.
- Kulingana na 1 Wakorintho 12:11, Roho Mtakatifu huchagua jinsi karama za kiroho zinavyopaswa kutolewa.
- Anashuhudia roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu (Warumi 8:16).
- Yeye hutuombea kwa Baba na ana akili ambayo inaweza kuelewa mapenzi ya Mungu (Warumi 8:26-27).
- Kulingana na Waefeso 4:30, anaweza kuhuzunishwa, ambayo inamaanisha kwamba anaelewa miitikio yetu na ana hisia.
- Anaweza kudanganywa, ambayo inamaanisha kwamba anaelewa mawasiliano (Matendo 5:3).
- Yeye hunena, hutoa mwongozo, na ana mapenzi ambayo watu wanapaswa kufuata (Matendo 13:2-4).
- Aliwaongoza mitume katika safari zao za umisionari na wakati mwingine aliwaambia wasiende mahali fulani (Matendo 16:6).

## MAZOEZI YA SOMO LA 10

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Matendo 1:4-8
    - Warumi 8:1-14
    - 1 Wakorintho 2:9-16
    - 1 Wakorintho 12:1-13
    - Wagalatia 5:22-26

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 10. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 10

1. Orodhesha sifa tatu za mwitikio wa kanisa la awali kwa Roho Mtakatifu.

2. Je, tunajuaje kwamba Roho Mtakatifu ana utu?

3. Orodhesha njia tano ambazo kwazo tunajua kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu.

4. Orodhesha kazi tisa za Roho Mtakatifu.

5. Je, ni kipi kipaumbele cha juu zaidi cha Roho Mtakatifu katika kazi yake maishani mwetu?

## SOMO LA 11

# UTAKATIFU WA KIKRISTO

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Matumizi ya Biblia ya neno *takatifu.*
    - Utakatifu wa Mungu kama msingi wa utakatifu wa Kikristo.
    - Umuhimu wa utakatifu kwa ajili ya ibada na uhusiano na Mungu.
    - Mifano ya Biblia ya matukio ya utakaso.
    - Tabia za kufikia ukomavu wa kiroho.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu utakatifu wa Kikristo.

2. Mwanafunzi atakuwa na imani kwamba neema ya Mungu itamfanya awe mtakatifu katika ulimwengu wa sasa.

## NENO LA KIBIBLIA

Neno la Kiebrania lililotafsiriwa *utakatifu* au *utakaso* linatokea zaidi ya mara 600 katika Agano la Kale. Maneno ya Kiebrania na Kigiriki yanayotafsiriwa *takatifu* kimsingi yanamaanisha kutengwa, kujitolea kwa kusudi fulani. Kitu kilichotakaswa kinaacha kutumiwa kwa matumizi ya awali na kinatengwa kwa ajili ya kusudi jipya mahususi. Tazama vitu kadhaa ambavyo viliwekwa wakfu na kuchukuliwa kuwa vitakatifu katika Agano la Kale:

- **Uwanja Mtakatifu.** Mungu alitenga uwanja kama mahali pa kukutania na Musa (Kutoka 3:5).

- **Hema na Hekalu Takatifu.** Vitu vingi vitakatifu vilihusishwa na Hema la Kukutania na Hekalu, vikiwemo mavazi ya kuhani (Mambo ya Walawi 16:32), mkate (Kutoka 29:34), na samani (Kutoka 40:9). Vitu hivi vilitengwa kwa ajili ya kumwabudu Mungu.

- **Siku Takatifu.** Siku ya Sabato ilitengwa kama siku takatifu (Mwanzo 2:3; Kutoka 20:8). Sikukuu nyingine za Kiyahudi kama Siku ya Upatanisho pia zilikuwa maalum (Mambo ya Walawi 23:26-29). Siku hizi zilitengwa kwa ajili ya mapumziko, tafakari na ibada.

- **Mungu Mtakatifu.** Mfano mkuu zaidi wa utakatifu katika Biblia ni Mungu mwenyewe. Kila kitu kumhusu Mungu ni kitakatifu. Jina lake ni takatifu (Mambo ya Walawi 22:2); maneno yake ni matakatifu (Yeremia 23:9); njia zake ni takatifu (Zaburi 77:13). Utakatifu unamaanisha Mungu ametengwa kabisa na kitu chochote chenye dhambi, najisi, cha kawaida au kisichofaa kwa nafsi na nafasi yake ya kiungu

Katika Agano Jipya Yesu anatajwa kama mtakatifu (Yohana 17:19; Matendo 4:27, 30) na asiye na dhambi (2 Wakorintho 5:21). Malaika (Marko 8:38), mitume na manabii (Waefeso 3:5) wanaelezwa kama watakatifu. Wote hawa walitengwa kwa ajili ya kusudi maalum.

Biblia inawahamasisha watu wa Mungu kuwa watakatifu (Mambo ya Walawi 11:44-45; 1 Wakorintho 1:2; 1 Petro 1:15-16). Somo hili litaeleza utakatifu ambao Mungu anatarajia kutoka kwetu.

## WAABUDU MUNGU WATAKATIFU

» Someni Zaburi 119:33-40 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu jinsi Mungu anavyombadilisha muumini?

Mungu alipoanza kujifunua, kusudi lake la kwanza lilikuwa kuonyesha yeye ni Mungu wa aina gani. Mungu kimsingi alijieleza kama mtakatifu. Isaya mara nyingi alimtaja Mungu kama “Mtakatifu wa Israeli.”

Utakatifu wa Mungu ulikuwa mada ya ibada:

> Na walishukuru jina lake kuu la kuhofiwa; Ndiye mtakatifu. Mtukuzeni BWANA, Mungu wetu; Sujuduni penye kiti cha miguu yake; Ndiye mtakatifu (Zaburi 99:3, 5).

Utakatifu wa Mungu ndio msingi wa jinsi anavyotaka mwanadamu awe. Kwa sababu yeye ni mtakatifu, anawahamasisha wale wanaomwabudu wawe watakatifu. Alisema, “Iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu” (Mambo ya Walawi 11:44-45, Mambo ya Walawi 19:2, Mambo ya Walawi 20:26, Mambo ya Walawi 21:8).

Mungu wa Israeli alikuwa tofauti na miungu ya uongo ya wapagani na alihitaji aina tofauti ya ibada.

> Ni nani atakayepanda katika mlima wa BWANA? Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake? Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe, Asiyeiinua nafsi yake kwa ubatili, Wala hakuapa kwa hila (Zaburi 24:3-4).

Swali hapa ni, “Mungu anakubali ibada ya nani?” Si kila mtu anakubaliwa kama mwabudu Mungu. Waabudu Mungu lazima wawe watakatifu.

Utakatifu ambao Mungu anatarajia si tu wa sherehe au kujifanya; ni utakatifu halisi. Kiwango cha utakatifu kwa waabudu Mungu kinarudiwa katika Agano Jipya:

> Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (1 Petro 1:15-16).

*Mwenendo* unarejelea tabia na mtindo mzima wa maisha ya mtu. Mungu haombi tu kwamba wanaomwabudu wawe watakatifu kisherehe, au waitwe watakatifu wakati wao si watakatifu. Anatarajia wanaomwabudu waishi maisha matakatifu.

» Je, baadhi ya sababu zinazofanya utakatifu uhusishwe na ibada ni zipi?

Utakatifu ni muhimu kwa ibada kwa sababu

1. **Tunampenda Mungu na tunataka kuwa kama yeye**. Kumwabudu Mungu ni kuona kwamba yeye ndiye kiumbe wa ajabu zaidi aliyepo na kumpenda jinsi alivyo. Kuabudu ni kuthamini sifa za asili yake. Asili ya Mungu kimsingi ni takatifu, hivyo ikiwa tunapenda sana asili ya Mungu, tutachukia dhambi na uchafu, hata kama tunauona ndani yetu.

2. **Tunampenda Mungu na tunataka kumpendeza**. Takwa la Mungu halitushangazi ikiwa tunaelewa ibada ni nini hasa. Hatumuabudu kwa sababu ya hofu. Hatumuabudu kwa sababu tu anatubariki. Tunamwabudu kwa sababu tunampenda.

## UTAKASO WAKATI WA KUONGOKA

Biblia inatumia neno *utakaso* kurejelea kile ambacho kimetokea katika maisha ya kila muumini. Paulo aliandika "Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, **wale waliotakaswa katika Kristo Yesu**, walioitwa wawe watakatifu" (1 Wakorintho 1:2). Paulo aliandika, "…lakini mlioshwa, **lakini mlitakaswa**, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu." (1 Wakorintho 6:11). Wakorintho walikuwa tayari wametakaswa ingawa hawakuwa wamekomaa kiroho na walikuwa bado watu wa kimwili, kama watoto wachanga katika Kristo (1 Wakorintho 3:1).

> **"Mzee mmoja Mhindu alimuuliza Amy Carmichael, 'Tumesikia mahubiri mengi, je, unaweza kutuonyesha maisha ya Bwana wako Yesu?"**

Neno *takasa*, linaporejelea Wakorintho hao, linatumiwa katika maana yake ya jumla. Wakorintho walikuwa wameitwa kutoka katika dhambi na ulimwengu na walikuwa wametengwa kwa ajili ya Mungu. Hakika

hawakuwa wamekomaa katika utakaso, lakini walikuwa wametengwa na maisha ya zamani na sasa walikuwa sehemu ya familia ya Mungu.

Tunapokutana na Mungu kwa mara ya kwanza, dhambi ni kikwazo katika uhusiano wetu naye. Ndio maana uhusiano wetu na Mungu hauwezi kuanza hadi tutubu, tusamehewe, na tupewe moyo mpya.

Wakati huo huo tunapopatanishwa na Mungu, tunabadilishwa (Tito 3:5). Kiroho, tunafanywa viumbe wapya. Tunawekwa huru kutokana na nguvu za dhambi, na tunatamani kumpendeza Mungu. Utakatifu wa Kikristo huanza mtu anapookoka.

Biblia inatufundisha kwamba wokovu husababisha maisha matakatifu mara moja. Neema ya Mungu iletayo wokovu inatufundisha kuishi maisha ya kiasi, ya uadilifu, na utauwa katika nyakati hizi (Tito 2:11-12). Kusudi la wokovu ni kutuweka huru kutokana na dhambi na kutufanya tuwe watakatifu, ili tuweze kuishi katika uhusiano na Mungu (Luka 1:74-75, Warumi 6:2, 11-16).

## KUKUA KATIKA UTAKASO

Tunapoishi katika uhusiano na Mungu, tunaendelea kukua katika utakatifu kadiri tunavyozidi kuelewa ukweli wake. Kuenenda katika nuru kunamaanisha kuendelea kumtii Mungu kadiri tunavyozidi kujifunza ukweli wake (1 Yohana 1:7). Kadiri tunavyoelewa vyema zaidi kile kinachompendeza na kisichompendeza, tunabadilishwa na ukweli wake na nguvu ya Roho Mtakatifu.

Mtu anayempenda Mungu atatamani kuwa mtakatifu kabisa. Hataki kubadilisha matendo yake tu. Anataka nia zake ziwe safi kabisa. Daudi aliomba kwamba aweze kuishi kwa ushindi kamili dhidi ya dhambi, kisha akaomba kwamba maneno yake na hata mawazo ya moyo wake yampendeze Mungu. (Zaburi 19:12-14. Tazama pia Zaburi 119:7, 34, 36, 69, 80, na 112.)

Mchakato mzima wa kupata ukomavu wa kiroho unaitwa utakaso. Utakaso ni mchakato wa maisha yote wa kuzidi kutengwa na dhambi na dunia, na kujitoa zaidi kwa Mungu. Hili linadhihirishwa na onyo la Paulo dhidi ya kufuata mfano wa dunia na himizo lake kwamba "mgeuzwe [wakati wote] kwa kufanywa upya nia zenu" (Warumi 12:2). Kutengwa na dunia na mabadiliko ya nia si matukio yanayokamilishwa kwa wakati maalum katika maisha ya Mkristo. Muumini huendelea kukua kadiri anavyotembea na Bwana. Haya yote yamejumuishwa katika neno *utakaso*.

## UPOTOVU WA KURITHI NA UTAKASO

***Upotovu wa kurithi*** ni upotovu wa asili ya kimaadili ya mtu ambao unampa msukumo wa kutenda dhambi tangu anapozaliwa. Wanatheolojia wakati mwingine huuita "dhambi ya asili," kwa sababu ni asili yetu ya dhambi tunayozaliwa nayo kwa sababu ya dhambi ya Adamu.

Kila mtu huzaliwa na nia ambayo ni ya ubinafsi na yenye msukumo wa kutenda dhambi. Nia zetu hazina uhuru wa kuchagua kile kilicho sahihi isipokuwa Mungu atupe hamu na nguvu ya kufanya hivyo (Warumi 6:16-17). Upotovu wa kurithi huchochea dhambi za ndani kama vile kiburi, wivu, chuki, na kutosamehe. Pia huchochea matendo ya dhambi.

» Je, baada ya mtu kuokoka, bado ana upotovu wa kurithi?

Mtu ambaye ameokoka hayuko tena chini ya udhibiti wa upotovu wa kurithi. Kama bado angekuwa anadhibitiwa nao, angekuwa anaishi katika dhambi na hajaokoka. Biblia inatuambia kwamba mtu anayedhibitiwa na akili ya kimwili amehukumiwa (Warumi 8:6-8, 13). Mtu aliyeokoka hayuko chini ya udhibiti wa upotovu wa kurithi na anaweza kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Warumi 8:1, 9, 13).

Hata hivyo, mtu aliyeokoka bado ana ushawishi wa upotovu wa kurithi ndani yake hadi atakapotakaswa kutokana nao. Paulo aliwaambia waumini wa Korintho kwamba bado walikuwa watu wa kimwili na walikuwa na mitazamo kama ya watu wa dunia, ingawa walikuwa wameokolewa. (1 Wakorintho 3:1-3.) Isitoshe alidokeza kwamba ni jambo la kawaida kwa Mkristo mpya kuwa katika hali hiyo. Alisema kwamba kuwa na mtazamo wa kimwili ni kuwa kama mtoto mchanga katika Kristo.

Muumini aliye katika hali hiyo anampenda Mungu, lakini hawezi kumpenda Mungu kwa moyo wake wote, nafsi yake yote, akili yake yote na nguvu zake zote (Mathayo 22:37). Hawezi kusema, kama Paulo, kwamba ana nia moja ya kufuata wito wa Mungu (Wafilipi 3:13-15). Anajua kwamba baadhi ya tafakari za moyo wake hazikubaliki kwa Mungu (Zaburi 19:14).

Mungu hatuachi katika hali hiyo. Hata hapo zamani za kale Mungu aliahidi Israeli kwamba atafanya kazi ya neema ambayo itawafanya waweze kumpenda kwa mioyo yao yote. (Soma Kumbukumbu la Torati 30:6.)

Daudi aliomba kwa ajili ya kazi ya neema ambayo ni zaidi ya msamaha. Alikuwa ametenda dhambi na kutambua kwamba hilo lilitokea kwa sababu ya tatizo moyoni mwake. Alijua kwamba dhambi ilikuwa katika asili yake, lakini aliamini kwamba Mungu alimtaka awe mtakatifu kikamilifu. Aliomba kwa ajili ya utakaso kamili. (Soma Zaburi 51:5-10.)

Waumini wa Agano Jipya walihamasishwa kupitia tukio lingine maalum baada ya kuongoka. Waumini wa Thesalonike walikuwa mfano mzuri wa waumini ambao walikuwa wameikubali

> **“Utakaso si wazo langu la kile ninachotaka Mungu anifanyie; utakaso ni wazo la Mungu la kile anachotaka kunifanyia, na hana budi kuniweka katika mtazamo wa akili na roho ambapo kwa gharama yoyote ile nitamruhusu anitakase kikamilifu.”**
>
> **Oswald Chambers**

injili, wamejitenga na sanamu, wamevumilia mateso, walikuwa na furaha katika Roho Mtakatifu, na walikuwa wakingoja kurudi kwa Yesu (1 Wathesalonike 1:6-10). Lakini bado kuna kitu kilichokuwa kimekosekana katika imani yao. Halikuwa jambo litakalotolewa kwa muda mrefu au baada ya kifo, kwa sababu Paulo alisema kwamba linaweza kutokea wakati atakapowatembelea. (1 Wathesalonike 3:10.) Aliomba hivi:

> Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya. (1 Wathesalonike 5:23-24).

Paulo aliomba kwamba waumini hao watakaswe kikamilifu. Matokeo yake ni kwamba waumini watakuwa bila lawama katika mwili, nafsi, na roho wakati Bwana atakaporudi.

Wanafunzi wa Yesu walipitia kazi maalum ya neema siku ya Pentekoste. Tunajua kwamba walikuwa tayari wameokolewa kabla ya wakati huo, kwa sababu Yesu alisema kwamba wao si wa dunia, kwamba wao ni wake na wa Baba, na kwamba majina yao yameandikwa mbinguni (Yohana 15:3, Yohana 17:14; 9-10; Luka 10:20). Lakini walikuwa na ubinafsi na hawakuzingatia vipaumbele vya Mungu. Yesu aliwarekebisha tena na tena kwa ajili ya mitazamo yao yenye dhambi. (Soma Marko 9:33-34; Marko 10:35-41; Luka 9:54-55.)

Baada ya kufufuka kwa Yesu, kabla tu hajarudi mbinguni, aliwaambia wanafunzi wake kwamba watakuwa mashahidi wake ulimwenguni. Lakini aliwaambia kwamba ni lazima kwanza wabatizwe kwa Roho Mtakatifu. (Luka 24:49; Yohana 20:22; Matendo 1:2-5, 8.) Tayari alikuwa amewaambia mengi kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu, hasa katika Yohana 14-16.

Wanafunzi walijazwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste (Matendo 2:4). Ujazo huo ulibadilisha nia, vipaumbele na matendo yao. Katika matukio mengine yote ya Agano Jipya, wanafunzi walionyesha mitazamo na vipaumbele kama vya Kristo, ingawa bado walikuwa na kutoelewana na walifanya makosa. Nyaraka zilizoandikwa

**"Kanisa lina wajibu maradufu kuhusiana na ulimwengu unaotuzunguka. Kwa upande mmoja tunapaswa kuishi, kutumika na kushuhudia ulimwenguni. Kwa upande mwingine tunapaswa kuepuka kuchafuliwa na ulimwengu. Kwa hivyo hatutakiwi kutafuta kuhifadhi utakatifu wetu kwa kuukimbia ulimwengu wala kupoteza utakatifu wetu kwa kufuata ulimwengu."**

**John Stott**

na Petro na Yohana zinadhihirisha ujumbe na moyo wa Kristo. Ujazo wa Roho Mtakatifu uliwawezesha kumpenda Bwana Mungu wao kwa mioyo yao yote, kwa roho zao zote, kwa akili zao zote, na kwa nguvu zao zote na kuwapenda majirani wao kama nafsi zao (Mathayo 22:37-39). Kwa sababu walikuwa wamejitoa kikamilifu kwa Roho Mtakatifu, aliishi kupitia kwao, kama vile alivyoishi kupitia Kristo (Luka 4:1, 14, 18; Matendo 2:22).

Walimu wa Kikristo huzingatia mchakato wa utakaso, na wengine huzingatia tukio maalum. Matukio ya Pentekoste na ubatizo wa Roho Mtakatifu ni mfano wa watu wanaopitia tukio maalum la utakaso. Ukweli kwamba hali fulani inaweza kuwa kamili au mtu anaweza kuipitia kikamilifu inamaanisha kuwa hali hiyo inatokea katika wakati fulani. Ni muhimu kwamba tusiweke mipaka katika kile ambacho injili inaweza kufanya, hata katika dakika moja ya kuwa na imani na kujisalimisha kikamilifu (Warumi 12:1-2). Yote ambayo Yesu alitoa kupitia kifo na ufufuo wake yanapatikana na wote ambao:

1. Wanajichukulia kuwa wafu kwa dhambi pamoja na Yesu (Warumi 6:11)
2. Hawaruhusu dhambi itawale katika miili yao (Warumi 6:12)
3. Wanatoa miili yao kama vyombo vya haki (Warumi 6:13)

Katika historia, Wakristo wakuu wameshuhudia kuhusu nyakati ambapo waliingia katika maisha yaliyojazwa Roho na uhusiano wa kina zaidi na Mungu, wakiwemo wanaume na wanawake kama vile John Bunyan, Hudson Taylor, Dwight L. Moody, Sammy Morris, Oswald Chambers, Frances Ridley Havergal na Amy Carmichael.[15]

Ingawa ni muhimu kwamba tusiweke mipaka katika kile ambacho Mungu anaweza kufanya katika muda mfupi, ni muhimu pia  tusisahau kazi ya Roho Mtakatifu kupitia michakato. Ingawa aina hii ya utakaso wakati mwingine huelezwa kuwa kamili, kiwango hiki hakimaanishi kwamba hakuwezi kuwa na ukuaji zaidi. Kwa mfano, baada ya kujifunza kuzungumza Kifaransa haimaanishi kwamba mtu hawezi kuendelea kujifunza kuzungumza Kifaransa kwa njia bora zaidi. Wale ambao wametakaswa kikamilifu wamewahi kufikia mahali ambapo walipitia utakaso ambao hawakuwa wameupitia hapo awali. Hata hivyo, hiyo si hali ya kuwa kamili. Ni maisha ya utakatifu ambapo muumini anaendelea kukua.

## UTAKASO NA UKOMAVU WA KIKRISTO

Biblia inaeleza maisha ya muumini aliyekomaa. Roho Mtakatifu hufanya kazi katika maisha ya muumini ili kukuza sifa za Kikristo. Kazi ya Roho inajumuisha nyakati maalum za utakaso au upako na pia michakato inayotendeka hatua kwa hatua. Muumini hatakiwi kuridhika na maisha ya kiroho ambayo hayalingani na maelezo ya Biblia kuhusu muumini aliyekomaa.

---

15 Unaweza kusoma  simulizi hizo katika kozi inayoitwa *Kanuni na Tabia za Maisha Matakatifu* ya Darasa la Kimataifa la Wachungaji.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alisema kwamba baadhi ya wasomaji wake walikuwa bado kama watoto (Waebrania 5:12). Aliwahimiza kuacha kanuni za kimsingi za Kristo na kuendelea hadi kufikia **ukomavu** (Waebrania 6:1).

Maombi ya mitume kwa ajili ya waumini yanatuonyesha mapenzi ya Mungu kwa ajili yetu.

## Upendo

Paulo aliomba akisema, "Bwana na **awaongeze na kuwazidisha katika upendo**, ninyi kwa ninyi, na kwa watu wote…" (1 Wathesalonike 3:12-13). Pia aliwaombea Waefeso akisema:

> Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani **mkiwa na shina na msingi katika upendo**, ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na **kuujua upendo wake Kristo**, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu (Waefeso 3:17-19).

Paulo alikuwa anaomba kwamba waumini hao wawe na upendo zaidi. Katika 1 Wakorintho 13, Paulo alieleza jinsi upendo huo unapaswa kuonekana katika muumini aliyekomaa. Maisha ya utakaso ni kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote, na nguvu zako zote na kumpenda jirani yako kama nafsi yako (Luka 10:27). Hiyo ndio aina ya uhusiano walio nao watu watakatifu na Mungu na wanadamu wenzao.

## Kutokuwa na Lawama

Paulo aliwaombea Wathesalonike, kwamba Mungu aifanye mioyo yao **iwe bila lawama katika utakatifu** (1 Wathesalonike 3:12-13). Sura mbili baadaye, anaomba kwamba watakaswe ili roho, nafsi na miili yao ihifadhiwe **bila lawama** wakati wa kuja kwake Bwana Yesu Kristo (1 Wathesalonike 5:23). *Kutokuwa na lawama* hakumaanishi ukamilifu katika kila njia. Mtu asiye na lawama hufanya makosa lakini ana tabia anayopaswa kuwa nayo.

## Nguvu ya Ndani

Paulo aliomba kwamba waumini wa Efeso **wafanywe imara kwa nguvu** katika utu wao wa ndani kupitia Roho wa Mungu (Waefeso 3:15-16). Tabia ya ndani inakuwa na nguvu kadiri mtu anavyozidi kuwa na imani. Nguvu ya ndani ni uwezo wa kufanya maamuzi sahihi na kukataa maamuzi mabaya.

## Kristo Akikaa Ndani Yetu

Paulo aliendelea na maombi kwa ajili ya Waefeso kwa kuomba kwamba **Kristo akae ndani ya mioyo yao** (Waefeso 3:17). Neno lililotafsiriwa "akae" katika kifungu hiki linamaanisha kukaa kwa kudumu si tu kukaa kwa muda mahali fulani. Usemi huu wa mfano unaonyesha

kwamba Yesu anataka kuishi nasi si kutembelea tu. Kristo huhisi kuridhika na wale wanaoishi maisha thabiti ya kiroho.

## Utimilifu wa Mungu

Paulo anatamatisha sehemu ya maombi ya sala yake kwa ajili ya Waefeso kwa kuomba kwamba **wajazwe utimilifu wote wa Mungu** (Waefeso 3:14-19). Hii ni kutumia mfano wa kimwili kuelezea ukweli wa kiroho. Inamaanisha kwamba Mungu anataka kudhibiti kikamilifu sehemu zetu zote; akili, nia, hisia, shughuli, mitazamo, matamanio, na miitikio yetu. Kati ya maelezo yote ya maisha matakatifu yanayopatikana katika Biblia, huenda haya ndio makuu zaidi—kujazwa na utauwa kiasi kwamba upotovu wowote usipatikane kwako.

Mistari miwili inayofuata inahitimisha sala hii:

> Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina (Waefeso 3:20-21).

Tamko hili la baraka linasema kwamba Mungu anaweza kufanya zaidi ya vile tunavyoweza kuomba au kufikiria. Paulo hazungumzi kuhusu kuwa na fedha nyingi bali kuhusu maisha ya kiroho. Hatupaswi kudharau viwango vya utakatifu na ukomavu ambavyo nguvu inayofanya kazi ndani yetu inaweza kutusaidia kufikia.

> **"Neema duni ni neema [ya kujibunia] tunayojitolea sisi wenyewe. Neema duni ni kuhubiri msamaha bila kuhitaji toba, ubatizo bila nidhamu ya kanisa, Meza ya Bwana bila maungamo... Neema duni ni neema bila uanafunzi, neema bila msalaba, neema bila Yesu Kristo, aishiye na aliyefanyika mwili."**
>
> **Dietrich Bonhoeffer**

## TABIA ZA KIKRISTO

Agano Jipya linatupatia tabia za kutuwezesha kupiga hatua katika utakatifu na ukomavu.

**Dumisha dhamiri njema**. Paulo anamwarifu Timotheo kwamba njia ya kupigana vita vilivyo vyema (mfano wa maisha ya Kikristo yenye ushindi), ni kwa kuwa na imani na dhamiri njema (1 Timotheo 1:18-19).[16] Paulo pia alisema, "Nami ninajizoeza katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu

16 Paulo alitaka sana kwamba wachungaji wawe na dhamiri safi kwa sababu alisisitiza suala hili mara tatu zaidi katika nyaraka zake za kichungaji kwa Mchungaji Timotheo, ikiwemo "dhamiri njema" (1 Timotheo 1:5) na "dhamiri safi." (1 Timotheo 3:8-9; 2 Timotheo 1:3).

siku zote" (Matendo 24:16). Kusikiliza dhamiri zetu kunaweza kutufanya tutubu, tutoe fidia, tupatanishwe na mtu fulani, au tubadili tabia zetu. Kuwa na dhamiri njema kunamaanisha kwamba watu watakirir dhambi na kuzitubu wakati wowote wanapotambua kwamba wamefanya makosa.

**Jitoe kwa Mungu**. Katika himizo lenye nguvu katika Warumi 12:1, Paulo anaandika, "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, **itoeni miili yenu** iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana." Waumini wa Rumi walikuwa tayari wamejitoa kwa Mungu walipoongoka. Hata hivyo, hapa Paulo anahimiza kujitoa kwa Mungu kikamilifu zaidi.

**Usifuate namna ya dunia** (Warumi 12:2). Kufuata namna ya dunia ni kushawishiwa na mtazamo wa jamii ya wasioamini, hadi kufikia hatua ya kukubali maadili yake na kuwa na tabia kama za wasioamini. Watu wa kidunia hupata sababu za kuhalalisha mtazamo wa kuwa na ubinafsi, kutozingatia haki na kutimiza tamaa za mwili kwa njia za dhambi. Muumini yuko tofauti (2 Wakorintho 10:3-4).

**Fanya upya nia yako**. Paulo anaendeleza himizo kwa Warumi kwa kusema,

> … bali mgeuzwe kwa **kufanywa upya nia zenu**, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu (Warumi 12:2).

Kadiri mtu anavyozidi kukataa mtazamo wa dunia na kukumbatia mtazamo wa Mungu, ndivyo atakavyozidi kubadilika.

**Enenda katika nuru**. Yohana aliandika, "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7). Nuru ni tamathali ya usemi inayowakilisha ukweli. Hivyo, kuenenda katika nuru kunamaanisha kuendelea kujifunza ukweli na kuufuata.

**Vumilia mateso kwa imani**. Tamko la baraka la Petro katika 1 Petro 5:10 linaashiria lengo tukufu la kuwa muumini aliyerejeshwa, mwenye nguvu, na aliye imara, lakini inaeleza njia isiyopendeza ya kufikia hali hiyo. "**Mkiisha kuteswa kwa muda kidogo**, yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu" (1 Petro 5:10). Mateso hutakasa mitazamo yetu na kurekebisha tabia zetu. Mungu huruhusu mateso yanayotujenga. Ni lazima tuyakubali na tujaribu kujifunza kile ambacho Mungu anatufundisha (2 Wakorintho 12:7-10).

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Utakatifu wa Kikristo huanza wakati mwenye dhambi anapotubu na kubadilishwa na neema ya Mungu. Muumini huyo anakua kiroho kadiri anavyozidi kukua katika uelewa wake wa mapenzi ya Mungu na kuendelea kutii. Utakaso ni kazi ya Mungu ambapo anamtakasa muumini na kumwezesha kuwa na tabia takatifu na maisha matakatifu.

## MAZOEZI YA SOMO LA 11

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Isaya 6:1-8
    - Matendo 2:1-18
    - 1 Wakorintho 10:1-13
    - 1 Wathesalonike 5:14-24
    - Tito 2:11-14

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 11. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 11

1. Je, ni nini maana ya msingi ya neno *takatifu*?
2. Je, inamaanisha nini Mungu kuwa mtakatifu?
3. Je, kwa nini utakatifu ni muhimu kwa ibada?
4. Je, utakatifu wa Kikristo huanza wakati gani?
5. Je, inamaanisha nini kuenenda katika nuru?
6. Je, ni nini kinatokea kwa muumini wakati wa mchakato wa utakaso wa maisha yote?
7. Je, upotovu wa kurithi ni nini?
8. Je, muumini anawezaje kukosa lawama katika mwili, nafsi na roho wakati Bwana atakaporudi?

## SOMO LA 12

# KANISA

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Asili ya kanisa.
    - Kanisa kama taasisi iliyo hai.
    - Kanisa kama kutaniko lililo hai la kieneo.
    - Msingi wa umoja wa kanisa la dunia nzima.
    - Msingi wa umoja wa kanisa la kieneo.
    - Sakramenti za kanisa.
    - Malengo ya kanisa.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu kanisa.

2. Mwanafunzi ataona wajibu wake wa kujitolea katika kanisa la eneo lake.

## ASILI YA KANISA

» Someni Waefeso 3:3-10 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu kanisa?

Katika kipindi cha karne zilizotangulia Agano Jipya, kanisa lilikuwa fumbo ambalo halikuwa limefunuliwa kikamilifu. Kulikuwa na watu waliopata neema ya Mungu na wakaishi katika uhusiano naye (Warumi 4:1-8), lakini kanisa lilikuwa bado halijaanzishwa.

» Kanisa lilianza wakati gani?

Kanisa lilianza na maisha na huduma ya Yesu. Kanisa lilijengwa kwenye msingi wa wokovu aliotoa (Mathayo 16:16-18). Enzi ya kanisa ilianza Siku ya Pentekoste. Kuanzia siku hiyo, kanisa limekuwa likifanya kazi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, bila uongozi wa kimwili na unaoonekana wa Kristo duniani (Yohana 16:7).

Yesu aliwapa wanafunzi wake mamlaka ya kueneza na kuanzisha kanuni zake kote duniani (Mathayo 28:18-20) na aliahidi kwamba Roho Mtakatifu atawaongoza kwenye kweli yote (Yohana 16:13). Kanisa linaweza kuitwa la kitume kwa sababu mafundisho ya mitume ndio kanuni za msingi za kanisa. Kanuni zozote zinazopingana na kanuni hizo za msingi hazipaswi kuitwa za Kikristo.

Kanisa lilianza kutokana na:

1. Huduma ya Yesu
2. Wokovu uliotolewa na Kristo
3. Tukio lililotokea Siku ya Pentekoste
4. Ukuzaji wa kanuni za kitume

## KANISA KAMA TAASISI ILIYO HAI

Kanisa linalinganishwa na familia ambapo Mungu ni Baba na waumini ni kaka na dada (Mathayo 12:48-50, Wakolosai 1:2). Kanisa linaitwa taifa ambalo halina kabila moja wala asili ya kawaida (1 Petro 2:9-10). Kanisa linalinganishwa na mwili, ambao Kristo ndiye kichwa chake (Waefeso 4:15-16, Waefeso 5:30). Washiriki wa mwili huo wanafanya kazi pamoja na kujaliana (1 Wakorintho 12:14, 26).

Kama mshiriki wa mwili, Mkristo lazima asiwe na mtazamo wa kujitegemea bila kanisa. Anahitaji washiriki wengine, nao wanamhitaji (1 Wakorintho 12:21). Ni makosa kwa Mkristo kuishi kana kwamba anaweza kujitosheleza mwenye  kiroho bila kanisa.

Kujitenga na kanisa ni kujitenga na kile ambacho Kristo anafanya duniani. Kutoheshimu na kutopenda kanisa ni kutomheshimu na kutompenda Kristo.

## KANISA KAMA KUTANIKO LILILO HAI LA KIENEO

Kuna kanisa moja la dunia nzima, hata hivyo pia kuna kanisa la kieneo. Washiriki wa mwili hawawezi kufanya kazi isipokuwa wawe pamoja mahali pamoja. Paulo aliwaandikia waumini wa Korintho akiwaambia kwamba wao ni mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:27), ambayo ina maana kwamba kanisa la kieneo ni mwili wa Kristo mahali hapo.

Mungu ameunda kanisa la kieneo kuwa familia ya imani:

1. Likifanya kazi kama mwili wenye karama za kiroho

2. Likikidhi mahitaji mbalimbali ya wale walio katika ushirika (kupitia rasilimali za kibinadamu na za kiungu)

3. Likionyesha ulimwengu hekima ya Mungu katika kila nyanja ya maisha

4. Likiwaalika wasioamni waongoke na kuingia katika familia

Ushirika wa kweli unajumuisha uchumi kwa sababu wale walio katika ushirika wanashiriki maisha pamoja na kuyajali mahitaji ya wengine (Yakobo 2:15-16, Yakobo 1:27). Hitaji la kaka au dada katika Kristo ni jukumu la kanisa ikiwa mshiriki huyo anashiriki katika maisha ya kanisa na anachukua majukumu kadiri anavyoweza.

Mungu hutoa karama za kiroho na miito maalum kwa ajili ya huduma ili kuimarisha na kujenga kanisa la kieneo (Waefeso 4:11-12).

Kanisa la kieneo hutumikia jamii inayoizunguka. Kipaumbele cha kwanza ni cha kiroho, kuhubiri injili na kukuza ukweli wa Mungu katika masuala yote. Kanisa hukidhi mahitaji ya kimwili katika jamii lakini huwapa kipaumbele watu walio katika ushirika wa kiroho wa kanisa (Wagalatia 6:10).

## UKAMILIFU WA KANISA

Yesu alijitoa kwa ajili ya kanisa, ili kulifanya liwe takatifu na bila dosari yoyote (Waefeso 5:27). Kanisa halipaswi kamwe kuvumilia dhambi, ingawa lazima liwe tayari kusamehe. Viongozi lazima wawe mifano ya maisha matakatifu (1 Timotheo 3:2-3). Mshirika wa kanisa akitenda dhambi, lazima akabiliwe na hatimaye kuondolewa katika ushirika ikiwa hatatubu (1 Wakorintho 5:11-13).

» Kwa nini kanisa si kamilifu?

Watu wa kanisa hawatakuwa wakamilifu katika kila njia. Kwa sababu kanisa linahubiri Injili, kuna watu katika kutaniko ambao bado hawajatubu dhambi. Hata kati ya wale ambao wameokoka, kutakuwa na mapungufu katika maisha yao kwa sababu bado hawaelewi jinsi ya kutumia ukweli katika mambo yote ya maisha yao. Hata miongoni mwa Wakristo waliokomaa, kunaweza kuwa na mapungufu na mitazamo isiyofaa kwa sababu hata Mkristo aliyekomaa bado yuko katika mchakato wa kukua kiroho. Ni sehemu ya kazi ya kanisa kuendelea kufundisha na kutumia Neno la Mungu, likiwawezesha watu kukomaa kiroho (Waefeso 4:11-16; 2 Timotheo 3:16-17).

## KUFAFANUA KANISA

**Kanisa la dunia nzima linajumuisha waumini wote wa nyakati zote na mahali pote.** Wakati mwingine linaitwa kanisa lisiloonekana kwa sababu hakuna shirika la kidunia ambalo linasimamia kanisa la dunia nzima au lenye orodha ya washiriki wake.

**Kanisa la kieneo ni jamii ya waumini katika sehemu moja ambao kwa pamoja wanafanya kazi ya mwili wa Kristo.** Kikundi si kanisa ikiwa kimeundwa kwa ajili ya kusudi finyu zaidi.

Huu hapa ni ufafanuzi wa kina zaidi wa kanisa la kieneo ambao unalitofautisha na aina nyingine za vikundi: "Kikundi la waumini waliobatizwa [wameungana] pamoja kwa ajili ya ibada, kujengana, huduma, ushirika, na kuwafikia wengine; kukubali uongozi wa kiroho; tayari kuhudumia makundi yote ya jamii kupitia karama mbalimbali katika mwili; na kutekeleza desturi za kanisa mara kwa mara".[17]

## UMOJA WA KANISA LA DUNIA NZIMA

Kuna kanisa moja la mahali pote na nyakati zote. Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu," si "makanisa." Mtume Paulo aliandika kwamba kuna mwili mmoja, na Roho mmoja, na tumaini moja, kama vile kuna Bwana mmoja, imani moja na ubatizo mmoja (Waefeso 4:4-6).

Kanuni za imani za Kikristo za kale zilirejelea "kanisa katoliki." Hilo halikurejelea Kanisa Katoliki la Roma, bali kanisa la dunia nzima linalojumuisha Wakristo wote wa kweli.

Msingi wa umoja wa kanisa la dunia nzima hauko katika kuwa shirika moja, chini ya utawala mkuu mmoja. Hilo halitatokea kamwe kabla ya kurudi kwa Kristo. Watu wengine wanatamani jambo hilo litokee, lakini linaonekana si mapenzi ya Mungu kwa sababu Yesu aliwasahihisha wanafunzi walipofikiri kwamba mtu hapaswi kufanya huduma nje ya shirika lake (Luka 9:49-50). Ikiwa Yesu angetaka kuwa na utawala mkuu juu ya kanisa la dunia nzima, angebaki duniani kimwili ili kuliongoza. Hata hivyo, Yesu aliona kwamba kazi mbalimbali za Roho Mtakatifu kote ulimwenguni hazingefanyika kama inavyopaswa ikiwa Yesu angebaki duniani kimwili (Yohana 16:7).

» Je, msingi wa umoja wa kanisa la dunia nzima ni upi?

Msingi wa umoja wa kanisa la dunia nzima ni

1. Kanuni za mitume
2. Uhusiano na Kristo unaobadilisha maisha

> **"Ikiwa moyo wako uko sawa na moyo wangu, kama wangu ulivyo sawa na moyo wako, basi nipende kwa upendo mwororo, kama rafiki aliye karibu zaidi kuliko ndugu; kama ndugu katika Kristo, raia mwenzako wa Yerusalemu Mpya, askari mwenzako anayepigana vita vile vile kama wewe, chini ya Jemedari yule yule wa wokovu wetu. Nipende kama mwenzako katika ufalme na katika kuvumilia kwa subira kama Yesu, na mrithi wa utukufu wake pamoja nawe."**
>
> **John Wesley**
>
> Imefupishwa kutoka katika mahubiri yanayoitwa "Roho ya Kikatoliki"

17 David Dockery, *Southern Baptist Consensus and Renewal: A Biblical, Historical, and Theological Proposal* (Nashville: B&H Publishing Group, 2008), 127

Umoja wa kikanuni haumaanishi kwamba Wakristo wanakubaliana kuhusu kila kitu, hata kuhusu kanuni zote muhimu. Unamaanisha kwamba wanakubaliana kuhusu kanuni za msingi juu ya asili ya Mungu na Kristo na mambo ya kimsingi juu ya injili. Bila hayo, wasingekuwa wanamwabudu Mungu yule yule au kuishi chini ya neema yake.

Kanuni si kitu pekee kinachohitajika kwa ajili ya umoja wa Kikristo. Wakristo wanashiriki uhusiano wa karibu kati yao kwa sababu ya uhusiano wao na Kristo unaobadilisha maisha. Kwa sababu wametubu dhambi, wameweka imani yao katika Kristo na wana Roho Mtakatifu, wana uhusiano maalum. Wakristo hutambuana kote ulimwenguni licha ya kuwa tofauti kwa njia nyingi.

> **"Nimefikia hatua ya kuamini kwamba alama ya mtu mwenye moyo uliotakaswa kweli ni kwamba anajali zaidi wokovu wa mwingine kuliko jinsi unavyojali ustawi wake mwenyewe."**
>
> **Dennis Kinlaw**

## UMOJA WA KANISA LA KIENEO

Tunaweza kumkubali kama Mkristo mtu yeyote anayeamini kanuni za msingi na anayeonekana kuwa katika uhusiano na Kristo unaobadilisha maisha. Lakini makubaliano ya kikanuni ya kanisa la kieneo lazima yawe ya kina zaidi.

Kanisa la kieneo ni kikundi cha watu ambao wamejitolea kuabudu pamoja, kufanya uinjilisti, kuwafundisha waongofu na vijana kuwa wanafunzi, kutumikia jamii, na kufundisha masuala ya kiutendaji ya maisha ya Kikristo. Ili watu watimize kusudi hilo pamoja, ni lazima wakubaliane kuhusu mambo mengi ya kikanuni.

Kwa mfano, labda mtu katika kanisa la kieneo anawaambia vijana wote na waongofu wote wapya waombe kwa ajili ya kupokea karama ya kunena kwa lugha. Lakini viongozi wengine katika kanisa hilo hawaamini kwamba kila muumini ameahidiwa karama ya kunena kwa lugha. Wana wasiwasi kwamba watu wataingia katika mkanganyo wa kiroho ikiwa watajaribu kupata kitu ambacho si mapenzi ya Mungu. Ni dhahiri kwamba itakuwa vigumu watu hao kufanya kazi pamoja katika kanisa la kieneo. Hata kama viongozi wanamchukulia mtu huyo kuwa muumini, hawapaswi kumruhusu kufundisha kanuni zinazoweza kuleta mkanganyo katika kutaniko hilo.

Kanisa la kieneo linahitaji kukubaliana kuhusu kanuni zinazoathiri jinsi wanavyoshiriki maisha pamoja na kufanya huduma. Ni vizuri kanisa kuwa na taarifa iliyoandikwa ya kanuni wanazoshiriki. Kauli hiyo haitumiwi kubaini iwapo mtu fulani ni muumini. Badala yake, inaonyesha ni kanuni gani zinaunganisha kikundi hicho cha waumini kwa ajili ya ibada na huduma ya mara kwa mara yenye umoja.

## SAKRAMENTI ZA KANISA



Yesu alitoa sakramenti mbili kwa kanisa. Wanaweza pia kuitwa desturi au sherehe.

**Ubatizo** ni ishara ya kifo na ufufuo wa Kristo (Warumi 6:3-4). Ubatizo ni ushuhuda kwamba muumini anajitambulisha na Kristo na amekuwa mfu kwa dhambi na akapata maisha mapya katika Kristo. Ubatizo haumwokoi mtu. Ubatizo ni ushuhuda wa hadharani kwamba uongofu umetokea (Yohana 3:7-8).

**Meza ya Bwana** ilianzishwa na Yesu kwenye mlo wake wa mwisho pamoja na wanafunzi kabla ya kusulubiwa kwake (1 Wakorintho 11:23-25). Mkate na divai vinawakilisha mwili na damu ya Yesu iliyotolewa kama dhabihu kwa ajili ya wokovu wetu. [18] Kama vile tunavyokula chakula kwa ajili ya uhai wa kimwili, tunategemea dhabihu yake kwa ajili ya uhai wetu wa kiroho (Yohana 6:53-58).

Sakramenti zinaweza kuitwa "njia za kupata neema." Hazitoi neema ikiwa zinafanywa bila imani na utiifu. Ni desturi ambazo Mungu ametupatia, na zikifanywa kwa imani, ni njia za kupokea neema kutoka kwa Mungu.

» Je, baadhi ya makusudi ya kanisa ni yapi?

## BAADHI YA MAKUSUDI YA KANISA LA KIENEO YANAYOPATIKANA KATIKA AGANO JIPYA

Kanisa linapaswa:

1. Kufanya kazi ya uinjilisti (Mathayo 28:18-20)
2. Kuabudu kama kutaniko (1 Wakorintho 14:26)
3. Kudumisha kanuni (1 Timotheo 3:15; Yuda 1:3)
4. Kuwasaidia wachungaji kifedha (1 Timotheo 5:17-18)
5. Kutuma na kuwasaidia mamisionari (Matendo 13:2-4; Warumi 15:24)
6. Kuwasaidia washirika wenye mahitaji (Warumi 12:13; 1 Timotheo 5:3)
7. Kuwatia nidhamu washirika wanaoanguka katika dhambi (1 Wakorintho 5:9-13)
8. Kutekeleza ubatizo na Meza ya Bwana (Mathayo 28:19; 1 Wakorintho 11:23-26)
9. Kuwafunza waumini hadi wafikie ukomavu (Waefeso 4:12-13)
10. Kuhudumia mahitaji ya jamii (Wagalatia 6:10; Waefeso 4:28; Waebrania 13:16)

---

18 Picha: "Meza ya Bwana" iliyopigwa na Allison Estabrook mnamo Oktoba 14, 2022, ilitolewa kutoka kwenye https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52476662295/, iliyoidhinishwa chini ya CC BY 4.0.

Mengi ya mambo haya hayawezi kutekelezwa na mtu mmoja anayefanya kazi peke yake. Makusudi haya yanategemea ushirikiano katika kikundi cha waumini na mfumo wa uongozi.

Mungu anahamasisha kila muumini kujitolea katika kanisa la kieneo na kusaidia kanisa hilo kutimiza kusudi lake ulimwenguni. Mshirika asipotumika kanisani, hatimizi kusudi lake kama sehemu ya mwili wa Kristo.

## MAKOSA YA KUEPUKA: UBINAFSI WA KIROHO

*Kidokezo kwa kiongozi wa darasa: Mshiriki wa darasa anaweza kueleza sehemu hii.*

Baadhi ya watu hawajitolei kamwe kuwa sehemu ya kanisa la kieneo. Wanataka kujihisi kuwa wako huru kuhudhuria kanisa lolote Jumapili yoyote. Hawawezi kusaidia katika huduma yoyote ya kanisa kwa sababu kanisa haliwezi kuwategemea. Hawana mahusiano yanayoruhusu ushirika wa kiroho na uwajibikaji. Ikiwa Wakristo wote wangefanya hivyo, kusingekuwa na makanisa.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

> **“Siamini kwamba Mungu anataka maisha yetu katika kanisa yazingatie majengo na huduma. Badala yake, Mungu anataka makanisa yetu—haijalishi makutaniko yetu yanachukua muundo gani—yazingatie uanafunzi hai, utume, na kutafuta umoja.”**
>
> **Francis Chan**

### KAULI YA IMANI

Kristo amejenga kanisa moja takatifu, la dunia nzima, linalodhihirishwa kama mwili wa Kristo katika makutaniko ya kieneo. Kanisa linashikilia kanuni za mitume na kutetea ukweli wote. Kanisa ni familia ya Mungu, yenye ushirika unaohudumia mahitaji yote. Kanisa linamwabudu Mungu, linaeneza injili ulimwenguni, na kuwafunza waumini.

## MAZOEZI YA SOMO LA 12

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - 1 Wakorintho 5:1-13
    - 1 Wakorintho 6:1-8
    - 1 Wakorintho 12:14-31
    - Waefeso 4:11-16
    - Yakobo 2:1-9

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 12. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 12

1. Je, enzi ya kanisa ilianza wakati gani?
2. Je, kwa nini kanisa linaweza kuitwa la kitume?
3. Je, vipengele vinne vya asili ya kanisa ni vipi?
4. Je, kanisa la dunia nzima ni akina nani?
5. Je, kanisa la kieneo ni nini?
6. Je, neno *kanisa katoliki* lilimaanisha nini hapo awali?
7. Je, kanisa la dunia nzima limeunganishwa na mambo gani mawili?
8. Je, kwa nini ni vizuri kwa kanisa kuwa na taarifa iliyoandikwa ya kanuni wanazoshiriki?
9. Orodhesha makusudi sita ya kanisa la kieneo.

## SOMO LA 13

# HATIMA YA MILELE

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Shughuli kuu ya mbinguni.
    - Sifa za mbinguni zilizofunuliwa katika maandiko.
    - Sifa za adhabu ya milele zilizofunuliwa katika maandiko.
    - Baadhi ya dini zinazokana ukweli wa adhabu ya milele.
    - Haki ya adhabu ya milele.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu hatima ya milele.

2. Mwanafunzi atakumbuka kwamba kuna matendo yenye matokeo ya milele ambayo hayatabadilika kamwe.

## SEHEMU YA 1: HATIMA YA MILELE YA WAUMINI

» Someni Ufunuo 21 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu mustakabali wa waumini?

Uumbaji wote upo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, lakini mbinguni ndio kitovu cha ulimwengu, mahali ambapo Mungu anaabudiwa kwa kiwango cha juu zaidi na viumbe alioumba kwa mfano wake. (Soma Ufunuo 5:11-14.) Utukufu wa Mungu utafunuliwa mbinguni kikamilifu kiasi kwamba mahali hapo patakuwa nuru ya mji (Ufunuo 21:23). Ni mahali ambapo tutamjua Mungu kikamilifu kiasi kwamba tutauona uso wake (Ufunuo 22:4).

Mbinguni, waumini watapata furaha kamili katika kumwabudu Mungu. Zaburi 16:11 inasema, "Mbele za uso wako ziko furaha tele; na katika mkono wako wa kuume mna mema ya milele." Inafaa kwamba furaha na ibada vinahusiana. Mungu alituumba kwa mfano wake, ili tuweze kuelewa asili yake vya kutosha kiasi kwamba tuweze kumwabudu jinsi alivyo. Tumepewa hisia, uwezo wa kupenda, na akili ili tuweze kumwabudu Mungu.

Yesu alitoa kauli hizi kwa wanafunzi wake:

> Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo (Yohana 14:1-3).

Maneno ya Yesu yanatuambia mambo fulani kuhusu mbinguni. Jambo muhimu zaidi ni kwamba mbinguni ni makao ya Mungu. Yesu alisema ni nyumba ya Baba yake. Jambo lingine muhimu ni kwamba siku moja tutaweza kuishi huko pamoja na Mungu.

Ahadi ya kuishi mbinguni inapaswa kuongoza jinsi tunavyoishi duniani. Mtu anayeishi kwa msingi wa maadili ya milele atafanya mema zaidi duniani. Mtu anayetarajia thawabu ya mbinguni ana motisha ya kuvumilia hali ngumu na kujitahidi kutimiza mapenzi ya Mungu. Yesu anawaambia wale wanaoteseka, "Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni" (Mathayo 5:12).

## Sifa za Mbinguni

» Je, baadhi ya mambo tunayojua kuhusu mbinguni ni yapi?

Wakati mwingine watu duniani hawawezi kununua nyumba wanayotaka, au hawawezi kuifanya nyumba yao iwe kama wanavyotaka iwe. Lakini Mungu ana uwezo na rasilimali zisizo na kikomo, hivyo tunajua kwamba nyumba yake iko jinsi anavyotaka iwe. Kwa hivyo, mbinguni panalingana kikamilifu na asili ya Mungu.

Hakutakuwa na dhambi mbinguni. Viumbe wote mbinguni, iwe ni malaika au wanadamu au viumbe wengine, watakuwa watakatifu kikamilifu. (Soma Ufunuo 21:8, 27.)

Mbinguni patakuwa huru kutokana na matokeo yote ya dhambi, ikiwa ni pamoja na uchungu, huzuni, migogoro, na hatari. (Soma Ufunuo 21:4.) Hakutakuwa tena na laana juu ya uumbaji, ikiwa ni pamoja na ugonjwa, kuzeeka, na kifo. (Soma Ufunuo 22:3.)

> **"Nikipata hamu ndani yangu isiyoweza kutoshelezwa na kitu chochote katika ulimwengu huu, yamkini ni kwa sababu niliumbwa kuishi katika ulimwengu mwingine....Yamkini anasa za dunia hazikukusudiwa kamwe kuitosheleza hamu hiyo, bali kuiamsha tu, kunionyesha nahitaji kitu kingine halisi zaidi.... Lazima nifanye lengo kuu la maisha yangu liwe kukaza mwendo kuelekea nchi hiyo nyingine na kuwasaidia wengine kufanya hivyo."**
>
> **C.S. Lewis**
> *Mere Christianity*

Uzuri wa mbinguni hauwezi kuelezeka. Maelezo tuliyopewa ni pamoja na kuta za yaspi, malango ya lulu, misingi ya vito adimu, na barabara za dhahabu. (Soma Ufunuo 21:18-21.)

## Nani na Wakati Gani?

Mbinguni pameandaliwa kwa ajili ya wale wanaotubu dhambi na kumwamini Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana (Yohana 3:16). Biblia inatuambia kwamba tukiishi kwa msingi wa maadili ya milele, tunaweza kuwekeza katika hazina ya milele na iliyo salama mbinguni. (Soma Mathayo 6:20.) Mbinguni pana mamilioni ya watu waliokombolewa pamoja na malaika (Ufunuo 5:8-11).

Mtu huenda mbinguni wakati gani? Yesu alimwambia mwizi aliyekuwa anakaribia kufa msalabani kwamba watakuwa pamoja katika paradiso siku hiyo (Luka 23:43). Paulo alisema kwamba kutokuwepo katika mwili ni kuwa pamoja na Bwana (2 Wakorintho 5:8). Kwa hivyo, tunajua kwamba muumini huenda mbinguni wakati wa kifo. Waumini ambao bado wako hai wakati wa kurudi kwa Yesu wataenda mbinguni bila kupitia kifo. (Soma 1 Wakorintho 15:51-52; 1 Wathesalonike 4:13-18).

## SEHEMU YA 2: HATIMA YA MILELE YA WASIOAMINI

Adhabu duniani siku zote huisha wakati fulani, hata ikiwa ni wakati wa kifo cha yule anayeadhibiwa. Lakini Yesu alieleza adhabu ambayo ni ya milele. Alisema,

> Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake…Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele (Mathayo 25:41, 46).

Yesu na mitume walithibitisha kwamba jehanamu, ziwa la moto, na adhabu ya milele zipo. Yesu alituonya tuepuke mahali hapo pa kuogofya sana. Hizi ni kauli kutoka kwa Yesu na mitume.

> Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki, na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno (MT 13:49-50).

Akizungumza na Mafarisayo, Yesu alisema, “Enyi nyoka, wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum?” (MT 23:33).

Wakati fulani Yesu alipokuwa akizungumza na Mafarisayo, alieleza kuhusu mateso ya mtu aliyekufa na kwenda jehanamu:

> Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake. Akalia, akasema, “Ee baba Ibrahimu,

> nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu" (Luka 16:23-24).

Mtume Paulo anaandika kwamba Yesu atafunuliwa

> …mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake (2 Wathesalonike 1:7-9).

Petro anaandika

> …Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu (2 Peto 2:4).

Yohana anaandika

> Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele…Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto (Ufunuo 20:10, 15).

Tazama aina ya maneno yanayotumika kueleza mahali hapo: moto, mateso, kisasi, maangamizi, giza, minyororo, hukumu, kilio, na kusaga meno.

Yesu alisema

> Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum. Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum (Mathayo 5:29-30).

Yesu alisema afadhali kung'oa jicho lako la kulia na kukata mkono wako wa kulia kuliko kutupwa jehanamu ukiwa na jicho hilo na mkono huo. Yesu hakuwa anahimiza ukataji wa viungo vya mwili, bali kusitisha kitendo chochote kitakachotuongoza katika dhambi na jehanamu, haijalishi ni cha thamani kiasi gani duniani.

» Je, baadhi ya dini ambazo zimepotoka katika kanuni zao kuhusu jehanamu ni zipi?

Biblia inatuambia kwamba kifo hutamatisha nafasi ya mwanadamu ya kuchagua hatima yake ya milele, na kwamba jehanamu ni (1) ya milele, (2) haiwezi kutenguliwa, na (3) ni mahali pa uchungu mwingi. Ukweli huu wa Biblia unakataliwa na wakana Mungu wanaosema hakuna chochote baada ya kifo, pamoja na Mashahidi wa Yehova, Wamormoni, na dhehebu

la Universalist wanaosema hakuna jehanamu. Ukweli wa kwamba kifo hutamatisha kipindi cha majaribio ya mwanadamu unakanushwa na Wakatoliki wanaoamini kwamba hali ya mwanadamu inaweza kurekebishwa baada ya kifo.

Kuna wale wanaokanusha kuwepo kwa jehanamu kwa sababu wanaona kuwa ni dhuluma. Wanasema kwamba ikiwa dhambi ilifanyika katika kipindi chenye kikomo, si haki kutoa adhabu ya milele dhidi ya dhambi. Mtakatifu Agostino alijibu pingamizi hili kupitia mfano wa sheria ya jinai. Wizi ukifanyika kwa dakika chache, je, mtu anapaswa kupewa adhabu ya dakika chache tu? Mauaji yanayotekelezwa haraka husababisha uharibifu usioweza kurekebishwa. Katika maandiko, tunaona kwamba dhambi dhidi ya Mungu wa milele na asiye na kikomo husababisha adhabu ya milele, ingawa dhambi hiyo ilitendwa katika maisha yenye kikomo.

» Je, kwa nini jehanamu ni ya milele?

Jehanamu ni ya milele kwa sababu

1. Dhambi ni kosa dhidi ya Mungu asiye na kikomo.
2. Wenye dhambi wasiotubu humnyima Mungu utumishi wa milele wanaohitaji kumpa.
3. Sisi ni viumbe wa milele na hatuna mahali pengine pa kwenda ikiwa tutachagua kutengwa na Mungu.

Duniani, tunapenda kwamba tunaweza kubadilisha maamuzi yetu. Inaonekana ni jambo zito sana kwamba uamuzi unaweza kuwa na matokeo ya milele. Tunapenda kufikiria kwamba kutakuwa na nafasi ya pili katika siku zijazo, hata ikiwa tunafanya uamuzi wa kimakusudi sasa. Lakini ni jambo linaloeleweka kwamba Mungu ameweka kikomo katika nafasi yetu ya kuamua hatima yetu ya milele ili ifikie kikomo baada ya kifo.

Wengine wanakataa kuamini kuwa kuna jehanamu kwa sababu wanashangaa jinsi Mungu mwenye upendo anaweza kumpeleka mtu mahali pa kuogofya kiasi hicho kama inavyoelezwa katika vifungu tulivyoona hapo awali. Ni lazima tukumbuke kwamba Mungu hataki

> **“Hatimaye mapingamizi dhidi ya kanuni zinazohusu jehanamu lazima yaibue swali hili: ‘Ni nini kingine unachomwomba Mungu afanye?’ Afute dhambi zao za zamani na awape mwanzo mpya, akitekeleza jambo hilo gumu kupitia msaada wa kimuujiza? Lakini tayari amejitolea kufanya hivyo. Awasamehe? Lakini wanakataa kusamehewa. Aachane nao? Nasikitika kwamba hivyo ndivyo anavyofanya.”**
>
> **C.S. Lewis**
>
> *Imefasiliwa kutoka kitabu kinachoitwa The Problem of Pain*

mtu yeyote apotee bali anataka kila mtu atubu na apate wokovu. Biblia inasema hivyo katika sehemu kadhaa. (Soma 2 Petro 3:9; 1 Timotheo 2:4; Matendo 17:30.) Wale wanaoenda jehanamu wamefanya maamuzi yanayowaweka mahali hapo pa kuogofya. Hakuna mtu anayejipata jehanamu kwa bahati mbaya. Wale wanaokwenda huko wamechagua mahali hapo kwa kumkataa Mungu, haki, na wokovu.

Kwa kuwa yote yaliyo mema hutoka kwa Mungu, kumkataa Mungu hatimaye ni kukataa yote yaliyo mema. Utulivu, usalama kutokana na hofu na uchungu, na mahali pa faraja ni mambo mazuri ambayo ni Mungu pekee ndiye anayeweza kutoa. Kutengana na Mungu kikamilifu kunamaanisha kukosa kila kitu ambacho ni kizuri, na hiyo ni jehanamu.

Mshukuru Mungu kwamba kupitia kazi ya upatanisho ya Yesu Kristo, upendo wake umefanya tuweze kuepuka ghadhabu inayokuja (1 Wathesalonike 1:10; 1 Wathesalonike 4:9). Badala ya mateso ya jehanamu, tunaweza kushiriki katika furaha ya wokovu na maajabu ya mbinguni. Tunachagua mbinguni kwa ajili ya hatima yetu tunapochagua kutubu kwa Mungu na kuweka imani katika Bwana wetu Yesu Kristo (Wafilipi 3:20, Matendo 20:21).

## MAKOSA YA KUEPUKA: KUSAHAU MATOKEO YA MILELE

Katika maisha ya duniani, maamuzi mengi hayaonekani kuwa ya mwisho. Kukiwa na muda wa kutosha, makosa mengi yanaweza kurekebishwa. Ni lazima tukumbuke kwamba maamuzi mengi yana matokeo ya milele. Hatujui tutakufa lini, na nafasi yetu ya kuchagua hatima yetu ya milele itakuwa imekwisha. Baada ya kifo hatutaweza kubadilisha matendo ambayo yaliathiri hatima yetu ya milele au matendo ambayo yaliathiri wengine katika maamuzi yao.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Kila mtu hatimaye ataishi milele mbinguni au jehanamu. Mbinguni ni makao ya Mungu ambapo waumini wataishi pamoja na Mungu, wakimwabudu kwa furaha. Mbinguni hakuna dhambi wala mateso yoyote yanayotokana na dhambi. Jehanamu ni ya milele, haiwezi kutenguliwa, na ni mahali pa adhabu yenye uchungu mwingi kwa wote ambao hawajaokolewa na Kristo kutokana nadhambi zao. Jehanamu ni adhabu ya haki kwa dhambi ya makusudi dhidi ya Mungu asiye na kikomo.

## MAZOEZI YA SOMO LA 13

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - Isaya 5:11-16
    - Mathayo 5:27-30
    - Luka 16:19-31
    - Ufunuo 22:1-5
    - Ufunuo 22:10-17

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 13. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 13

1. Je, shughuli kuu ya mbinguni ni ipi?
2. Orodhesha vitu vinne ambavyo havitakuwa mbinguni.
3. Je, ni nani ataenda mbinguni?
4. Je, waumini huenda mbinguni wakati gani?
5. Je, ni mambo gani matatu ambayo Biblia inatuambia kuhusu jehanamu?
6. Je, Yesu alimaanisha nini aliposema mtu anapaswa kukata mkono wake?
7. Orodhesha sababu tatu kwa nini jehanamu ni ya milele.

## SOMO LA 14

# MATUKIO YA MWISHO

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Viwango vya umuhimu katika mada zinazohusu matukio ya mwisho.
    - Kurudi kwa Kristo na maana yake kwa maisha ya Kikristo.
    - Ufufuo wa watu wote na thamani ya mwili.
    - Hukumu ya mwisho ya viumbe wote wenye ufahamu wa maadili.
    - Ufalme wa milele wa Mungu.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu matukio ya mwisho.

2. Mwanafunzi atajua umuhimu wa kuona maisha ya duniani kwa mtazamo wa umilele.

## UTANGULIZI

» Someni Danieli 7:9-14 pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu siku za baadaye?

Mada katika unabii wa Biblia ni pamoja na: alama ya mnyama, baragumu, dhiki kuu, mpinga Kristo, miaka saba, miaka 1,000, kiti cha enzi kikubwa cheupe, mji unaoshuka, ziwa la moto.

» Je, wewe hufikiria juu ya masuala gani katika unabii wa Biblia?

## VIWANGO VYA UMUHIMU

Majadiliano kuhusu unabii mara nyingi huzingatia maswali yasio na umuhimu mkubwa badala ya kweli kuu. Si mada zote katika unabii zina umuhimu sawa. Hatutajaribu kuzingatia kila kitu kuhusu unabii katika kozi hii.

Wakati mwingine watu hujiuliza alama ya mnyama itafananaje, mpinga Kristo atatoka nchi gani, na wale mashahidi wawili watakuwa akina nani. Haya ni maswali ambayo Biblia haijibu kwa uwazi, na kubishana juu ya maswali hayo hakuna faida.

Kuna mada zingine ambazo Biblia inafafanua zaidi. Baadhi ya mifano ni kama Yesu atarudi mwanzoni, katikati, au mwishoni mwa dhiki kuu; na kama milenia ni miaka 1,000 au la. Hata hivyo, kanuni hizi hazina umuhimu wa msingi kwa injili. Hupaswi kuvunja ushirika na mtu kwa sababu hukubaliani na maoni yake kuhusu mojawapo ya maswali haya.

Kuna kweli muhimu katika unabii wa Biblia. Hizi ni kweli ambazo ziko wazi sana kiasi kwamba kila mtu anayeamini Biblia anazikubali. Kanuni hizi zinaathiri maisha ya Kikristo na mfumo mzima wa kanuni za Kikristo. Hebu tuangalie kweli nne muhimu zilizofunuliwa katika unabii wa Biblia kuhusu matukio ya mwisho.

## KURUDI KWA YESU KIMWILI

Yesu atarudi katika dunia hii akionekana. Ingawa kiroho yuko pamoja na waumini duniani sasa, atarudi katika umbo lake lililotukuzwa la ufufuo akionekana na dunia nzima. (Soma Ufunuo 1:7.)

» Je, ni mambo gani yatakayotokea Yesu atakaporudi?

Kurudi kwa Kristo kutakuwa kilele cha historia ya dunia. Falme za ulimwengu zitakuwa falme za Kristo. Wale ambao wamekuwa waaminifu kwake watapewa thawabu na kuheshimiwa. Wale ambao wamekuwa katika uasi dhidi yake watawekwa chini, naye atakuwa na nguvu ambazo zitashinda upinzani wote. (Soma Mathayo 26:64.) Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri kwamba Yesu ni Bwana (Wafilipi 2:10-11).

Wakristo waliokufa watafufuliwa ili watawale pamoja na Kristo (2 Timotheo 2:12). Wao na waumini walio hai watanyakuliwa juu ili kumlaki Bwana atakapotokea (1 Wathesalonike 4:16-17).

Kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye baraka la Wakristo wote. (Soma Tito 2:13.) Fikiria yote ambayo kurudi kwake kunamaanisha kwetu: mwisho wa mateso, dhiki, na huzuni; kuungana tena na watakatifu na

**"Hakuna mtu amepiga hatua mbele katika shule ya Kristo ambaye hasubiri kwa furaha siku ya kifo na ufufuo wa mwisho. Tusubiri ujio wa Bwana kwa hamu kwa sababu hilo ndilo jambo la kufurahisha zaidi kuliko yote. Atakuja kwetu kama Mkombozi na atatuongoza katika urithi huo uliobarikiwa wa uzima na utukufu wake."**

**John Calvin**

Imetolewa kutoka katika kitabu kinachoitwa *Institutes*

wapendwa Wakristo; uthibitisho kwamba imani yetu haikuwa kazi bure; kumwona Yesu mwenyewe; na kuingia mbinguni na utimilifu wa uzima wa milele pamoja na Mungu. Mambo haya yote hayategemei wakati wa kurudi kwake, bali yanategemea tu ukweli kwamba atarudi kama alivyoahidi.

Yesu alisema kwamba atarudi katika nguvu na utukufu (Mathayo 24:30). Aliahidi kwamba atakuja kuwachukua watu wake ili waishi naye (Yohana 14:3). Malaika walisema kwamba atarudi kwa njia ile ile aliyopaa kwenda mbinguni (Matendo 1:11). Mitume walihubiri toba huku wakingoja Kristo arudi ili aanzishe mpango mkuu wa Mungu kwa ajili ya ulimwengu huu. (Soma Matendo 3:19-21.) Kurudi kwa Yesu duniani tena katika nguvu na utukufu ni jambo linalofunzwa tena na tena katika Agano Jipya.[19]

Ingawa kuna ishara zitakazotangulia kuja kwa Yesu mara ya pili, hatuwezi kujua ni lini hasa atarudi. Ni vizuri kwa waumini siku zote kutazamia kuja kwa Yesu na kuishi ipasavyo. (Soma Marko 13:33-37.)

» Je, Yesu atarudi tena kwa nini?

Tunaishi katika ulimwengu ambapo watu wengi wanamwasi Mungu. Uumbaji wote unateseka kutokana na laana ya dhambi. Ulimwengu hautafanywa kuwa mkamilifu kamwe kupitia hatua za kisiasa, mageuzi ya kijamii, elimu iliyoboreshwa, au mafanikio ya kiuchumi. Yesu ataingia ghafla katika uumbaji wake kama mfalme anayerudi ili kuuweka sawa.

Watu wote ni wenye dhambi, lakini wakijiunga na ufalme wa Mungu kwa hiari sasa, wanaweza kuepuka hukumu inayokuja. Ufalme wa Mungu tayari unafanya kazi kati ya wale wanaotubu na kuamini (Marko 1: 14-15, Marko 9: 1). Ufalme huo utakuja kikamilifu na kwa uwazi wakati wa kurudi kwa Yesu.

» Je, tunapaswa kuishi vipi kwa sababu tunajua Yesu anarudi?

Ni lazima tukumbuke vipaumbele vya Wakristo wa awali. Tunahamaishwa kudumisha imani yetu (1 Wakorintho 16:13) na kuvumilia hadi mwisho (Mathayo 24:13). Tunaonywa tusiruhusu anasa na mambo ya dunia yatufanye tusahau kuhusu kuja kwa Kristo (Luka 21:34-36). Tunaishi kulingana na maadili ya milele kwa kuwa mambo ya ulimwengu huu yatapita (2 Petro 3:11-13). Tunaambiwa tukeshe, si kwa kutazama anga kwa ajili ya kuonekana kwake, bali kwa kukaa macho kiroho ili ujio wake usitupate tukiwa hatujajitayarisha (Marko 13:33-37). Tunaomba kwa ajili ya usafi na kuishi maisha safi kwa sababu tunataka kuwa kama yeye (1 Yohana 3:3).

Wale wanaoishi leo kana kwamba Yesu hatarudi hawatakuwa tayari kwa kurudi kwake. Ujio wa Yesu utakuwa kama umeme (Mathayo 24:27; 1 Wakorintho 15:52), utakuwa wa

---

19 1 Wathesalonike 4:15-16; 2 Wathesalonike 1:7, 10; Tito 2:13; Waebrania 9:28; Yakobo 5:7-8; 1 Petro 1:7, 13; 2 Petro 1:16, 2 Petro 3:4, 12; 1 Yohana 2:28

ghafla sana kiasi kwamba hakuna mtu atakayekuwa na wakati wa kubadilisha chochote baada ya kutokea kwake. 1 Wathesalonike 5:1-6 inaonyesha kwamba wale walio gizani, wale wanaoishi kwa ajili ya ulimwengu huu, watashtushwa na kurudi kwa Bwana. Kwao, kurudi kwake kutakuwa kama kuingiliwa na mwizi. Kwa waumini, kurudi kwake hakutawashtua, bali kutawaleta furaha kuu, kama vile bwana harusi anavyokuja kumchukua bibi harusi wake (Yohana 14:2-3).

Tunasubiri kuja kwa Yesu kwa

1. Kudumisha vipaumbele vya milele
2. Kuishi maisha safi
3. Kujilinda kiroho kwa maombi

## UFUFUO WA KIMWILI WA WATU WOTE

Tunajua kwamba mwili una thamani ya milele kwa sababu Biblia inafundisha ufufuo wa watu wote. Kanuni ya ufufuo ni muhimu. Tunajua hilo kwa sababu Mtume Paulo alitumia 1 Wakorintho 15 yote kutetea kanuni hiyo. Alieleza kwamba kukana ufufuo ni kukana injili. Ikiwa hakuna ufufuo, basi Yesu asingeweza kufufuka (1 Wakorintho 15:13). Ikiwa Yesu hakufufuka kutoka kwa wafu, injili haiwezi kuwa ya kweli, na hakuna mtu ambaye ameokoka (1 Wakorintho 15:17).

Kila mtu atafufuliwa, lakini si watu wote kwa wakati mmoja. Wakati wa kurudi kwa Yesu, atawachukua Wakristo wote, akiwafufua wale waliokufa (1 Wathesalonike 4:16-17; Ufunuo 20:6). Wale waliokufa katika dhambi zao hawatafufuliwa katika ufufuo wa kwanza. Watafufuliwa baadaye ili wahukumiwe hukumu (Ufunuo 20:13).

> **"Ewe mauti, uchungu wako uko wapi?**
> **Ewe Kuzimu, ushindi wako uko wapi?**
> **Kristo amefufuka, nanyi mmeangamizwa.**
> **Kristo amefufuka, na pepo wametupwa chini.**
> **Kristo amefufuka, na malaika wanafurahi.**
> **Kristo amefufuka, na uzima umewekwa huru.**
> **Kristo amefufuka,**
> **na wafu wameondolewa kaburini:**
> **kwa maana Kristo, akiwa amefufuka kutoka kwa wafu, amekuwa Kiongozi na Mfufuaji wa wale waliokufa.**
> **Utukufu na nguvu ni zake milele na milele. Amina."**
>
> **Chrysostom,**
> "Hotuba ya Pasaka"

Wakristo watafufuliwa katika miili iliyotukuzwa kama Yesu (1 Yohana 3:2). Wenye dhambi ambao hawajaongoka watafufuliwa kwa namna nyingine kwa ajili ya adhabu ya milele (Yohana 5:28-29).

» Je, ikiwa huamini kwamba mwili utafufuliwa, hilo lingeleta tofauti gani kwako?

Imani ya kwamba siku moja tutafufuliwa huathiri mtindo wetu wa maisha. Tunaweza kuona athari za kiutendaji za kanuni hiyo tunapoangalia mifano ya watu wanaolikana. Watu fulani katika kutaniko la Korintho walikana kwamba mwili wa mwanadamu utafufuliwa. Wale walioamini kosa hilo waligawanyika katika misimamo miwili.

Kuna wale waliosema, **"Kwa kuwa mwili hautafufuliwa, roho pekee ndio yenye umuhimu**. Hiyo ina maana kwamba dhambi tunazofanya kupitia mwili si mbaya. Tunaweza hata kuzini kwa sababu mwili utatupiliwa mbali."

Baadhi ya Wakorintho walionekana kuwa na kauli mbiu inayosema, "Chakula ni kwa ajili ya tumbo na tumbo ni kwa ajili ya chakula," ikimaanisha kwamba mwili hauna kazi yoyote isipokuwa kukidhi tamaa. Paulo aliwaambia kwamba watu watahukumiwa kwa ajili ya matumizi mabaya ya mwili (1 Wakorintho 6:13). Alisema kwamba mwili ni kwa ajili ya Bwana, na kwamba Mungu ataifufua miili yetu kama alivyoufufua mwili wa Yesu (1 Wakorintho 6:14).

Wengine walisema, **"Kwa kuwa mwili hautafufuliwa, ni lazima uwe hauna thamani na mwovu.** Tunapaswa kuzuia tamaa zote za mwili, tusile chochote chenye ladha nzuri wala tusifurahie ndoa."

Makosa haya yote mawili yalitokana na kukana ufufuo. Kukataa ufufuo kunashusha thamani ya mwili. Lakini kanuni ya Kikristo ya ufufuo inaupatia mwili thamani.

» Soma 1 Wakorintho 6:14, 15, 19-20.

Vifungu hivi vinaonyesha kwamba miili ya Wakristo ni yenye thamani kwa sababu Wakristo

- Wamekombolewa
- Ni mahekalu ya Roho Mtakatifu
- Ni viungo vya Kristo
- Watafufuliwa na kutukuzwa

Kanuni ya ufufuo ni muhimu kwa sababu inamaanisha kwamba

- Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.
- Watu wote watafufuliwa.
- Mwili una thamani ya milele.
- Injili ni kweli.

## HUKUMU

Siku ya Hukumu hakika ni mwisho kwa wale ambao majina yao hayamo katika kitabu cha uzima. Si mwisho wa uhai wao, lakini ni mwisho wa fursa yao ya kufanya maamuzi. Katika umilele unaofuata, watu watapata matokeo yasiyo na kikomo ya maamuzi yao, ambayo hayawezi kutenguliwa.

Hukumu inayapa maamuzi yetu umuhimu zaidi ya matokeo yao ya hapo mwanzoni. Watu wengine hufikiri kwamba mradi tu wanaweza kudhibiti matokeo ya matendo yao, hakuna kitu kingine cha kuwatia wasiwasi. Wanataka kuamini kwamba dhambi yao si mbaya ikiwa haina madhara yoyote. Kwa kweli, dhambi zote zina madhara. Lakini hata kama haikuleta madhara katika maisha haya, dhambi ni jambo zito kwa sababu ya hukumu. Neno la Mungu linasema kwamba watu watahukumiwa kwa ajili ya matendo yao. (Soma 2 Wakorintho 5:10; Waroma 2:6-11.)

Katika hukumu, watu wengine watapelekwa kwenye adhabu ya milele na wengine kwenye thawabu ya milele. Maandiko yanaeleza tukio moja la hukumu kwa wenye dhambi ambao hawajaongoka watakaofufuliwa ili kukabiliwa na hukumu kwa ajili ya matendo yao ya dhambi. (Tazama Ufunuo 20:11-15.) Kuna hukumu nyingine kwa Wakristo, ambapo watapewa thawabu kwa ajili ya matendo yao yenye matokeo mazuri na yenye kudumu. (Soma 1 Wakorintho 3:14-15.)

Hukumu inamaanisha kwamba siku moja dhambi haitakuwepo tena. Ni vigumu kufikiria ulimwengu usio na dhambi, lakini siku moja uasi wote dhidi ya Mungu utakomeshwa.

Mungu hataki tuishi kwa hofu wakati wote, au hofu hiyo iwe kitu kinachotutia motisha kuishi kwa haki. Hata hivyo, kufahamu kwamba kuna hukumu inayokuja kunatupatia hisia ya uwajibikaji inayoongoza maisha yetu.

Lazima tujue kuhusu hukumu ili tuelewe

1. Umuhimu wa dhambi
2. Uwajibikaji wetu kwa Mungu
3. Umuhimu wa maamuzi yetu
4. Mwisho wa dhambi zote

## UFALME WA MILELE WA MUNGU

Kulingana na falsafa na dini zingine, wakati unaendelea milele katika mizunguko, bila mwanzo wala mwisho, na hakuna matukio yanayobadilisha mambo milele. Lakini kulingana na Biblia, wakati una mwanzo na mfululizo wa matukio yanayoendelea hadi kufikia tamatisho. Biblia inaeleza kuhusu uumbaji, kisha anguko la kusikitisha la mwanadamu, kisha mpango wa wokovu ambao Mungu anautekeleza katika karne za historia ya mwanadamu.

Katika Mwanzo 3 tunapata mwanzo wa dhambi. Katika Ufunuo dhambi hairuhusiwi katika mji wa milele wa Mungu (Ufunuo 21:27). Katika Mwanzo tunaona kupotea kwa mti wa uzima na hukumu ya kifo (Mwanzo 3:22-24). Katika Ufunuo tunaona urejesho wa mti wa uzima, majina katika kitabu cha uzima, na mwaliko kwenye mto wa maji ya uzima (Ufunuo 22:1-2, 19).

Ujio wa ufalme mkamilifu na wa milele wa Mungu kutatimiza mpango wa Mungu. Mungu siku zote amekuwa Mfalme wa ulimwengu wake, lakini tangu anguko la mwanadamu, wanadamu wengi wamekuwa katika uasi dhidi ya ufalme wa Mungu. Uasi huo utaisha ghafla, na Mungu atatawala milele bila mpinzani. Ulimwengu utakuwa mkamilifu kama vile Mungu anavyotaka, kama vile ilivyo mbinguni.

## MAKOSA YA KUEPUKA: KUZINGATIA MAMBO YA KIDUNIA

Kuna mwelekeo wa mwanadamu wa kuishi kana kwamba maisha ya dunia yataendelea milele. Tunajaribu kuboresha hali zetu, kutatua matatizo yetu, na kuunda mazingira yanayoturidhisha. Tunahitaji kuwa kama Abrahamu ambaye alikuwa akitarajia makao ya milele alipokuwa akiishi katika hema na kuhamahama mara kwa mara (Waebrania 11:8-10, 14-16). Tunapaswa kukumbuka kwamba vitu tunavyojenga, vitu tulivyo navyo, na hali tunazounda vyote ni vya muda tu. Tunapaswa kufanyia kazi vitu ambavyo vina thamani ya milele.

» Someni pamoja kauli ya imani angalau mara mbili.

### KAULI YA IMANI

Yesu atarudi kama alivyoahidi, akiwafufua waumini wa zamani, na kuwachukua waumini wote ili watawale katika ufalme wake. Kila mtu atafufuliwa kutoka kwa wafu ili ahukumiwe kwa ajili ya matendo yake. Atapewa thawabu ya milele au kuhukumiwa adhabu ya milele. Ufalme wa Mungu utakuja kikamilifu, na Mungu atatawala milele.

## MAZOEZI YA SOMO LA 14

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

   - Danieli 2:31-45
   - Mathayo 25:31-46
   - 1 Wakorintho 15:51-58
   - 2 Petro 3:1-14
   - Ufunuo 20:11-15

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 14. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 14

1. Je, ni zipi kweli nne muhimu zilizotolewa katika unabii wa Biblia kuhusu matukio ya mwisho?

2. Je, nini kitatokea kwa Wakristo Yesu atakaporudi?

3. Je, tunapaswa kusubirije ujio wa Yesu?

4. Je, kwa nini kanuni ya ufufuo ni muhimu?

5. Tunapaswa kujua kuhusu hukumu ili tuelewe mambo gani manne?

## SOMO LA 15

# KANUNI ZA IMANI ZA KALE

### MALENGO YA SOMO

1. Mwanafunzi ataweza kueleza:

    - Kusudi na matumizi ya kauli ya imani kama taarifa ya imani.
    - Baadhi ya mifano ya kanuni za imani katika Biblia.
    - Asili na maudhui ya kanuni tatu za imani za kihistoria.
    - Kwa nini Wakristo wa kisasa lazima washikilie Ukristo wa kihistoria.
    - Kauli ya kanuni za Kikristo kuhusu kanuni za imani.

2. Mwanafunzi atathamini kanuni za msingi za kanisa la awali kama Ukristo wa asili.

## UTANGULIZI

» Someni 2 Yohana pamoja. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu umuhimu wa kanuni za asili za kanisa?

## Asili ya Kanuni za Imani

Kanuni ya imani ni muhtasari wa kanuni za msingi za Kikristo. Kanisa la awali liliona haja ya kufanya muhtasari wa kanuni za Biblia.


» Je, kwa nini kanisa lilihitaji kanuni za imani? Biblia haikutosha?

Siku zote kuna watu wanaodai kuamini Biblia ilhali wanafundisha kanuni zinazopingana na Biblia. Kanisa lilibuni kauli za kanuni za Biblia ambazo zilitofautisha Ukristo halisi na kanuni za uongo.

Mojawapo ya kauli za kwanza za kanuni ilikuwa "**Yesu ni Bwana**," ambayo ilimaanisha kwamba Yesu ni Mungu. Maneno, ***Bwana Yesu Kristo*** pia yalitoa kauli, yakisema kwamba

Yesu ndiye Masihi (*Christos*) na kwamba yeye ni Mungu. Mtu aliyekataa kusema kwamba Yesu ni Bwana au kutumia maneno *Bwana Yesu Kristo* alichukuliwa kuwa si muumini.

Baadaye kulikuwa na watu waliodai kuwa Wakristo lakini hawakuamini kwamba **Yesu kweli alikuwa mwanadamu**. Ndio maana katika waraka wa 1 Yohana tunapata kanuni hii ya imani, "Kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu" (1 Yohana 4:2-3). Mtume pia alisema kwamba mtu akikana kanuni za msingi za Kristo, anafanya dhambi na si wa Mungu (2 Yohana 1:9).



*Atanasi*

Kanuni ya imani ya kale zaidi inayotoa kauli kadhaa iko katika 1 Timotheo 3:16:

> Mungu alidhihirishwa katika mwili, akajulika kuwa na haki katika roho, akaonekana na malaika, akahubiriwa katika mataifa, akaaminiwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika utukufu.

Hatujui masuala yote yaliyokuwa yanashughulikiwa na kanuni ya imani ya 1 Timotheo, lakini inasisitiza uungu na ubinadamu wa Yesu inaposema kwamba Mungu alidhihirishwa katika mwili.[20]

> **"Inahitajika kwa ajili ya wokovu wa milele kwamba mtu pia aamini ipasavyo umwilisho wa Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa maana imani sahihi ni kwamba tuamini na tukiri kwamba Bwana wetu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ni Mungu na Mwanadamu."**
>
> Kanuni ya Imani ya Atanasi

Kauli hizi fupi za imani zilitimiza kusudi fulani. Ikiwa Mkristo wa awali angekutana na mtu mwingine aliyedai kumwamini Yesu, Mkristo huyo angeweza kuuliza, "Je, unaamini kwamba Yesu ni Bwana?" au "Je, unaamini kwamba Yesu ni Mungu aliyekuja katika mwili?" Ikiwa mtu huyo angesema "hapana," basi Mkristo huyo alijua kwamba mtu huyo hajui au hakubali yale ambayo Yesu na mitume walifundisha.[21]

---

20 Picha: "S. Athanasius", imetolewa kutoka Bibliothèque Sainte-Geneviève Images, https://archive.org/details/EST84RESP8A, kikoa cha umma.

21 Atanasi, aliyeishi takriban miaka ya 296-373, aliandika makala maarufu kwa jina "Kuhusu Umwilisho," ambapo alieleza kwa nini uungu kamili na ubinadamu kamili wa Yesu ulikuwa muhimu sana kwa imani ya Kikristo. Alikuwa na ushawishi mkubwa katika Baraza la Nisea, ambalo lilitoa Kanuni ya Imani ya Nisea.

Katika karne chache za kwanza baada ya Pentekoste, kanisa liliona ni muhimu kutoa kauli za wazi kuhusu Utatu wa Mungu, umwilisho wa Kristo, na utambulisho wa Roho Mtakatifu. Waliweka viwango vya kanuni kama kinga dhidi ya mafundisho potovu. Kanuni za imani zilikusudiwa kuwa mihtasari ya kweli za msingi ambazo kila Mkristo aliamini.

Kanuni hizo za imani hazingeweza kuzingatia kila suala, lakini mtu hangechukuliwa kuwa Mkristo ikiwa angekana chochote katika kanuni hizo za imani za kale. Zilikuwa ni jaribio la kufafanua imani ya Kikristo.

Hizi hapa ni kanuni tatu za kale za kanisa.

## KANUNI YA IMANI YA MITUME

Kanuni ya Imani ya Mitume haikuandikwa na mitume, lakini iliandikwa katika karne ya pili ili kueleza kanuni za mitume.

> Namwamini Mungu Baba mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi;
>
> Namwamini Yesu Kristo Mwana wake wa pekee, Bwana wetu. Aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na akazaliwa na Bikira Mariamu. Aliteswa mikononi mwa Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa. Akashuka kuzimu. Siku ya tatu akafufuka kutoka kwa wafu. Akapaa mbinguni na ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi; kutoka huko atakuja kuwahukumu watu walio hai na waliokufa.
>
> Namwamini Roho Mtakatifu, kanisa Takatifu Katoliki, ushirika wa watakatifu, ondoleo la dhambi, kufufuliwa kwa mwili, na Uzima wa milele. Amina.

Inaonekana kwamba kanuni hii ya imani ilikusudiwa kufichua makosa ya wale waliokana kwamba Yesu kweli alikuwa mwanadamu na alizaliwa na bikira. Pia kulikuwa na wengine waliokana kwamba Yesu alikufa kweli au kwamba alifufuka kimwili kutoka kwa wafu.

Machache sana yanasemwa kuhusu Roho Mtakatifu katika Kanuni ya Imani ya Mitume. Hiyo si kwa sababu kanisa halikujua Roho Mtakatifu ni nani; ni kwa sababu mafundisho potovu kuhusu utambulisho wake bado hayakuwa yanaleta changamoto kwa kanisa.

Neno *katoliki* linamaanisha “ya dunia nzima” ambayo inamaanisha kwamba kuna kanisa moja la kweli.

“Msamaha wa dhambi” unamaanisha wokovu kwa neema badala ya matendo au desturi.

## KANUNI YA IMANI YA NISEA

Kanuni ya Imani ya Nisea ilizinduliwa katika baraza la kanisa mwaka 325. Kusudi lake lilikuwa kulinda kanuni ya uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu. Kauli chache ziliongezwa katika baraza lingine mwaka 381. Kanuni hii ya imani hii inashughulikia masuala ambayo hayakuwa yameibuka hapo awali.

> Tunamwamini Mungu mmoja, Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.
>
> Tunamwamini Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa kutoka kwa Baba kabla ya enzi zote, Mungu kutoka Mungu, yu Nuru kutoka Nuru, yu Mungu kweli kutoka Mungu kweli; aliyezaliwa bila kuumbwa; mwenye uungu mmoja na Baba. Kupitia yeye huyu vitu vyote viliumbwa. Aliyeshuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu na kwa ajili ya wokovu wetu; akatwaa mwili kwa uweza wa Roho Mtakatifu na Bikira Mariamu, akawa mwanadamu. Akasulibiwa kwa ajili yetu mikononi mwa Pontio Pilato; aliteswa, akafa, akazikwa. Siku ya tatu akafufuka kama yanenavyo Maandiko Matakatifu. Akapaa mbinguni na ameketi mkono wa kuume wa Baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai una wafu. Na ufalme wake hauna mwisho.
>
> Tunamwamini Roho Mtakatifu, Bwana, mtoa uzima. Anatoka katika Baba na Mwana, anaabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana. Alinena kwa vinywa vya manabii.
>
> Tunaamini Kanisa moja takatifu la katoliki na la kitume. Tunakiri ubatizo mmoja kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Tunatazamia ufufuo wa wafu, na uzima wa ulimwengu unaokuja. Amina.

» Je, ni yapi baadhi ya mambo unayoyaona katika kanuni hii ya imani ambayo hayakuwa katika Kanuni ya Imani ya Mitume?

Hapa tunaona kauli zilizofafanuliwa kuhusu nafsi zote tatu za Utatu wa Mungu. Uungu kamili wa Kristo unasisitizwa kwa njia ya kuulinda dhidi ya wale wanaodai kuamini kwamba Yesu ni Mungu na bado wanadidimisha uungu wake. Yeye ni wa milele (tangu kabla ya enzi zote), hajaumbwa, na ana asili moja na Baba. Yesu anapaswa kuitwa Mungu kwa sababu zile zile zinazofanya Baba aitwe Mungu.

Roho Mtakatifu anapaswa kuabudiwa kama Baba na Mwana, ambayo inathibitisha kwamba yeye ni Mungu.

## KANUNI YA IMANI YA CHALSEDONIA

Kanuni ya Imani ya Chalsedonia iliandikwa mwaka 451. Kusudi lake lilikuwa kulinda kanuni ya umwilisho wa Kristo. Lengo la waandishi lilikuwa kulinda kanuni ya uungu kamili na ubinadamu kamili wa Kristo, bila kipengele chochote kati ya hivyo viwili kudidimishwa sana kiasi cha kukifanya kiwe hakina maana.

Mwishowe waandishi walisema kwamba walichukulia kwamba kanuni hizo zina msingi wa kimaandiko na zimekuwa sehemu ya desturi za kanisa. Hawakuwa wanakuza mawazo mapya bali walikuwa wanatetea kile ambacho kanisa limekuwa likiamini siku zote.

> Kwa hivyo, tukiwafuata baba watakatifu, sote tunaungana katika kufundisha kwamba tunapaswa kumkiri Mwana mmoja, Bwana wetu Yesu Kristo, mtu yule yule mkamilifu katika uungu na pia mkamilifu katika ubinadamu; Mungu kweli na mwanadamu kweli, mwenye nafsi ya kimantiki na mwili. Yeye ni mwenye asili sawa na Baba kulingana na uungu wake, na ni mwenye asili sawa na sisi kulingana na ubinadamu wake, kama sisi katika mambo yote, lakini bila dhambi. Kabla ya wakati, alizaliwa kutokana na Baba kulingana na uungu wake. Katika siku za mwisho, kwa ajili yetu na kwa ajili ya wokovu wetu, alizaliwa na Bikira Mariamu, mama ya Mungu kulingana na ubinadamu wake. Yeye ni Kristo, Mwana, Bwana, na mzaliwa wa pekee yule yule, ambaye anajulikana katika asili mbili ambazo hazipaswi kukanganywa, hazibadiliki, haziwezi kugawanywa, na hazitenganishwi. Tofauti kati ya asili zake haiharibiki hata kidogo kwa sababu ya muungano wao, badala yake, sifa za kila asili zimehifadhiwa, na hutokea kwa wakati mmoja katika mtu mmoja na katika uhai mmoja, ambao haujatenganishwa au kugawanywa katika nafsi mbili, bali yeye ni Mwana mmoja, na mzaliwa wa pekee, Mungu Neno, Bwana Yesu Kristo. Hivyo ndivyo manabii walivyonena juu yake tangu mwanzo, na ndivyo alivyotufundisha Yesu Kristo mwenyewe, na Baraza la akina baba limetukabidhi imani.

» Je, unaona mambo fulani yaliyosisitizwa katika kanuni hii ya imani?

Uungu wa Kristo haikuwa sifa ambayo Yesu alikuwa nayo mbinguni tu lakini si duniani. Wakristo wa awali waliamini kwamba Yesu kweli alikuwa Mungu katika mwili. Alikuwa na sifa za Mungu na za mwanadamu kikamilifu alipokuwa duniani. Walichukulia asili hiyo ya Kristo kuwa sifa yake ya kipekee iliyomwezesha kuhitimu kama Mwokozi.

## KANUNI ZA IMANI LEO

Karne nyingi zimepita tangu kanisa lianze. Ulimwengu umebadilika kwa njia nyingi. Imani nyingi za kidini zimesitawi.

Watu wengine wanafikiri kwamba hakuna kanuni ambazo ni lazima zibaki vile vile. Wanahisi wako huru kuamini chochote wanachotaka na bado wajiite Wakristo.

» Je, ni muhimu kwetu kuamini kanuni za imani za kale za kanisa?

Mungu wa Biblia, aliyeelezwa katika kanuni za imani za kale, habadiliki. Wakristo wa mapema walijua kwamba Mungu aliwaokoa kwa sababu ya itikio lao la imani kwake. Kauli hizi kuhusu asili ya Mungu na njia za wokovu zilikuwa ni Ukristo wa msingi tangu mwanzo.

> **"Lakini kanuni yoyote mpya lazima iwe potovu; kwani dini ya zamani ndio dini pekee ya kweli; na hakuna kanuni inayoweza kuwa sahihi, isipokuwa iwe lile lile 'iliyokuwako tangu mwanzo.'"**
>
> **John Wesley**
> "Kuhusu Dhambi Katika Waumini"

Inawezekana mtu kuokoka bila kujua kanuni hizi zote au kuzielewa kwa usahihi. Si kanuni zote ni muhimu kwa injili. Mtu hawezi kukana kile anachojua ni kweli na bado awe Mkristo, lakini anaweza kukosea katika mambo fulani.

Kanuni za imani za kale katika somo hili zinazungumza tu kuhusu kanuni za msingi. Ikiwa kanisa fulani lina mtazamo wa Mungu ambao ni tofauti na kanuni hizi za msingi, lazima pia wabuni njia tofauti ya wokovu, ambayo ni injili nyingine. Wakifanya hivyo, hawapaswi kujiita Wakristo kwa sababu wanabuni dini mpya.

Bila shaka, kila mtu yuko huru kufikiria kile anachotaka, lakini ikiwa hafuati kanuni za Kikristo, yeye si mfuasi wa kweli wa Yesu.

Katika karne chache za kwanza hapakuwa na madhehebu kama tulivyo nayo leo. Kulikuwa na kanisa moja. Kwa hivyo kanuni za imani zilikuwa ni kauli za kanisa zima. Leo, makanisa yanayoheshimu mamlaka ya Biblia yanashikilia imani ya kanuni za imani, ingawa hayakubaliani katika masuala mengine mengi.

Kanisa la awali lilijua kwamba kuwa na uhusiano na Mungu ndio jambo la muhimu zaidi. Walijua kwamba waliokolewa kupitia uhusiano wao na Mungu. Ndio maana ilikuwa muhimu sana kwao kuhakikisha kwamba wanajua jinsi Mungu alivyo.

Kitabu cha Yuda kinatuonya kwamba ni lazima tutetee imani iliyopewa kanisa hapo mwanzoni (Yuda 1:3). Mungu na autie mafuta ukweli wake tunapohudumu kwa uaminifu katika kuhubiri injili, kuwafundisha waumini, na kuwafundisha wale anaowaita katika huduma.

## MAKOSA YA KUEPUKA: KIBURI CHA KIDHEHEBU

Kundi la makanisa lililounganishwa katika shirika moja linaitwa dhehebu. Kuna maelfu ya madhehebu ambayo yanadai kuwa ya Kikristo. Pia kuna maelfu ya makanisa huru ambayo si sehemu ya dhehebu lolote.

Wakati mwingine madhehebu huanza na uinjilisti. Ikiwa kuna waongofu wengi katika eneo fulani, na hakuna dhehebu linalowatunza, dhehebu jipya linaweza kujitokeza. Dhehebu linaweza kuanza kutokana na kazi ya shirika la misheni katika nchi.

Wakati mwingine dhehebu huanzishwa na kundi la watu wanaoamini kwamba kanuni muhimu inakanwa au kupuuzwa na kanisa lao. Wanaanzisha dhehebu jipya wakiwa na nia ya kuwa sahihi kikanuni. Kadiri muda unavyozidi kupita, wanaendelea kukuza kanuni zao. Kwa sababu wanaelewa Biblia kwa njia tofauti na vikundi vingine vya Wakristo, baadhi ya kanuni zao ni tofauti na madhehebu mengine.

Madhehebu pia hukuza desturi kuhusu aina sahihi za ibada na mambo ya maisha ya Kikristo. Madhehebu hutofautiana katika desturi zao.

Madhehebu mengi ya Kikristo hayadai kuwa kanisa pekee la kweli. Ikiwa shirika fulani linadai kuwa kanisa lote la Mungu duniani, halipaswi kuaminiwa.

Wasioamini mara nyingi hupinga Ukristo kwa sababu ya migawanyiko yake na aina mbalimbali za Ukristo zilizopo. Wasioamini hufikiri kwamba madhehebu mbalimbali ya Ukristo yote yanapingana. Watu wengi ulimwenguni hufikiri kwamba kuna kiwango kidogo cha umoja miongoni mwa Wakristo.

Dhehebu au kanisa la kieneo ambalo kweli ni la Kikristo huamini kanuni za imani za Kikristo za kale. Huo ndio umoja wa kikanuni uliopo miongoni mwa mashirika yote ya Kikristo. Kuna maoni mengi mbalimbali katika masuala madogo ya kikanuni na desturi, lakini hatupaswi kusema kwamba kanisa fulani si la Kikristo kweli kwa sababu ya tofauti hizo.

## MAKOSA YA KUEPUKA: KUTOELEWA MASADIKISHO YA KIBINAFSI

Mkristo anapoishi katika uhusiano na Mungu, anakuza uelewa wake wa ukweli wa Biblia. Hatafikia mahitimisho sawa na wengine siku zote. Kadiri anavyotumia ukweli katika maisha ya kila siku, atakuza kanuni na sheria kwa ajili yake mwenyewe ambazo zitakuwa tofauti na za Wakristo wengine.

Mtu anapofikiri juu ya imani yake, hapaswi kuhisi yuko huru kukataa kanuni za msingi za Ukristo wa awali isipokuwa awe ameamua kwamba yeye si Mkristo tena.

Mkristo anapaswa pia kuamini kanuni zilizowekwa za kanisa lake. Ikiwa anaamini kwamba kanuni za kanisa lake si sahihi, itakuwa vigumu kwake kujitolea kikweli kwa kanisa hilo kama mshirika.

Mkristo ataongozwa na mafundisho ya kanisa lake, lakini huenda akawa na masadikisho ya kibinafsi yanayotofautiana hata na ya washirika wengine wa kanisa lake. Sadikisho la kibinafsi si jambo linalosemwa moja kwa moja katika Biblia; ni jaribio la mtu kutumia ukweli wa Biblia katika suala fulani.

Kila Mkristo anapaswa kutumia ukweli wa Biblia kwa unyoofu katika hali zake, lakini hapaswi kuwa mwepesi kuwahukumu wengine kwa msingi wa mahitimisho yake mwenyewe. Ni sawa kwetu kutarajia Wakristo wote washikilie kanuni za imani za kale, na ni sawa kwetu kutarajia washirika wa kanisa washikilie kanuni za kanisa lao, lakini si sawa Mkristo kutarajia wengine wakubaliane na kanuni zake zote za kibinafsi.

» Someni kauli ya imani pamoja angalau mara mbili.

## KAULI YA IMANI

Maandiko yanatuambia tushikilie na tutetee kanuni za asili za Ukristo. Wakristo wa awali walitoa kauli za imani ambazo ni muhimu kwa injili na uhusiano wetu na Mungu. Kauli hizo bado zinafafanua Ukristo wa msingi.

## MAZOEZI YA SOMO LA 15

1. Zoezi la Kifungu cha Biblia: Kila mwanafunzi atapewa mojawapo ya vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini. Kabla ya kipindi kinachofuata cha darasa, unapaswa kusoma kifungu chako na kuandika aya moja kuhusu kile ambacho kifungu hicho kinasema kuhusu mada ya somo hili.

    - 1 Timotheo 3:16
    - 1 Timotheo 4:1-7
    - Tito 1:7-14
    - 1 Yohana 4:1-3, 14-15; 1 John 5:12
    - Yuda 1:3-13

2. Mtihani: Utaanza darasa linalofuata kwa kufanya mtihani juu ya Somo la 15. Jiandae kwa kuchunguza maswali ya mtihani kwa makini.

3. Zoezi la Kufundisha: Kumbuka kupanga na kutoa ripoti juu ya wakati wako wa kufundisha nje ya darasa.

## MTIHANI WA SOMO LA 15

1. Je, kanuni ya imani ni nini?
2. Taja kauli mbili za kikanuni za kwanza kuhusu Yesu.
3. Je, rejeo la kanuni ya imani ya kwanza katika maandiko ambalo linatoa kauli kadhaa ni lipi?
4. Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Mitume lilikuwa lipi?
5. Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Nisea lilikuwa lipi?
6. Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Chalsedonia lilikuwa lipi?

# NYENZO ZINAZOPENDEKEZWA

Ili kujifunza mengi zaidi kuhusu mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki, tafadhali angalia nyenzo zifuatazo.


## Kitabu cha Mungu

Dockery, David S. *Christian Scripture*. Nashville: Broadman and Holman, 1995.

## Sifa za Mungu

Purkiser, W.T., ed. *Exploring Our Christian Faith*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1960.

Tozer, A. W. *The Knowledge of the Holy*. New York: Harper and Row, 1961.

## Utatu wa Mungu

Morey, Robert. *The Trinity: Evidence and Issues*. Iowa Falls: Word Bible Publishers, 1996.

White, James. *The Forgotten Trinity: Recovering the Heart of Christian Belief*. Minneapolis: Bethany House Publishers, 1998.

## Ubinadamu

Purkiser, W.T., ed. *Exploring Our Christian Faith*. Kansas City, MO: Beacon Hill, 1978. (See Chapter 10: "What is Man?")

## Dhambi

Wesley, John. "The Doctrine of Original Sin," in *The Complete Works of Wesley. Vol. 9*.

Wilcox, Leslie. *Profiles in Wesleyan Theology*. Salem, OH: Schmul Publishing, 1985. (See Chapter 7: "Origin and Nature of Sin," 141-170.)

## Roho

Lewis, C. S. *The Screwtape Letters*. New York: Macmillan Co., 1968.

Wesley, John. "Satan's Devices." *Wesley's 52 Standard Sermons*. Salem, OH: Schmul Publishing, 1988.

## Kristo

Strobel, Lee. *The Case for Christ*. Grand Rapids: Zondervan, 1998.

Zacharias, Ravi. *Jesus Among Other Gods*. Nashville: Word Publishing, 2000.

## Wokovu

Purkiser, W. T., ed. *Exploring Our Christian Faith*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1960. (See Chapter XI and XII: "Man's Predicament," and "The Doctrine of Atonement.")

Wilcox, Leslie. *Profiles in Wesleyan Theology*. Salem, OH: Schmul Publishing, 1985. See Chapters 9-10: "Atonement" and "Conditions of Reconciliation," 171-214.

Wiley, H. Orton and Culbertson, Paul T. *Introduction to Christian Theology*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1946.

## Masuala ya Wokovu

Shank, Robert. *Life in the Son*. Minneapolis: Bethany House Publishers, 1989.

Wiley, H. Orton and Culbertson, Paul T. *Introduction to Christian Theology*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1946.

## Roho Mtakatifu

Carter, Charles. *The Person and Ministry of the Holy Spirit: A Wesleyan Perspective*. Grand Rapids: Baker Book House, 1974.

Murray, Andrew. *Andrew Murray on the Holy Spirit*. New Kensington: Whitaker House, 1998.

## Kanisa

Noll, Mark. *Turning Points*. Grand Rapids: Baker Academic, 1997.

Oden, Thomas. *Life in the Spirit*. Peabody: Prince Press, 2001.

## Hatima ya Milele

Lewis, C. S. “The Weight of Glory,” in *The Weight of Glory and Other Addresses*. New York: Macmillan Publishing, 1980.

Purkiser, W.T., ed. *Exploring Our Christian Faith*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1967. (See Chapter XXVIII, “The Future Life.”)

Wesley, John. “The Great Assize.” *Wesley’s 52 Standard Sermons*. Salem, OH: Schmul Publishing, 1988.

## Matukio ya Mwisho

Ladd, George Eldon. *The Blessed Hope*. Grand Rapids: Eerdmans, 1992.

Wiley, H. Orton & Culbertson, Paul T. *Introduction to Christian Theology*. Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1949.

## Kanuni za Imani za Kale

Gonzalez, Justo L. *The Story of Christianity, Vol. I*. New York: Harper, 2010.

Noll, Mark. *Turning Points: Decisive Moments in the History of Christianity*. Grand Rapids: Baker, 2012.

# REKODI YA MAZOEZI

## JINA LA MWANAFUNZI___________________________

Andika herufi za kwanza za jina la  mwanafunzi baada ya kila zoezi kukamilishwa. Mitihani inachukuliwa kuwa "imekamilishwa" wakati mwanafunzi anapata alama ya 70% au zaidi. Mazoezi yote lazima yakamilishwe kwa mafanikio ili kupokea cheti kutoka kwa Darasa la Kimataifa la Wachungaji.

| SOMO | KIFUNGU | MTIHANI |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| 13 | | |
| 14 | | |
| 15 | | |

| KUFUNDISHA NJE YA DARASA | |
|---|---|
| TAREHE | MAZINGIRA |
| | |
| | |
| | |

Ombi la Cheti cha Ukamilisho kutoka kwa Darasa la Kimataifa la Wachungaji linaweza kukamilishwa kwenye tovuti yetu ya www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kidijitali kutoka kwa rais wa SGC hadi kwa walimu na wawezeshaji wanaokamilisha ombi kwa niaba ya wanafunzi wao.

# MAREJEO YA MAANDIKO

**Mwanzo 1,** 28, 38, 43, 48, 52, 54, 116
**Mwanzo 2,** 38, 125
**Mwanzo 3,** 51, 53, 54, 65, 69, 83, 96, 163
**Mwanzo 6,** 24, 57
**Mwanzo 9,** 48, 80
**Mwanzo 18,** 25
**Mwanzo 19,** 64
**Mwanzo 22,** 83
**Mwanzo 31,** 55
**Mwanzo 41,** 55
**Mwanzo 50,** 29

**Kutoka 3,** 25, 77, 125
**Kutoka 20,** 25, 125
**Kutoka 25,** 63
**Kutoka 29,** 125
**Kutoka 32,** 55
**Kutoka 33,** 13, 25
**Kutoka 34,** 28
**Kutoka 35,** 117
**Kutoka 40,** 125

**Mambo ya Walawi 4,** 55, 58
**Mambo ya Walawi 11,** 126
**Mambo ya Walawi 16,** 125
**Mambo ya Walawi 17,** 80
**Mambo ya Walawi 19,** 126
**Mambo ya Walawi 20,** 126
**Mambo ya Walawi 21,** 126
**Mambo ya Walawi 22,** 126
**Mambo ya Walawi 23,** 125

**Hesabu 23,** 27
**Hesabu 34,** 11
**Hesabu 35,** 11

**Kumbukumbu la Torati 6,** 34
**Kumbukumbu la Torati 9,** 13
**Kumbukumbu la Torati 21,** 80
**Kumbukumbu la Torati 30,** 30, 129
**Kumbukumbu la Torati 32,** 27, 67

**Yoshua 24,** 30, 46, 51

**Waamuzi 3,** 117
**Waamuzi 15,** 117
**Waamuzi 20,** 55

**2 Samweli 7,** 27

**1 Wafalme 8,** 44

**2 Wafalme 3,** 55
**2 Wafalme 19,** 65

**1 Mambo ya Nyakati 13,** 65

**Ayubu 1,** 48, 64, 69, 75
**Ayubu 2,** 69
**Ayubu 33,** 117
**Ayubu 34,** 117
**Ayubu 38,** 64
**Ayubu 42,** 15

**Zaburi 8,** 28, 43, 44, 48
**Zaburi 16,** 149
**Zaburi 19,** 27, 128, 129
**Zaburi 23,** 28
**Zaburi 24,** 126
**Zaburi 34,** 66
**Zaburi 36,** 28
**Zaburi 51,** 54, 55, 57, 95, 96, 129
**Zaburi 58,** 56
**Zaburi 77,** 126
**Zaburi 80,** 64
**Zaburi 85,** 95
**Zaburi 90,** 25
**Zaburi 99,** 27, 126
**Zaburi 102,** 26, 84
**Zaburi 103,** 28, 47
**Zaburi 104,** 27
**Zaburi 106,** 67
**Zaburi 114,** 15
**Zaburi 115,** 25, 29
**Zaburi 119,** 9, 12, 16, 20, 108, 109, 126, 128
**Zaburi 135,** 29
**Zaburi 139,** 26, 31, 48, 113, 115
**Zaburi 147,** 26

**Mithali 9,** 31
**Mithali 30,** 14, 20

**Isaya 1,** 30, 95, 96
**Isaya 5,** 155
**Isaya 6,** 25, 27, 63, 64, 65, 136
**Isaya 7,** 83
**Isaya 9,** 83
**Isaya 14,** 66
**Isaya 31,** 64
**Isaya 37,** 65
**Isaya 40,** 23, 26
**Isaya 42,** 24
**Isaya 44,** 48, 84
**Isaya 46,** 24, 29, 31, 34
**Isaya 55,** 15, 30, 91
**Isaya 61,** 117
**Isaya 66,** 26

**Yeremia 23,** 26, 126
**Yeremia 24,** 55

**Ezekieli 1,** 63, 65
**Ezekieli 10,** 63, 65
**Ezekieli 18,** 30
**Ezekieli 28,** 66

**Danieli 2,** 164
**Danieli 7,** 13, 157
**Danieli 10,** 65, 67
**Danieli 12,** 66

**Nahumu 1,** 24
**Zephaniah 00**
**Sefania 3,** 24

**Malaki 3,** 26

**Mathayo 1,** 53, 55, 56, 74, 83
**Mathayo 3,** 117
**Mathayo 4,** 16, 63, 67

**Mathayo 5,** 11, 15, 20, 28, 150, 152, 155
**Mathayo 6,** 151
**Mathayo 8,** 16, 64
**Mathayo 12,** 64, 71, 140
**Mathayo 13,** 83, 110
**Mathayo 14,** 96
**Mathayo 16,** 139
**Mathayo 17,** 81
**Mathayo 18,** 66, 84
**Mathayo 22,** 58, 64, 129, 131
**Mathayo 24,** 159
**Mathayo 25,** 64, 69, 84, 151, 164
**Mathayo 26,** 158
**Mathayo 28,** 64, 82, 84, 121, 140, 144

**Marko 1,** 35, 47, 85, 90, 116, 159
**Marko 2,** 77
**Marko 4,** 67
**Marko 5,** 15, 68
**Marko 8,** 126
**Marko 9,** 130, 159
**Marko 10,** 130
**Marko 12,** 11
**Marko 13,** 95, 121, 159
**Marko 16,** 90

**Luka 1,** 64, 74, 75, 93, 128
**Luka 2,** 64, 76, 83
**Luka 4,** 67, 131
**Luka 5,** 84
**Luka 7,** 55, 84
**Luka 8,** 15, 17, 71
**Luka 9,** 130, 142
**Luka 10,** 69, 130, 132
**Luka 12,** 115
**Luka 15,** 64, 106
**Luka 16,** 152, 155
**Luka 19,** 96
**Luka 20,** 64
**Luka 21,** 159
**Luka 22,** 67
**Luka 23,** 151
**Luka 24,** 81, 130

**Yohana 1,** 25, 34, 75, 76, 77, 83, 90, 94
**Yohana 2,** 77, 81, 84, 100
**Yohana 3,** 28, 37, 75, 88, 94, 95, 114, 117, 144, 151
**Yohana 4,** 24, 44
**Yohana 5,** 37, 77, 78, 81, 84, 85, 92, 161
**Yohana 6,** 25, 57, 85, 90, 119, 144
**Yohana 8,** 67, 77, 84, 85, 106
**Yohana 10,** 11, 76, 77, 84
**Yohana 11,** 77
**Yohana 12,** 67, 83
**Yohana 14,** 33, 78, 84, 109, 116, 117, 119, 121, 150, 159, 160
**Yohana 14-16,** 40, 116, 130
**Yohana 14-17,** 35
**Yohana 15,** 35, 37, 41, 104, 105, 116, 117, 130
**Yohana 16,** 66, 115, 116, 117, 121, 139, 140, 142
**Yohana 17,** 41, 105, 116, 126, 130
**Yohana 18,** 74
**Yohana 20,** 84, 130

**Matendo 1,** 117, 118, 122, 130, 159
**Matendo 2,** 85, 119, 121, 130, 131, 136
**Matendo 3,** 11, 83, 159
**Matendo 4,** 29, 90, 114, 126
**Matendo 5,** 34, 67, 114, 115, 121
**Matendo 7,** 55, 117
**Matendo 12,** 71
**Matendo 13,** 118, 121, 144
**Matendo 15,** 102, 114, 118, 120
**Matendo 16,** 121
**Matendo 17,** 154
**Matendo 19,** 64
**Matendo 20,** 83, 154
**Matendo 24,** 134
**Matendo 13,** 117
**Matendo 15,** 117
**Matendo 16,** 117

**Warumi 1,** 10, 44, 46, 57, 61, 67, 90, 96
**Warumi 2,** 27, 28, 46, 89
**Warumi 3,** 57, 61, 88, 90, 96
**Warumi 4,** 95, 139
**Warumi 5,** 28, 53, 54, 55, 76, 88, 93
**Warumi 6,** 47, 51, 57, 89, 99, 107, 108, 128, 129, 131, 144
**Warumi 7,** 89
**Warumi 8,** 28, 51, 81, 92, 96, 104, 106, 115, 117, 118, 119, 120, 121, 122, 129
**Warumi 9,** 83
**Warumi 10,** 92
**Warumi 11,** 27, 96
**Warumi 12,** 102, 118, 128, 131, 134, 144
**Warumi 13,** 58, 108
**Warumi 14,** 27
**Warumi 15,** 144

**1 Wakorintho 1,** 87, 95, 126, 127
**1 Wakorintho 2,** 114, 115, 117, 122
**1 Wakorintho 3,** 16, 116, 127, 129, 162
**1 Wakorintho 4,** 118
**1 Wakorintho 5,** 141, 144, 146
**1 Wakorintho 6,** 48, 64, 117, 119, 127, 146, 161
**1 Wakorintho 9,** 109
**1 Wakorintho 10,** 67, 69, 103, 111, 136
**1 Wakorintho 11,** 144
**1 Wakorintho 12,** 38, 114, 118, 119, 121, 122, 140, 146
**1 Wakorintho 13,** 132
**1 Wakorintho 14,** 11, 119, 144
**1 Wakorintho 15,** 47, 54, 76, 81, 151, 159, 160, 164
**1 Wakorintho 16,** 159

**2 Wakorintho 3,** 49, 117
**2 Wakorintho 4,** 67
**2 Wakorintho 5,** 30, 84, 88, 90, 93, 108, 126, 151, 162
**2 Wakorintho 10,** 134
**2 Wakorintho 11,** 67, 71
**2 Wakorintho 12,** 134
**2 Wakorintho 13,** 106, 114, 121

**Wagalatia 1,** 34
**Wagalatia 2,** 89, 108
**Wagalatia 3,** 80, 89, 118
**Wagalatia 4,** 83
**Wagalatia 5,** 61, 115, 118, 119, 120, 122
**Wagalatia 6,** 108, 141, 144

**Waefeso 1,** 28, 29, 41, 82, 93, 94
**Waefeso 2,** 28, 47, 51, 57, 67, 89, 91, 94, 95, 96, 106, 117, 119
**Waefeso 3,** 115, 120, 126, 132, 133, 139

**Waefeso 4,** 38, 49, 57, 108, 114, 118, 121, 140, 141, 142, 144, 146
**Waefeso 5,** 61, 76, 120, 140, 141
**Waefeso 6,** 11, 16, 64, 68, 108, 117, 118

**Wafilipi 1,** 94
**Wafilipi 2,** 74, 75, 83, 114, 118, 158
**Wafilipi 3,** 84, 129, 154

**Wakolosai 1,** 41, 64, 77, 84, 94, 140
**Wakolosai 2,** 66, 69, 81, 82
**Wakolosai 3,** 49

**1 Wathesalonike 1,** 11, 117, 130, 154
**1 Wathesalonike 3,** 105, 130, 132
**1 Wathesalonike 4,** 65, 81, 151, 154, 158, 159, 160
**1 Wathesalonike 5,** 51, 59, 102, 120, 130, 132, 136, 160

**2 Wathesalonike 1,** 152, 159

**1 Timotheo 1,** 25, 133
**1 Timotheo 2,** 30, 154
**1 Timotheo 3,** 66, 84, 133, 141, 144, 168, 175
**1 Timotheo 4,** 67, 90, 175
**1 Timotheo 5,** 144

**2 Timotheo 1,** 133
**2 Timotheo 2,** 67, 158
**2 Timotheo 3,** 11, 12, 18, 19, 20, 21, 95, 115, 141

**Tito 1,** 14, 61, 175
**Tito 2,** 83, 90, 93, 128, 136, 158, 159
**Tito 3,** 117, 128

**Waebrania 1,** 13, 41, 48, 64, 66, 75, 84, 96
**Waebrania 2,** 69, 76, 83, 90
**Waebrania 4,** 26, 76, 83
**Waebrania 5,** 76, 132
**Waebrania 6,** 132
**Waebrania 7,** 76
**Waebrania 8,** 93
**Waebrania 9,** 55, 79, 80, 115, 159
**Waebrania 10,** 76, 80, 83, 95, 110
**Waebrania 11,** 96, 163
**Waebrania 12,** 104
**Waebrania 13,** 84, 144

**Yakobo 1,** 26, 51, 110, 141
**Yakobo 2,** 28, 88, 141, 146
**Yakobo 4,** 56, 58, 61, 68, 69
**Yakobo 5,** 24, 159

**1 Petro 1,** 27, 54, 64, 118, 126, 127, 159
**1 Petro 2,** 16, 108, 140
**1 Petro 4,** 118
**1 Petro 5,** 24, 67, 69, 71, 134

**2 Petro 1,** 11, 13, 14, 16, 110, 115, 117, 159
**2 Petro 2,** 61, 66, 105
**2 Petro 3,** 11, 20, 90, 154, 159, 164

**1 Yohana 1,** 58, 92, 101, 102, 109, 116, 128, 134
**1 Yohana 2,** 28, 78, 90, 92, 93, 100, 117, 159
**1 Yohana 3,** 55, 56, 59, 69, 81, 88, 100, 101, 159, 161
**1 Yohana 4,** 28, 83, 92, 106, 168, 175
**1 Yohana 5,** 76, 99, 100, 101, 108

**2 Yohana ,** 168

**Yuda ,** 57, 65, 66, 67, 144, 173, 175

**Ufunuo 1,** 25, 69, 81, 84, 85, 158
**Ufunuo 2,** 84
**Ufunuo 3,** 30, 105, 110
**Ufunuo 4,** 27, 31
**Ufunuo 5,** 65, 73, 84, 149, 151
**Ufunuo 12,** 66
**Ufunuo 19,** 25, 74
**Ufunuo 20,** 29, 47, 74, 88, 152, 160, 162, 164
**Ufunuo 21,** 96, 149, 150, 151, 163
**Ufunuo 22,** 20, 84, 105, 149, 150, 155, 163

# FARAHASA


## C

**Creeds,** *Somo la 15*

## D

**Dhambi ya Makusudi,** 59

**Dhambi za kutojua,** 59

## H

**Hakikisho,** 92, 99

**Hukumu,** 162, 169

## I

**Imani inayookoa,** 91

**Infirmity,** *Human weakness*

## K

**Kanuni za Imani,** *Somo la 15*

Kanuni ya Imani ya Chalsedonia, 171

Kanuni ya Imani ya Mitume, 169

Kanuni ya Imani ya Nisea, 170

**Karama za Kiroho,** 118

**"Kauli ya Imani"**

Biblia, 19

Dhambi, 60

Hatima ya milele, 154

Kanisa, 145

Kanuni za Imani, 175

Matukio ya Mwisho, 163

Mungu, 30

Roho, 70

Roho Mtakatifu, 120

Ubinadamu, 50

Ushindi dhidi ya dhambi, 110

Utakatifu, 135

Utatu wa Mungu, 40

Wokovu, 94

Yesu, 82

**Kunena kwa lugha,** 118

**Kurudi kwa Yesu,** 160, 163

## M

**Mada za "Makosa ya Kuepuka"**

Dhana Potovu Kuhusu

Maisha ya Kikristo, 49

Masadikisho ya Kibinafsi, 173

Dhana Potovu Kuhusu

Maisha ya Kikristo, 106

Dhana potovu kuhusu baraka

Utatu wa Mungu, 39

Dini bila toba, 94

Kiburi cha Kidhehebu, 173

Kudhoofosha mamlaka ya Biblia, 18

Kusahau Matokeo ya Milele, 154

Kuvutiwa na Ulimwengu wa Roho kwa Njia Mbaya, 69

Kuzingatia mambo ya kidunia, 163

Matarajio duni, 106

Sababu duni za kujifunza Biblia, 18

Ubinafsi wa Kiroho, 145

**Madhehebu Potovu,** 19, 73, 79

**Majaribu,** 103

**Makristo wa uongo,** 73

**Malaika Walioanguka,** 66

**Meza ya Bwana,** 144

**Mfano wa Mungu,** 38

## S

**Sakramenti,** 144

**Shetani,** 66

## T

**Toba,** 90

## U

**Ubatizo,** 144

**Ubinadamu wa Yesu,** 82

**Udhaifu,** *Udhaifu wa kibinadamu*

**Udhaifu wa kibinadamu,** 103–104, 106

**Ufafanuzi wa maneno**

Kufanywa Wana, 94

Kufidia, 93

Kuhesabiwa Haki, 93

Kuongoka, 94

Kutiwa Muhuri, 94

Kuwekwa Huru, 93

Kuzaliwa Upya, 94, 108

Ukombozi, 93

Upatanisho, 93

Upotovu wa kurithi, 102

Uridhisho, 93

Utakaso, 94

**Ufafanuzi wa maneno**

Kanisa, 142

Ubatizo, 144

**Ufafanuzi wa Maneno**

Hali ya kutokuwa na makosa, 14

Kutoweza kuwa na makosa, 14

Uhamasisho, 14

**Ufufuo wa watu wote,** 160

**Ufufuo wa Yesu,** 81

**Ufunuo Maalum,** 10

**Ufunuo wa Jumla,** 10

**Ukiukaji usiokuwa wa makusudi,** 55, 58

**Umoja,** 142–143

**Umwilisho,** 75

**Upatanisho,** 79, 89

**Upotovu wa kurithi,** 56, 102, 106

**Upotovu wa Kurithi,** 128

**Usalama wa milele,** 105

**Ushindi**

dhidi ya dhambi, 120

kupitia nguvu ya Mungu, 68

**Ushindi dhidi ya dhambi**

dhidi ya dhambi, 100–103, 106–108

**Utu wa Roho Mtakatifu,** 114, 120

**Uungu wa Yesu,** 76, 83

## W

**Wenye Dhambi,** 88–89

**Wokovu katika Agano la Kale,** 95

# DARASA LA KIMATAIFA LA WACHUNGAJI
# MAELEZO YA KOZI

## KOZI ZA MISINGI ZA KIKANUNI

### Kanuni za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea kanuni za Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, mwanadamu, dhambi, Kristo, wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na matukio ya mwisho.

### Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na misheni kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Warumi, ikijadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa na utata katika kanisa.

### Eskatolojia

Kozi hii inafundisha kuhusu vitabu vya Biblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu nyingine za maandiko ya kinabii na inatilia mkazo kanuni za msingi kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa milele wa Mungu.

### Kanuni na Matendo ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatazamia na huwezesha katika maisha ya Mkristo.

### Kanuni na Matendo ya Kanisa

Kozi hii inaeleza muundo na mpango wa Mungu kwa ajili ya kanisa na mada za kibiblia kama vile kuwa mshirika katika kanisa, ubatizo, meza ya Bwana, zaka, na uongozi wa kiroho.

## KOZI ZA UCHUNGUZI WA BIBLIA

### Kuchunguza Agano la Kale

Kozi hii inafundisha kuhusu maudhui na mafundisho ya msingi ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

### Kuchunguza Agano Jipya

Kozi hii inafundisha kuhusu maudhui na mafundisho ya msingi ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

### Kanuni za Ufasiri wa Biblia

Kozi hii inafundisha kuhusu kanuni na mbinu za kufasiri Biblia ipasavyo ili kuongoza maisha na uhusiano wetu na Mungu.

## KOZI ZA UINJILISTI NA UANAFUNZI

### Utangulizi wa Utetezi wa Ukristo

Kozi hii inafundisha kuhusu msingi wa kisayansi, kihistoria, na kifalsafa wa mtazamo wa Kikristo, na inaonyesha jinsi imani ya Kikristo inavyopatana na mantiki na uhalisia.

### Dini za Ulimwengu na Madhehebu Potovu

Kozi hii inampa muumini wa kiinjilisti ufahamu wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya kidini.

### Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi

Kozi hii inawasilisha kanuni za kibiblia zinazoongoza mbinu za uinjilisti. Inaeleza aina za uinjilisti na inatoa masomo ya kutumia katika kuwafanya waongofu wapya kuwa wanafunzi.

### Kukua Kiroho

Katika kozi hii wanafunzi hujifunza kuwa na mitazamo ya Yesu, kuhusiana na Mungu jinsi Yesu alivyohusiana na Baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kutekeleza nidhamu za kiroho na za kibinafsi za Yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) iliyoundwa na Yesu.

### Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Matendo

Kozi hii inatumia kanuni za kimaandiko katika matumizi ya pesa, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na nyanja zingine za maisha ya kila siku.

### Ndoa na Familia ya Kikristo

Kozi hii inawasilisha mtazamo wa Kikristo juu ya maendeleo ya binadamu kupitia hatua za maisha na inatumia kanuni za kimaandiko katika majukumu na mahusiano ya familia.

## KOZI ZA UONGOZI WA KIKRISTO

### Uongozi wa Huduma

Kozi hii inatilia mkazo tabia ya Kikristo inapofundisha viongozi kuongoza mashirika katika mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushiriki maono, kuweka malengo, kupanga mikakati, kuchukua hatua, na kupata mafanikio.

### Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inachunguza maisha ya Yesu kama kielelezo cha huduma na uongozi katika karne ya 21.

### Kanuni za Mawasiliano

Kozi hii inafundisha kuhusu theolojia ya mawasiliano, mbinu za kuhutubu kwa ufanisi, na mbinu za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

### Utangulizi wa Ibada ya Kikristo

Kozi hii inaeleza jinsi ibada inavyoathiri nyanja zote za maisha ya muumini na inawasilisha kanuni zinazopaswa kuongoza desturi za ibada za kibinafsi na za kutaniko.

## KOZI ZA HISTORIA YA KANISA

### Uchunguzi wa Historia ya Kanisa I

Kozi hii inaeleza jinsi kanisa lilivyotimiza utume wake na kulinda kanuni za msingi kuanzia kipindi cha kanisa la awali hadi Matengenezo.

### Uchunguzi wa Historia ya Kanisa II

Kozi hii inaeleza jinsi kanisa lilivyopanuka na kukabiliana na changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo hadi nyakati za sasa.